

IMANI NA MATENDO

ELLEN G. WHITE

IMANI NA MATENDO

IMANI NA MATENDO

Hotuba na Makala za Ellen G. White

Masomo kutoka katika Hotuba zake Kumi na Tisa

zilizotolewa Nzima au kwa Sehemu

kuanzia mwaka 1881 na kushuka mpaka mwaka 1902

kwa Mfuatano wa Miaka.

"Imani na matendo ni makasia mawili
ambayo tunapaswa kuyatumia sawasawa"
(Review and Herald, Juni 11, 1901).

"Haki ambayo kwayo sisi tunahesabiwa haki
huwa tunawekewa kwenye akaunti yetu;
Haki ambayo kwayo sisi tunatakaswa
huwa tunapewa kuwa sehemu ya maisha yetu kabisa
kwa kushirikishwa [kuiweka katika matendo yetu].
Ya kwanza ni haki yetu ya kuingilia mbinguni,
Ya pili ni stahili yetu ya kuishi mbinguni."
(Review and Herald, Juni 4, 1895).

Mfasiri: M. Mwamalumbili

Faith and Works - Kiswahili

YALIYOMO

Utangulizi.....
Ellen White Aifafanua Hoja.....
Kipimo cha Utakaso wa Kweli.....
Bwana ni Haki Yetu.....
Ellen White Aweka Msimamo Ulio Wazi.....
Imani na Matendo.....
Onyo Dhidi ya Utakaso wa Uongo.....
Jinsi ya Kujua Kama ni Mungu Anayetuongoza.....
Watu wa Mungu Wazishikao Amri Zake [Kumi].....
Kiwango cha Imani Yetu.....
Taarifa ya E. G. White Kuhusu Itikio Kwa Hotuba Yake ya Ottawa.....
Utii na Utakaso.....
Kuitumia Haki ya Kristo Katika Maisha Yetu.....
Imani na Matendo - Bega kwa Bega.....
Uzoefu wa Maisha ya Haki kwa Imani Wafafanuliwa kwa Muhtasari.....
Huko Ndiko Kuhesabiwa Haki kwa Imani.....
Twakubalika Katika Kristo.....
Ushauri kwa Mchungaji Maarufu Kuhusu Hotuba Yake Juu ya Uhusiano	
Uliopo Kati ya Imani na Matendo.....
Mwanadamu Anaweza Kuwa Mtakatifu Katika Mazingira Yake Kama Vile	
Mungu alivyo Mtakatifu Katika [Mazingira] Yake.....
Maoni Yetu na Desturi Zetu ni Lazima Zipatane na Neno la Mungu.....

UTANGULIZI

Pamoja na hamu inayozidi kuongezeka kuhusu kweli zile kuu za Haki kwa Imani, yaani, kuhesabiwa haki, na utakaso, huenda ikawa ni vyema kumsikiliza zaidi mjumbe wa Bwana kuona alivyozifafanua katika miaka mbalimbali iliyofuatana.

Ili kutoa picha ya mafundisho yake, yaani, masomo haya kumi na nane, kuanzia mwaka 1881 na kushuka chini mpaka mwaka 1902, wafanyakazi wa Maandiko ya Ellen G. White wameyakusanya pamoja humu kwa kufuata mpangilio wake wa miaka bila kuyaweka katika mfumo [mtiririko] wake maalum. Hotuba pamoja na makala zake hufafanua kwa uaminifu kweli hizi za msingi za wokovu ambazo zimejumuishwa katika Sheria na Injili ----- zile zilizo katika gazeti la Review and Herald kwa ajili ya kanisa na zile katika gazeti la Signs of the Times, ambazo zinafaa kwa walimwengu pia. Mambo kadhaa yaliyochaguliwa yanaanza kwa usemi unaofafanua katika jalada kama Manuscript 36, 1890, kutoka katika maandiko yake ya mkono yaliyoandikwa katika kipindi kile cha mgogoro kilichofuatia kikao kile cha mwaka 1888 cha Konferensi Kuu (General Conference), wakati ule, kama alivyoeleza mahali pengine, watu walikuwa katika "hatari kubwa ya kuchukua misimamo potofu" juu ya "imani na matendo" (MS 23, 1891). Katika maandiko yake ya mkono yasiyo na vichwa ya mwaka 1890, alifafanua kwa maneno dhahiri jinsi mambo hayo yalivyo.

Ingawa mara nyingi Ellen White anazipitia njia zile zile kwa wakati tofauti katika kuzishughulikia kweli hizo kuu, maono ya maana yanaweza kupatikana kwa kuzisoma hotuba zake, makala zake, pamoja na maandiko yake ya mkono katika mfululizo wake wa kawaida. Kila moja ni toleo lenye uwiano sawa juu ya somo hilo, ila mara nyingi linakuwa na mkazo wake wa pekee. Masomo yake mengi huonekana katika utimilifu wake, ambapo mengine, kwa ajili ya kuokoa nafasi, yamefupishwa ili yawe na sehemu ile tu ----- kwa kawaida sehemu ile kuu ----- ihusuyo imani na matendo. Vichwa vidogo, na vichwa vya sura vimewekwa katika mifano kadhaa na wale walioyakusanya maandiko hayo na kuyaweka katika kitabu hiki. Hakuna jitihada yo yote iliyofanyika ili kulikamilisha kabisa somo hili. Vitabu vyake pamoja na hotuba zake zingine na makala zake huzishughulikia kweli hizo kuu. Ye yote anayeyachunguza masomo haya ataona waziwazi umuhimu wa somo hili kwa kila Mkristo. Atauona msimamo thabiti wa yule aliyeongozwa hasa na Bwana katika makala zake zifuatazo.

Mpango wa wokovu wa wanadamu waliopotea umejengwa juu ya msingi wa ukubali wa mwanadamu kwa njia ya imani peke yake wa kifo chake Kristo alichokufa badala yetu. Fundisho hili lilifundishwa penye lango la Edeni wakati Adamu na uzao wake walipomchinja mwana-kondoo

wa dhabihu. Lilifundishwa jangwani wakati nyoka yule wa shaba alipoinuliwa juu na Musa, na watu wale waliokuwa na sumu ya nyoka wale wenye sumu katika mishipa yao ya damu waliponywa kwa kuitazama kwa imani ishara ile ya wokovu. Lilifundishwa kwa njia ya mfumo ule wa kafara uliotolewa kwa Israeli. Lilifundishwa na manabii pamoja na mitume. Tena na tena tunafundishwa kwamba wokovu ni kwa neema kwa njia ya imani, na wakati uo huo tunaeleweshwa hivi:

Imani ya kweli inamtegemea kabisa Kristo kwa wokovu, nayo

humwongoza mtu huyo kwenye utii kamili kwa Sheria ya Mungu.

Imani inadhihirishwa kwa matendo (Review and Herald, Oktoba 5, 1886).

Msukumo huo wenye uwiano sawa utaonekana katika maelezo yaliyomo katika kitabu hiki kidogo, yakiwa yamechaguliwa bila kufuata mpangilio [mtiririko] wake.

Kushuka chini kuelekea kwetu katika vizazi vyote, kuanzia kwa Kaini, adui yule mkuu ameupinga mpango mwema wa Mungu kwa kuwaongoza wakazi wa dunia hii kulikubali pendekezo lisemalo kwamba, mwanadamu ambaye amegeuka na kuwa mwenye dhambi kwa kuivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi], analazimika kujipatia sifa na wokovu kwa njia ya matendo yake mwenyewe, kwenda kuhiji mahali panapodhaniwa kuwa ni patakatifu, kufanya kitubio, kulipa fedha katika makasha ya kanisa, au yeye mwenyewe kwa jitihada yake kubwa kujaribu kuishi maisha mema, yaani, maisha ya utauwa.

Uzoefu huu rahisi wa kupokea wokovu kwa imani huonekana kwa wengi kuwa ni rahisi mno, na idadi isiyohesabika ya wale wanaojidai kumfuata Kristo, kusema kweli, wanauchukua msimamo usemao kwamba kwa sehemu moja wokovu ni kwa imani katika kifo chake Kristo juu ya Kalvari na kwa sehemu nyingine hutegemea juhudi ya kibinadamu.

Waadventista Wasabato wale wa kwanza walipoyaona madai ya Sheria ya Mungu isiyobadilika [Amri Kumi], ndipo mielekeo ya kukaza kushika sheria kama njia ya wokovu ilipoanza kuwa tishio, na kwa kipindi fulani ilizaa matunda yasiyofaa kitu katika maisha ya wengi wao. Walakini kule kujua Sheria ya Mungu kwa makini sana kutamwongoza mtu kuachana na dhambi na kuishi maisha matakatifu, yaani, maisha yaliyotakaswa. Huo ndio mwelekeo wa masomo haya juu ya imani na matendo ----- yaani, masomo haya juu ya Sheria na Injili.

Karibu kabisa na katikati ya miongo [miaka kumi] miwili iliyowakilishwa katika kijitabu hiki, kikao cha Konferensi Kuu (General Conference) cha mwaka 1888 kilifanyika kule Minneapolis, Minnesota, kikiwa kimetanguliwa na kikao maalum cha Wachungaji. Wakati wa vikao hivyo mkazo ulitiwa kwa zile kweli za msingi kuhusu haki na imani. Ellen white alikitaja kuwa kilikuwa kikao cha kuzifufua kweli zile zilizokuwa hazizingatiwi kwa sehemu kubwa. Wakati wa kikao kile yeye binafsi hakutoa hotuba yo yote juu ya somo hilo. Mzigo wa hotuba zake ulikuwa juu ya wale waliohudhuria kwamba wapate kuiacha wazi mioyo yao ipate kupokea nuru toka katika Neno la Mungu kama lilivyotolewa na wazee E. J. Waggoner na A. T. Jones. Kuupokea mkazo huo mpya kulikuwa kwa mchanganyiko. Baadhi ya wasikilizaji waliupokea kwa furaha na kwa ukamilifu, na baadhi yao walichukua msimamo usiopendelea upande wo wote. Wengine waliukataa.

Kumbukumbu zinaonyesha wazi kwamba wengi walitoka katika kikao kile wakiwa na uzoefu [wa maisha] mpya, wenye utukufu, katika Kristo Yesu.

Kwa njia ya mahubiri yaliyotolewa makanisani baada ya kikao kile, pamoja na hotuba nyingi zilizotolewa na Ellen White, na makala zake alizoandika yeye mwenyewe, Waadventista kwa kawaida waliongozwa na kuwa na ufahamu ulio wazi zaidi na kuikubali haki kwa imani. Wengi ambao mwanzoni waliikataa dhana ile iliyotolewa pale Minneapolis walishawishika kuikubali.

Kweli zile za msingi zilizohusika katika fundisho hilo la haki kwa imani ni rahisi mno kuzielewa kiasi kwamba hakuna haja ya kitabu cha E. G. White kinacholieleza kwa ukamilifu kabisa ambacho kinatakiwa kuweza kulifafanua. Wazo hilo kuu limeenea katika vitabu vyake vingi, pamoja na vielelezo vinavyotolewa hapa na pale. Alichapisha kujitabu chenye kichwa cha "Kuhesabiwa Haki kwa Imani" katika mwaka ule wa 1893. Hicho kinaonekana katika sehemu kuu ya kurasa hamsini katika kitabu cha Selected Messages, Kitabu cha Kwanza, chini ya kichwa cha "Kristo ni Haki Yetu." Tunapendekeza sehemu hiyo yote isomwe.

Uzoefu huo wa kukaa katika joto la kuikubali haki yake Kristo unaweza kufurahiwa leo na kupotezwa kesho yake kwa njia ya uzembe au kiburi. Ni uzoefu wa mtu mmoja mmoja binafsi wa kukubali kwa njia ile rahisi na kutumaini, na wakati mwingine [uzoefu huo] unaweza kutoweka upesi. Unaweza kutiwa giza kwa njia ya mabishano juu ya hoja ndogo sana za kitheolojia. Ellen White aliliona jambo hilo:

Wengi wanafanya kosa la kujaribu kufafanua kinaganaga
hoja zile zinazohusu tofauti iliyopo kati ya Kuhesabiwa Haki
na Utakaso. Katika kutoa ufafanuzi wa maneno hayo mawili
mara nyingi wanayaingiza mawazo yao wenyewe pamoja na
kukisia kwao. Kwa nini kujaribu kueleza kinaganaga kuliko
Maandiko yaliyovuviwa yanavyoeleza juu ya hoja hiyo kuu ya
Haki kwa Imani? Kwa nini kueleza kila pointi kwa kinaganaga,
kana kwamba wokovu wa mtu ulikuwa unategemea juu ya wote
kuwa na ufahamu unaofanana kabisa juu ya jambo hilo? Wote
hawawezi kuona kwa maono yale yale mamoja (Manuscript 21,
1891; angalia pia katika Seventh-day Adventist Bible Commentary,
Gombo la 6, uk. 1072).

Kwamba njia kadhaa za kuzielewa kweli zilizoelezwa humu na mjumbe huyu wa Bwana zitaweza kulifanya somo hili la maana juu ya Haki kwa Imani kuwa wazi, lenye uwiano sawa, na lisilo na utata wote ndani yake, hilo ndilo tumaini la Wachapishaji pamoja na

WADHAMINI WA MAANDIKO YA ELLEN G. WHITE, WASHINGTON, D.C.,

Desemba 7, 1978.

SURA YA 1

Ellen White Aifafanua Hoja

Maandiko ya kawaida ya mkono yaliyoandikwa mwaka 1890
wakati wa kikao maalum cha Wachungaji kule Battle Creek,
yaliyowekwa katika jalada kama Manuscript 36, 1890, na

kuchapishwa katika gazeti la Review and Herald, Februari 24
na Machi 3, 1977. Usemi huu muhimu wa ufafanuzi ni sehemu
inayofaa ya utangulizi kwa zile hotuba zake kumi na nane
zinazofuata, zilizopangwa kwa mfuatano wa miaka.

Alisema mtume Paulo maneno haya, "Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu?... Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu"

(1 Wakorintho 6:9-11). Kukosekana kwa hali ya kumcha Mungu, utauwa, na utakaso wa mtu yule wa nje huja kwa njia ya kumkana Yesu Kristo aliye haki yetu. Upendo wa Mungu unahitaji kukuzwa daima....

Wakati kundi moja linapotosha fundisho la Kuhesabiwa Haki kwa Imani na kudharau kuyatii masharti yale yaliyowekwa katika Neno la Mungu ----- yasemayo "Mkinipenda, mtazishika amri zangu [kumi]" ----- kuna kosa kubwa kama hilo kwa upande wa wale wanaodai kuziamini na kuzitii amri za Mungu [kumi], lakini ambao wanajiweka katika hali ya upinzani dhidi ya mionzi ya nuru ya thamani ----- kwao ikiwa mipya ----- ambayo inaakisiwa [inaangaza] toka kwenye msalaba ule wa Kalvari. Kundi lile la kwanza haliyaoni maajabu yatokayo katika Sheria ya Mungu [Amri Kumi] yanayowatokea wale wote walio watendaji wa Neno lake. Wale wengine wanalaumu mambo madogo sana na kuyapuuzia mambo mazito zaidi, yaani, rehema na upendo wa Mungu. Kwa upande mwingine, Wanadini kwa kawaida wameitaliki Sheria [Amri Kumi] kutoka kwa Injili, wakati sisi, kwa upande mwingine, tumefanya karibu yayo kwa mtazamo wetu mwingine. Hatujaweka mbele ya watu wetu haki ya Kristo na maana kamili ya mpango wake mkuu wa ukombozi. Tumemwacha nje Kristo na upendo wake usio na kifani, tumeleta nadharia na sababu mbalimbali, na kuhubiri mahubiri yenye hoja ndani yake.

Watu wale ambao hawajaongoka wamesimama kwenye mimbara na kuhutubu. Mioyo yao wenyewe haijapata kamwe kuonja ushuhuda mtamu wa msamaha wa dhambi zao kwa njia ya imani ile inayoshikilia sana na kutumaini. Wanawezaje, basi, kuhubiri juu ya upendo, huruma, na msamaha wa Mungu kwa dhambi zote? Wanawezaje kusema, "Tazama, uishi"? Ukiutazama msalaba wa Kalvari, utakuwa na shauku ya kuubeba msalaba huo. Mtazame Mkombozi wa ulimwengu, ambaye ndani yake ulikaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Je, kuna ye yote awezaye kutazama na kuiona kafara ya Mwana huyo mpendwa wa Mungu, na moyo wake usiweze kuyeyuka na kuvunjika, na yeye mwenyewe kuwa tayari kusalimisha kabisa moyo wake na nafsi yake kwa Mungu?

Hebu jambo hili na liamuliwe kabisa ndani ya kila moyo: Iwapo tunampokea Kristo kama Mkombozi wetu, basi, yatupasa kumkubali kama Mtawala wetu. Hatuwezi kuwa na hakika wala imani kamili ya kumtegemea Kristo kama Mwokozi wetu mpaka hapo tutakapomkiri yeye kama Mfalme wetu na kuwa watiifu kwa amri zake [kumi]. Kwa njia hiyo tutashuhudia utiifu wetu kwa

Mungu. Hapo ndipo tutakuwa na mlio halisi wa imani yetu, maana itakuwa ni imani inayotenda kazi. Itafanya kazi yake kwa upendo. Uiseme [imani hiyo] kutoka ndani ya moyo wako: "Bwana, naamini wewe umenifia ili kunikomboa nafsi yangu. Ikiwa wewe umeweka thamani kama hiyo juu ya nafsi yangu kiasi cha kutoa maisha yako kwa ajili ya maisha yangu, basi, mimi ninaitikia [nakubali]. Nayaweka katika ulinzi wako maisha yangu pamoja na uwezekano wake wote, na udhaifu wangu wote."

Nia [mapenzi] yetu haina budi kuletwa katika mwafaka kamili na nia [mapenzi] ya Mungu. Jambo hilo likifanyika, ndipo hakuna mwonzi wa wote wa nuru unaoangaza moyoni mwako na katika vyumba vya moyo wako utakaoweza kuzuiwa. Moyo hautawekewa kizuizi cho chote kutokana na chuki isiyo na sababu, kwa kuiita nuru kuwa ni giza na giza kuwa ni nuru. Nuru kutoka mbinguni itakaribishwa, na kuwa nuru itakayovijaza vyumba vyote vya moyo wako. Huko ndiko kumwambia Mungu nyimbo tamu.

Kuamini na Kutokuamini

Ni kwa kiasi gani sisi tunaamini toka moyoni mwetu? Mkaribieni Mungu, naye Mungu atawakaribia. Hiyo maana yake ni kuwa na Bwana katika maombi kwa muda mwingi. Wale waliojizoeza wenyewe kushuku na kupendelea kutoamini, wakiruhusu mashaka yaliyojaa maswali katika maisha yao, hutwiwa hatiani na Roho wa Mungu, yaani, wanaona ni wajibu wao kuungama kutokuamini kwao. Ndipo wanafungua mioyo yao kuipokea nuru iliyotumwa kwao na kwa imani wanajitupa wenyewe upande ule wa pili wa mstari toka dhambini kwenda kwenye haki, toka mashakani kwenda kwenye imani. Wanajitoa wakf kabisa kwa Mungu, kuifuata nuru yake badala ya cheche zao walizoziwasha wenyewe. Wanapodumisha kujitoa wakf kwao huko, ndipo watakapoona nuru iliyoongezeka na nuru hiyo itazidi kung'aa zaidi na zaidi mpaka siku ile kamilifu.

Kule kutokuamini kunakohifadhiwa moyoni kuna nguvu ya kuduwaza ndani yake. Mbegu za mashaka ambazo wamekuwa wakizipanda zitaleta mavuno yake, walakini, yawapasa kuendelea kuuchimbua na kuung'oa kila mzizi wa kutokuamini kwao. Mimea hiyo yenye sumu inapong'olewa, inakoma kukua kwa kukosa lishe kwa njia ya neno na tendo. Moyo hauna budi kuwa na mimea ya thamani ya imani na upendo ikipandikizwa katika udongo wa moyo na kutawazwa mle.

Mawazo Yenye Kuchanganyikiwa Juu ya Wokovu

Je, hatuwezi kuelewa kwamba kitu chenye gharama kubwa mno duniani ni dhambi? Ni kwa hasara ya kukosa usafi wa dhamiri, kwa gharama ya kupoteza upendeleo wa Mungu na kuitenga nafsi mbali naye, na hatimaye kuipoteza mbingu. Dhambi ya kumkufuru Roho Mtakatifu wa Mungu na kwenda kinyume naye imewagharimu watu wengi hasara ya nafsi zao.

Ni nani awezaye kutathmini majukumu yatokanayo na mvuto wa kila wakala [mjumbe] wa kibinadamu ambaye Mkombozi wetu amemnunua kwa kujitoa mhanga nafsi yake mwenyewe? Ni mandhari [picha] gani itakayoonekana wakati ule hukumu itakapowekwa na vitabu vitakapofunguliwa kushuhudia wokovu au kupotea kwa watu wote! Itahitajika hukumu isiyokosea ya yule Mmoja aliyepata kuishi katika mwili wa kibinadamu, aliyewapenda binadamu, aliyetoa nafsi yake kwa ajili ya binadamu, ili kutoa mgawo wa mwisho wa thawabu kwa wenye haki watiifu, na adhabu kwa waovu wasiotii, yaani, wasio waaminifu. Mwana wa Mungu amekabidhiwa uwezo wa kufanya tathmini kamilifu ya kila tendo na jukumu la kila mtu mmoja mmoja. Kwa wale ambao wameshiriki katika dhambi za watu wengine na kufanya kinyume na maamuzi ya Mungu, itakuwa ni mandhari ya kuogofya mno.

Hatari hiyo imeonyeshwa kwangu tena na tena kwamba sisi, kama watu wake, tusikaribishe mawazo potofu juu ya Kuhesabiwa Haki kwa Imani. Kwa miaka mingi nimeonyeshwa kwamba Shetani angefanya kazi yake kwa njia ya aina yake ili kuifanya mioyo ichanganyikiwe kuhusu suala hili. Sheria ya Mungu [Amri Kumi] kwa sehemu kubwa imeongelewa sana na kuwekwa mbele ya mikusanyiko ya watu, ambao karibu hawana maarifa kabisa ya kumjua Yesu Kristo wala uhusiano wake alio nao kwa Sheria hiyo kama vile ilivyokuwa ile sadaka ya Kaini. Nimeonyeshwa kuwa wengi wamezuiwa wasiweze kuipokea imani yetu kwa sababu ya mawazo yao yenye utata na kuchanganyikiwa juu ya wokovu, kwa sababu wachungaji wamefanya kazi yao kwa njia isiyo sahihi kuweza kuifikia mioyo hiyo. Jambo hasa lililositizwa katika moyo wangu kwa miaka mingi ni Haki ya Kristo tunayowekwa kwenye akaunti yetu (imputed righteousness). Nimeshangaa sana kwamba jambo hilo halijafanywa kuwa somo mojawapo miongoni mwa hotuba za hadhara katika makanisa yetu katika nchi nzima, wakati jambo hilo limewekwa mbele yangu daima na kusesitizwa, na mimi nimelifanya kuwa somo langu karibu katika kila hotuba na maongezi yangu ambayo nimeyatoa kwa watu.

Katika kuyachunguza maandiko yangu ya miaka kumi na mitano hadi ishirini iliyopita (kabla ya 1890) [nagundua kwamba] yanaliweka suala hilo katika nuru iyo hiyo ----- kwamba wale wanaoingia katika kazi hii nzito, takatifu ya uchungaji wangepewa kwanza maandalizi ya masomo hayo juu ya mafundisho ya Kristo na mitume katika kanuni hai za maisha ya utauwa kwa vitendo. Wanapaswa kuelimishwa juu ya kile kinachofanya imani iwe ya dhati na hai.

Kwa Njia Ya Imani Peke Yake

Wanaume vijana wengi ambao hawauielewi mpango ule wa wokovu na maana ya kuongoka kweli kweli hupelekwa kufanya kazi [ya Mungu]; kwa kweli, wao wanahitaji kuongoka [kwanza]. Tunahitaji kuelimishwa juu ya suala hili, na wachungaji wanahitaji kufunzwa kuongelea zaidi sana juu ya masomo yale yanayofafanua uongofu wa kweli. Wale wote waliobatizwa wanatakiwa kutoa ushuhuda unaonyesha kwamba wameongoka. Hakuna suala lipaswalo kuongelewa kwa dhati

sana, kurudiwa mara kwa mara, au kuimarishwa kwa nguvu katika mioyo ya wote kama lile la kutokuwapo uwezekano wa wote kwa mwanadamu aliyanguka dhambiini kustahili kitu cho chote kwa matendo yake mema sana [anayotenda]. Wokovu ni kwa njia ya imani katika Yesu Kristo peke yake.

Hoja hii inapochunguzwa inaumiza sana moyoni mwetu kuona jinsi yalivyo hafifu mno maneno ya wale ambao wangestahili kuzielewa siri hizi za utauwa. Wanasema bila kutumia busara juu ya mawazo ya ndugu zetu wanaodai kuiamini kweli na kuifundisha kweli hiyo. Wanapungukiwa sana katika kuupata ule ukweli halisi kama ulivyowekwa wazi mbele yangu. Adui ameyatatanisha sana mawazo yao na kuyaingiza katika umande na ukungu wa kidunia, tena inaonekana kana kwamba wametopea katika ufahamu wao huo [potofu] hata imekuwa sehemu ya imani na tabia yao. Ni kuongoka upya tu kunakoweza kuwabadilisha na kuwafanya waweze kuyatupilia mbali mawazo hayo potofu ----- maana ndivyo yanavyoonyeshwa kwangu kuwa ndivyo yalivyo. Wanayang'ang'ania kama mtu yule anayezama anavyoking'ang'ania kifaa kile cha kuokolea maisha [boya] ili kuwafanya wasizame na kuvunjikiwa na imani yao hiyo.

Kristo amenipa mimi maneno haya ya kusema: "Yawapasa ninyi kuzaliwa mara ya pili, vinginevyo hamtaweza kamwe kuingia katika ufalme wa Mungu." Kwa hiyo, wale wote wanaolielewa vizuri suala hili wanapaswa kuweka mbali roho yao iletayo mabishano na [kuanza] kumtafuta Bwana kwa mioyo yao yote. Watamwona Kristo, nao wataweza kuupa uzoefu wa maisha yao ya Kikristo tabia ile ya pekee. Wangepaswa kuliweka suala hili ----- urahisi wa kuwa na utauwa halisi ----- kwa wazi mbele ya watu katika kila hotuba wanayotoa. Jambo hilo litaingia mpaka moyoni mwa kila mtu anayeona njaa na kiu, yaani, anayetamani sana kupata hakika ya tumaini na imani na tegemeo lake kamili kwa Mungu kwa njia ya Bwana Yesu Kristo.

Hebu somo hili na liwekwe wazi na kwa njia rahisi [mbele ya watu] kwamba haiwezekani kufanya lo lote katika msimamo wetu mbele zake Mungu au katika kipawa kile cha Mungu kilichotolewa kwetu kwa kutegemea sifa inayofanywa na kiumbe [mwanadamu]. Endapo imani na matendo vingeweza kumnunulia mtu ye yote kipawa hicho cha wokovu, basi, Muumbaji angekuwa anawajibika kwa kiumbe chake. Hapa ndipo upo mwanya kwa uongo kuweza kukubalika kama ndiyo kweli. Iwapo mtu ye yote anaweza kustahili wokovu kwa jambo lo lote lile awezalo kulifanya, basi, huyo yuko katika hali ile ile moja kama Mkatoliki yule afanyaye kitubio kwa ajili ya dhambi zake. Basi, [kwa maana hiyo] wokovu kwa sehemu fulani ni deni, ambalo linaweza kulipwa kama ujira. Iwapo mtu, kwa matendo yake mema yawayo yote yale, hawezi kustahili kupata wokovu, basi, [kwa maana hiyo] ni lazima [wokovu huo] uwe kabisa kwa neema, ukipokewa na mwenye dhambi kwa sababu anampokea na kumwamini Yesu. Huo ni kipawa kinachotolewa bure kabisa. Kuhesabiwa haki kwa imani kumewekwa mbali kabisa na mabishano yo yote. Na mabishano yote hayo hukomeshwa, mara tu suala hilo linaposuluhishwa kwa kusema kwamba sifa nzuri alizo nazo mwanadamu aliyanguka [dhambiini] zitokanazo na matendo yake mema haziwezi kamwe kumpatia uzima ule wa milele.

Ni Kwa Neema Peke Yake

Nuru aliyonipa Mungu inaliweka somo hili la maana juu ya swali lo lote linaloweza kunijia moyoni mwangu. Kuhesabiwa haki ni kwa neema peke yake, wala hakutokani na matendo mema yo yote ambayo mwanadamu aliyeanguka [dhambini] anaweza kuyatenda. Suala hili limeonyeshwa mbele yangu kwa wazi kwamba [haiwezekani hata kwa] mtu yule aliye tajiri kama anazo fedha na mali nyingi, kisha akatoa sadaka kwa Bwana katika hiyo, halafu mawazo potofu yakaingia ndani yake na kuiharibu sadaka yake hiyo kwa kuwaza kwamba [kwa tendo hilo la kutoa sadaka] amejipatia sifa ya kupata upendeleo kwa Mungu, na ya kwamba Bwana anawajibika kwake kumfikiria kwa upendeleo wa pekee kwa sababu ya toleo [sadaka] hilo.

Pamekuwa na mafundisho kidogo mno yaliyo wazi juu ya suala hili. Mungu amemwazima mwanadamu mali yake mwenyewe kama amana ----- mali ambayo anataka kurudishiwa wakati uongozi wake unapotoa ishara ya kufanya hivyo na kazi ya Mungu inapoitaka [mali hiyo]. Bwana alitoa akili. Alitoa afya na uwezo wa kuchuma mali ya dunia hii. Aliviumba vitu vilivyomo duniani humu. Anaudhirisha uweza wake wa uungu kwa kuendeleza utajiri wote [wa dunia]. Ni matunda yake mwenyewe kutoka katika shamba lake. Alitoa jua, mawingu, manyunyu ya mvua ili kuifanya mimea kusitawi. Ninyi kama watumishi walioajiriwa na Mungu mlikusanya na kuweka ghalani mavuno yake ili kuyatumia kulingana na mahitaji yenu kwa kuwa na uangalifu katika matumizi yenu na kuihodhi mali iliyobakia tayari kutumika hapo Mungu atakapotoa wito wake. Ninyi mwaweza kusema pamoja na Daudi maneno haya, "Kwani vitu vyote vyatoka kwako na katika vitu vyako mwenyewe tumekutolea" (1 Mambo ya Nyakati 29:14). Hivyo basi, utoshelevu wa sifa ya kiumbe [mwanadamu] hauwezi kuwa katika kumrudishia Bwana kile kilicho chake mwenyewe, kwa kuwa sikuzote kilikuwa mali yake mwenyewe ili kutumika kwa uongozi wake kama yeye atakavyoagiza.

Upendeleo wa Mungu Ulipotezwa

Kwa njia ya maasi na ukafiri wake mwanadamu aliupoteza upendeleo wa Mungu; sio zile haki zake, kwa maana asingaliweza kuwa na thamani yo yote isipokuwa ile iliyonunuliwa ndani ya Mwana mpendwa wa Mungu. Pointi hii haina budi kueleweka. Alipoteza manufaa yale ambayo Mungu kwa rehema yake alimpa kama kipawa kitolewacho bure, hazina ile aliyopewa kama amana kutumika kuendeleza kazi yake na utukufu wake, kuwanufaisha viumbe wake aliokuwa amewaumba. Dakika ile kiumbe kile cha Mungu kilipokataa kuzitii sheria zile za ufalme wa Mungu, ikawa ndiyo dakika ile ile aliyogeuka na kuwa mwasi kwa serikali ya Mungu na kujifanya yeye mwenyewe kutostahili kabisa mibaraka yote ambayo Mungu alikuwa amempa kwa upendeleo.

Hiyo ndiyo hali ya wanadamu baada ya mwanadamu huyo kujitenga mwenyewe na Mungu kwa uvunjaji wake wa Sheria [Amri Kumi]. Kuanzia hapo hakustahili tena kuvuta hewa, kupata mwonzi wa jua, wala kula kipande kidogo cha chakula. Na sababu iliyomfanya mwanadamu asiangamizwe papo hapo ilitokana na Mungu kumpenda yeye sana hata akatoa kipawa cha Mwanawe mpendwa ili asipate adhabu ya uasi [dhambi] wake. Kristo alitoa pendekezo lake

kwamba yeye atakuwa Mdhamini wake na Badala yake huyo mwanadamu, ili mwanadamu huyo, kwa neema isiyo na kifani, apate nafasi nyingine ya kupimwa ----- muda wa majaribio wa pili ---- - akiwa na onyo la uzoefu ule wa Adamu na Hawa ili asipate kuivunja Sheria ya Mungu katika kipawa cha mwanga wa jua na kipawa cha chakula, ni lazima, kwa upande wake mwanadamu, pawepo na hali ya kusujudu kwa shukrani mbele zake Mungu akikiri kwamba vitu vyote hutoka kwake Mungu. Cho chote kinachorudishwa kwake [Mungu] ni mali yake mwenyewe yule aliyekitoa.

Mwanadamu aliivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi], na kwa njia ya Mkombozi ahadi mpya na zenye nguvu zikatolewa kwa msingi tofauti. Mibaraka yote ni lazima ije kupitia kwa yule Mpatanishi [Kristo]. Basi, kila mmoja katika familia hii ya kibinadamu amekabidhiwa kabisa mikononi mwake Kristo, pamoja na vitu vyote tulivyo navyo ----- kiwe ni kipawa cha fedha, nyumba, mashamba, uwezo wa kufikiri, nguvu za mwili, au talanta za akili ----- katika maisha haya ya sasa, na mibaraka ile katika maisha yale ya baadaye, vimewekwa mikononi mwetu kama hazina zake Mungu ili zipate kutumika kwa uaminifu kwa manufaa ya mwanadamu. Kila kipawa tulicho nacho kimepigwa muhuri wa msalaba wake, tena kina sura yake, na juu yake kimeandikwa jina la Yesu Kristo. Vitu vyote vyatoka kwa Mungu. Kuanzia manufaa yaliyo madogo sana mpaka kwenye mbaraka mkubwa sana, vyote vinatiririka kuja kwetu kwa njia ya Mfereji ule Mmoja [Kristo] ----- Upatanishi ule usiokuwa wa kibinadamu ulionyunziwa damu ile iliyo ya thamani mno kupita makadirio yote kwa sababu ilikuwa ndio uzima wa Mungu ndani ya Mwanawe.

Sasa basi, hakuna mtu ye yote awezaye kumpa Mungu kitu cho chote ambacho si chake [Mungu] tayari. Zingatia maneno haya: "Kwani vitu vyote vyatoka kwako na katika vitu vyako mwenyewe tumekutolea" (1 Mambo ya Nyakati 29:14). Jambo hilo ni lazima liwekwe wazi mbele ya watu ko kote tuendako ----- kwamba sisi hatuna kitu cho chote cha kwetu, hatuwezi kutoa cho chote chenye thamani, kwa kazi yetu, kwa imani yetu, ambacho hatujakipokea kwanza toka kwa Mungu, na ambavyo kwa wakati wo wote ule anaweza kuweka mikono yake juu yake na kusema, Hivi ni Vyangu ----- vipawa na mibaraka na mali ambayo ni mimi niliyekukabidhi, si kwa ajili ya wewe kujitajirisha mwenyewe, bali kwa ajili ya kuviendeleza kwa busara ili vilete manufaa kwa ulimwengu.

Vyote Ni Vyake Mungu

Viumbe vyote ni mali ya Mungu. Bwana, kwa kutomjali mwanadamu, angeweza kuikomesha punzi yake mara moja. Jinsi [mwanadamu] alivyo kimwili na vyote alivyo navyo vimefungamana na Mungu. Ulimwengu mzima ni wake Mungu. Nyumba alizo nazo mwanadamu, mapato yake binafsi, cho chote kile kilicho cha thamani kwake au kinachong'aa sana, ni kipaji cha Mungu mwenyewe. Vyote ni vipawa vyake vinavyopaswa kurudishwa kwa Mungu ili kusaidia kuuadilisha moyo wa mwanadamu. Sadaka nzuri sana zinaweza kuwekwa juu ya madhabahu ya Mungu, ndipo wanadamu watamsifu, watamtukuza, na kumhimidi Mpaji huyo kwa sababu ya ukarimu wake. Kwa vitu gani? "Kwani vitu vyote vyatoka kwako na katika vitu vyako mwenyewe tumekutolea" (1 Mambo ya Nyakati 29:14). Hakuna kazi yo yote [tendo lo lote] anayofanya

mwanadamu inayoweza kumpatia sifa ya kupewa upendo wa Mungu unaosomehe, bali upendo wa Mungu ukiujaza moyo wa mtu huyo utamwongoza kufanya mambo yale ambayo sikuzote yalitakiwa kwake na Mungu, tena kwamba apate kuyafanya hayo kwa furaha. Amefanya yale tu ambayo wajibu uliyataka daima kutoka kwake.

Malaika wa Mungu mbinguni ambao hawajapata kamwe kuanguka dhambini wanafanya mapenzi yake daima. Katika yote yale wanayofanya katika safari zao za rehema zenye shughuli nyingi wanapokuja katika dunia yetu ili kutulinda, kutuongoza, na kuilinda kazi ya uumbaji ya Mungu kwa vizazi vyote ----- yaani, kwa wenye haki pamoja na wasio haki ----- kwa kweli [wanadamu] wanaweza kusema, "Vyote vyatoka kwako. Katika vitu vyako mwenyewe tunakutolea." Laiti kama jicho la mwanadamu lingaliweza kuona picha kidogo tu ya huduma ile wanayotoa malaika! Laiti kama mawazo [ya mwanadamu] yangeweza kuzingatia na kutafakari sana juu ya huduma nyingi na tukufu za wale malaika wa Mungu na kuona mapambano wanayopambana nayo kwa ajili ya kuwalinda wanadamu, kuwaongoza, kuwaleta kwa Mungu, na kuwatoa katika mitego ya Shetani. Mwenendo wake ungekuwa tofauti jinsi gani, yaani, ile hisia yake ya kidini!

Sifa ya Kiumbe

Mijadala inaweza kuendeshwa na wanadamu walio na hali ya kufa wakitetea kwa nguvu zote sifa za kiumbe [mwanadamu], na kila mtu akijitahidi kushinda, lakini wao hawajui kabisa ya kwamba wakati wote huo, kwa kanuni na tabia, wanaueleza vibaya ukweli huo kama ulivyo ndani ya Yesu. Wamo katika ukungu wa kuchanganyikiwa. Wanahitaji upendo wa Mungu ambao unawakilishwa kama dhahabu iliyosafishwa kwa moto; wanahitaji mavazi meupe ya tabia takatifu ya Kristo; tena wanahitaji dawa ya macho kutoka mbinguni ili wapate kuona kwa mshangao jinsi sifa ya kiumbe [mwanadamu] isivyofaa kabisa katika kuwapatia ujira wa uzima wa milele. Huenda ikawapo bidii ya kufanya kazi na upendo wenye nguvu sana, mafanikio ya hali ya juu na bora ya akili, upana wa kuelewa mambo, na kujidhalilisha kabisa, yote hayo yakiwa yamewekwa miguuni pake Mkombozi wetu; walakini hakuna hata chembe moja ndogo inayoongezeka kuliko neema ile na talanta ile iliyotolewa kwanza na Mungu. Yapasa kisitolewe kitu cho chote kilicho pungufu kuliko wajibu huo unavyoagiza, wala hapawezi kuwa na chembe moja ndogo inayotolewa kuliko ile waliyokwisha kupokea kwanza; tena vyote vinapaswa kuwekwa juu ya moto wa haki yake Kristo ili kuvitakasa na kuondoa harufu yake ya kidunia kabla havijapanda katika wingu la moshi wa uvumba kwenda kwa Yehova Mkuu na kukubalika kama harufu nzuri inayopendeza.

Najiuliza, Hivi nawezaje mimi kulieleza jambo hili kama lilivyo hasa? Bwana Yesu anatoa uweza wote, neema yote, toba yote, mwelekeo wote mzuri, msamaha wote wa dhambi, anapoitoa haki yake kwa mwanadamu ili aishikilie kwa njia ya imani iliyo hai ----- ambayo pia ni kipawa cha Mungu. Iwapo ungekusanya mahali pamoja kila kitu kilicho chema na kitakatifu na kizuri na cha kupendeza ambacho kimo ndani ya mwanadamu, kisha ukatoa somo hilo kwa malaika wa Mungu kuonyesha kwamba hao wanayo sehemu ya kufanya katika wokovu wa roho yake ya kibinadamu au katika kumpatia sifa, basi, pendekezo lako hilo lingekataliwa na kuonekana kama ni

usaliti. Wakiwa wanasimama mbele za Muumbaji wao na kuutazama utukufu ule usio na kifani unaomzunguka yeye, wanamtazama yule Mwana-Kondoo wa Mungu aliyetolewa tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu huu, apate kuishi maisha yale ya kudhalilishwa, kukataliwa na wanadamu wenye dhambi, na kusulibiwa. Ni nani awezaye kukadiria thamani ya kafara hiyo isiyo na kikomo!

Kwa ajili yetu Kristo akawa maskini, ili sisi kwa umaskini wake tupate kuwa matajiri. Basi, matendo yo yote ambayo mwanadamu anaweza kumtendea Mungu yatakuwa na upungufu mno kuliko si kitu. Dua zangu zinakubalika tu kwa sababu zinawekwa juu ya haki yake Kristo. Wazo la kufanya tendo lo lote ili kustahili neema yake ya msamaha ni kosa tangu mwanzo mpaka mwisho wake. "Bwana, mkononi mwangu sina kitu cho chote cha thamani cha kukupa, ni msalaba wako tu ninaoung'ang'ania."

Kile Asichoweza Kufanya Mwanadamu

Mwanadamu hawezi kutenda matendo yo yote yanayostahili sifa yawezayo kumpa yeye utukufu uwao wote. Watu wana mazoea ya kuwatukuza wanadamu na kuwasifu sana. Jambo hilo linanifanya nitetemeke kuona na kusikia habari zake, maana nimeonyeshwa si watu wachache ambao maisha yao ya nyumbani mwao na kazi ile inayofanyika ndani ya mioyo ya watu hao hao huonyesha kuwa wamejawa na uchoyo. Ni wafisadi, wachafu, waovu; na hakuna cho chote kinachotokana na matendo yao yote kinachoweza kuwainua juu kwa Mungu, kwa maana mambo yote wanayofanya ni chukizo mbele ya macho yake. Kuongoka kweli kweli hakuwezi kuwapo bila kuachana kabisa na dhambi, na kuitambua tabia mbaya sana ya dhambi. Kwa utambuzi mkali ambao haujafikiwa kamwe na macho ya wanadamu wanaokufa, malaika wa Mungu wanatambua kwamba viumbe wale wanaozuiwa na mivuto yao iletayo uharibifu, wale walio na mioyo michafu na mikono michafu, wanaamua mwisho wao wa milele, tena wanafahamu kidogo mno kile kinachoifanya dhambi iwe dhambi na tiba yake.

Tunasikia mambo mengi yakihubiriwa kuhusu kuongoka kwa mtu ambayo si ya kweli. Watu wanafundishwa kufikiri kwamba kama mtu akitubu, basi, atasamehewa, wakidhani kwamba toba ndiyo njia, yaani, ndio mlango wa kuingilia mbinguni; kwamba kuna thamani ya hakika kwa kiasi fulani katika toba kuweza kumnunulia [mtu huyo] msamaha. Je! mwanadamu anaweza kutubu yeye mwenyewe? Ni sawa tu na vile mtu asivyoweza kujisamehe mwenyewe. Machozi, kupiga kite sana, maazimio ----- hayo yote ni kutumia ipasavyo uwezo ule ambao Mungu alimpa mwanadamu, bali kule kugeuka kutoka dhambini kwa kufanya matengenezo katika maisha ya mtu ni uweza wa Mungu. Iko wapi basi, sifa ndani ya mwanadamu inayomwezesha kujipatia wokovu wake, au kuweka mbele za Mungu kitu fulani cha thamani, kilicho bora kabisa? Je, kule kutoa sadaka ya fedha, nyumba, mashamba, kunaweza kukuweka wewe katika orodha ya wale wanaostahili? Haiwezekani kabisa!

Hatari ipo katika kukufikiria Kuhesabiwa Haki kwa Imani kama ni kuweka sifa ya mtu [matendo yake] juu ya imani. Unapoipokea haki ya Kristo kama kipawa kinachotolewa bure, hapo ndipo unapohesabiwa haki bure kwa njia ya ukombozi wake Kristo. Imani ni nini? "Ni kuwa na

hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya [ushahidi wa] mambo yasiyoonekana" (Waebrania 11:1, KJV). Ni ufahamu wetu wa kuyakubali maneno ya Mungu unaoufunga moyo katika kujitoa wakf kwa hiari na kumtumikia Mungu, yeye aliyetupa ufahamu huo, yeye aliyegusa moyo wetu, yeye aliyevuta kwanza moyo wetu upate kumtazama Kristo juu ya msalaba ule wa Kalvari. Imani ni kumpa Mungu uwezo wetu wa ufahamu, kuusalimisha kabisa moyo wetu na mapenzi yetu kwa Mungu, na kumfanya Kristo kuwa [ndiye] mlango wa pekee wa kuingilia katika ufalme ule wa mbinguni.

Watu wanapojifunza kwamba hawawezi kujipatia haki kwa matendo yao mema wanayotenda wenyewe, tena wanapomtazama Yesu Kristo kwa tegemeo thabiti na kamili kama ndiye tumaini lao la pekee, hapo ndipo nafsi haitaweza kujitokeza sana, wala Yesu hataonekana kidogo sana ndani yao. Nafsi na miili yetu hunajisiwa na kuchafuliwa na dhambi, moyo hutengwa mbali na Mungu, lakini wengi wanazidi kujitahidi kuzitegemea nguvu zao za kibinadamu ili kujipatia wokovu kwa kutenda matendo mema. Wanafikiri kwamba Yesu atafanya sehemu fulani katika kuwaokoa; na wao watapaswa kufanya sehemu iliyosalia. Wanahitaji kuiona kwa imani haki ya Kristo kuwa ndilo tumaini lao la pekee kwa wakati huu na kwa milele zote.

Mungu Hufanya Kazi, na Mwanadamu Hufanya Kazi

Mungu amewapa wanadamu akili na uwezo. Mungu hufanya kazi kwa kushirikiana na vipawa vile alivyompa mwanadamu, na mwanadamu naye, akiwa mshirika wa tabia ile ya uungu na kufanya kazi ya Kristo, anaweza kuwa mshindi na kujipatia uzima ule wa milele. Bwana hatushauri sisi kwamba anaweza kufanya kazi ile aliyompa mwanadamu uwezo wa kuifanya. Sehemu ile inayomhusu mwanadamu ni lazima aifanye. Yampasa kuwa mtenda kazi pamoja na Mungu, akijitia nira pamoja na Kristo, akijifunza upole wake, unyenyekevu wake wa moyo. Mungu ndiye mwenye uwezo wa kuongoza mambo yote. Anagawa vipawa; mwanadamu anavipokea na kuvitendea kazi kwa uwezo wa neema ya Kristo akiwa kama mjumbe wake aliye hai.

"Ninyi ni shamba la Mungu" (1 Wakorintho 3:9). Moyo hauna budi kufanyiwa kazi, kudhibitiwa, kulimwa kwa plau, kupigwa haro, kupandwa mbegu, ili upate kutoa mavuno yake kwa Mungu kwa njia ya matendo mema. "[Ninyi] ni jengo la Mungu." Wewe huwezi kujijenga mwenyewe. Uwezo uko nje yako mwenyewe ambao unapaswa kufanya kazi ya ujenzi wa kanisa, ukiweka tofali juu ya tofali, ukishirikiana sikuzote na uwezo wa akili na nguvu alizotoa Mungu kwa mwanadamu. Mkombozi sharti apate makao ndani ya jengo lake hilo. Mungu hufanya kazi na mwanadamu hufanya kazi. Daima panatakiwa kuwapo na upokeaji wa vipawa vya Mungu ili pawe na utoaji huria wa vipawa hivyo. Ni kuendelea daima kupokea, kisha kurudisha [kutoa]. Mungu amefanya mpango kwamba nafsi ipate kupokea lishe kutoka kwake, ili kutolewa tena katika utekelezaji wa makusudi yake. Ili paweze kuwapo na mtiririko wa kutoa, hapana budi kuwapo na upokeaji wa uungu kwenda kwa ubinadamu. "Nitakaa ndani yao, na kati [ndani] yao nitatembea" (2 Wakorintho 6:16).

Hekalu la mwili linapaswa kuwekwa wakf, takatifu, safi, na bila kunajisiwa. Lazima uwepo ushirikiano wa pande mbili ambao kwa huo uwezo wote ni wa Mungu na utukufu wote ni wa Mungu. Uwajibikaji unabaki kwetu. Yatupasa kupokea kwa njia ya mawazo yetu na hisia zetu, ili tupate kutoa kwa njia ya usemi wetu. Sheria ya utendaji wa binadamu pamoja na Mungu humfanya mpokeaji huyo kuwa mtenda kazi pamoja na Mungu. Inamleta mwanadamu mahali ambapo akiunganika na Mungu, anaweza kufanya kazi zake [matendo yake] Mungu. Ubinadamu huugusa ubinadamu. Uweza wa Mungu na utendaji wa kibinadamu vikiunganishwa pamoja vitaleta mafanikio kamili, maana ni ile haki yake Kristo inayokamilisha kila kitu.

Uweza wa Mungu kwa Kazi Zile Zinahohitaji Uweza wa Mungu

Sababu inayowafanya wengi kushindwa kuwa watenda kazi wenye mafanikio ni kwamba wanatenda kazi yao kana kwamba Mungu alikuwa anawategemea wao, na kwamba, wao ndio wanaopaswa kumshauri Mungu katika kile anachochagua kuwafanyia, badala ya wao kumtegemea Mungu. Wanauweka kando uweza wa Mungu na kushindwa kuifanya kazi ile inayohitaji uweza wa Mungu. Wakati huo wote wao wanazitegemea nguvu zao wenyewe pamoja na nguvu za kibinadamu za ndugu zao. Wana ufinyu [wa mawazo] ndani yao, nao sikuzote wanatoa maamuzi yao kulingana na ufahamu wao wa kibinadamu wenye upeo mfupi. Wanahitaji kutiwa moyo, kwa maana hawana uwezo wa wote kutoka juu. Mungu anatupa sisi miili yetu, nguvu ya ubongo, wakati na nafasi nzuri ambazo tunaweza kuzitumia kufanya kazi yake. Inatakiwa kwamba vyote hivyo vitumike kwa juhudi kubwa. Ubinadamu na uungu vikiunganishwa pamoja, ndipo wewe unaweza kufanikiwa kuifanya kazi ile ambayo itadumu milele zote. Wanadamu wanapofikiri kwamba Mungu amefanya makosa katika mambo yao, kila mmoja peke yake, na kujichagulia kazi yao wenyewe, watakutana na masikitiko yatakawavunja moyo.

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu" (Waefeso 2:8). Hapa upo ukweli ambao utalifunua wazi somo hili katika mioyo yenu iwapo ninyi hamtaifunga ili ipate kupokea mionzi ya nuru hiyo. Uzima wa milele ni kipawa cha Mungu. Jambo hilo linauweka nje ya uwezekano wetu wa kufanya kazi ili kuupata kwa sababu ni wa Mungu. Ni lazima uwe kipawa hasa. Kama kipawa unapaswa kupokewa kwa imani, ndipo shukrani na sifa zitakapotolewa kwa Mungu. Imani thabiti haitamfanya mtu ye yote kuingia katika ushupavu wa dini [kushikilia imani ya dini bila kutumia akili], wala kutenda kama mtumwa yule mlegevu. Ni uwezo wa Shetani unaoduwaza unaowafanya watu kujiangalia wenyewe badala ya kumwangukia Yesu. Haki ya Kristo haina budi kututangulia iwapo utukufu wa Bwana utatufuata nyuma yetu na kutulinda. Kama tunafanya mapenzi ya Mungu, tunaweza kupokea mibaraka mikubwa kama vipawa vya Mungu vinavyotolewa bure kwetu, lakini si kwa sababu ya wema wa wote ulio ndani yetu; huo hauna thamani yo yote. Fanyeni kazi ya Mungu, nanyi mtafanikiwa na kuwa zaidi ya washindi kwa njia yake yeye aliyetupenda na kutoa maisha yake kwa ajili yetu, ili sisi tupate uzima na wokovu ndani ya Yesu Kristo.

SURA YA 2

Kipimo cha Utakaso wa Kweli

Makala ya Review and Herald, iliyochapishwa

Machi 8, 1881.

"Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa;

nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe

mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana

wetu Yesu Kristo" (1 Wathesalonike 5:23).

Utakaso unapatikana tu kwa njia ya utii kwa mapenzi ya Mungu. Wengi ambao kwa makusudi kabisa wanaikanyaga Sheria ya Yehova [Amri Kumi] chini ya miguu yao hudai kwamba wanao utakatifu wa moyo wao na utakaso wa maisha yao. Walakini hawanayo kabisa maarifa ya wokovu wa Mungu wala ya Sheria yake [Amri Kumi]. Wanasimama katika safu za yule mwasi mkuu [Shetani]. Yeye anaipiga vita Sheria ya Mungu [Amri Kumi], ambayo ndiyo msingi wa serikali ya Mungu mbinguni na duniani. Watu hao wanafanya kazi ile ile kama bwana wao alivyokwisha kufanya kwa kujaribu kuitangua Sheria ya Mungu takatifu [Amri Kumi]. Hakuna mvunja Sheria [mwasi] ye yote atakayeruhusiwa kuingia mbinguni; kwa sababu yule ambaye hapo mwanzo alikuwa mtakatifu na mwenye cheo kikubwa mno, kerubi yule afunikaye, alitupwa chini kwa uasi wake dhidi ya Serikali ya Mungu.

Kwa walio wengi, utakaso ni haki ya mtu mwenyewe tu. Lakini bado watu hao wanadai kwa ukakamavu kabisa kwamba Yesu ni Mwokozi na Mtakasaji wao. Ni kudanganyika sana kulikoje huko! Je! Mwana wa Mungu atamtakasa mtu yule anayeivunja Sheria ya Baba yake [Amri Kumi] ----- Sheria ile ile Kristo aliyokuja kuitukuza na kuiadhimisha? [Isaya 42:21]. Yeye mwenyewe anatoa ushuhuda huu, anasema, "Mimi ni[me]zishika amri [kumi] za Baba yangu" [Yohana 15:10]. Mungu hatashusha chini kiwango cha Sheria yake [Amri Kumi] ili kukidhi kipimo kile cha mwanadamu kisichokuwa kikamilifu; wala mwanadamu hawezi kutimiza madai ya Sheria ile takatifu [Amri Kumi] pasipokuwa na toba kwa Mungu na imani kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

"Na kama mtu akitenda dhambi [akivunja Amri Kumi - Yak.2:10-12] tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki" (1 Yohana 2:1). Walakini, Mungu hakumtoa Mwanawe kuishi maisha yale yaliyojaa mateso na aibu na kufa kifo kile cha aibu ili kumwacha mwanadamu huru kuvunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Ni wenye nguvu nyingi sana uwezo wa madanganyo ya Shetani hata wengi wameongozwa kuuangalia upatanisho wa Kristo kama hauna faida sana. Kristo alikufa kwa sababu hapakuwa na tumaini jingine lo lote kwa mwasi [yule anayevunja Sheria]. Huyu [mwasi] angeweza kujaribu kuitunza Sheria ya Mungu [Amri Kumi] hapo baadaye; lakini deni alilokuwa nalo kwa wakati uliopita lingeweza kuendelea kubaki, na Sheria hiyo ni lazima imhukumu kufa. Kristo alikuja kulilipa deni lile kwa ajili ya mwenye dhambi ambalo lilikuwa haliwezekani kwake mwenyewe kujilipia. Hivyo, kwa njia ya kafara ya upatanisho wake Kristo, mwanadamu mwenye dhambi alipewa nafasi nyingine ya majaribio.

Madanganyo ya Shetani

Ni madanganyo ya Shetani kusema kwamba kifo chake Kristo kilileta neema ambayo ilichukua mahali pa Sheria. Kifo cha Yesu hakikubadili wala kutangua wala kupunguza hata kwa kiwango kidogo sana Sheria ile ya Amri Kumi. Neema ile ya thamani iliyotolewa kwa wanadamu kwa njia ya damu yake Mwokozi inaithibitisha Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Tangu kuanguka kwa mwanadamu [dhambini], Serikali ya Mungu ya Kimaadili [Amri Kumi] na Neema yake haviwezi kutenganishwa kamwe. Vinakwenda bega kwa bega katika mpango [wa wokovu] aliouweka Mungu kwa vizazi vyote. "Fadhili [Neema] na Kweli [Sheria - Zab.119:142] zimekutana [msalabani], Haki [Sheria - Rum.7:12] na Amani [Msamaha au Neema - Lk.2:14] zimebusiana [msalabani]" (Zaburi 85:10).

Yesu, aliye Badala yetu, alikubali kuchukua adhabu ya Sheria ile iliyovunjwa kwa niaba ya mwanadamu [aliyeivunja]. Aliufunika uungu wake kwa ubinadamu na kwa njia hiyo akawa Mwana wa Adamu, Mwokozi na Mkombozi. Ukweli wa kifo cha Mwana wa Mungu huyo mpendwa kwa ajili ya kumkomboa mwanadamu huonyesha jinsi Sheria hiyo ya Mungu [Amri Kumi] isivyoweza kubadilika kamwe. Kwa mtazamo wa mwenye dhambi, ingekuwa rahisi jinsi gani kwa Mungu kuweza kuifutilia mbali Sheria yake [Amri Kumi], na kwa njia hiyo kuweka njia ambayo kwayo wanadamu wangeweza kuokolewa na Kristo angeweza kubaki kule kule mbinguni! Fundisho lile linalofundisha kwamba kwa njia ya neema hiyo watu wanao uhuru wa kuivunja Sheria [Amri Kumi] ni imani potofu ya kufisha. Kila mtu atakayeivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi] ni mwenye dhambi, na hakuna watu wanaoweza kutakaswa wakati wanaendelea kuishi katika dhambi [kuvunja Sheria] inayojulikana.

Kujidhili kwake na maumivu makali sana aliyopata Mwana mpendwa wa Mungu hakuvistahimili ili kumnunulia mwanadamu uhuru wa kuivunja Sheria ya Baba yake [Amri Kumi] na baadaye [kumruhusu mwanadamu huyo mwasi] kukaa pamoja na Kristo katika kiti chake cha enzi. Ilikuwa ni kwa madhumuni kwamba kwa njia ya wema wake [Kristo] na kutumia toba na imani mwenye dhambi huyo aliye na hatia kubwa sana apate kupokea msamaha na kupewa nguvu za kumwezesha kuishi maisha yale ya utii. Mwenye dhambi huyo haokolewi pamoja na dhambi zake, bali anaokolewa kutoka katika dhambi zake.

Maana ya Dhambi

Nafsi yake ni lazima ionekane kuwa ina hatia ya dhambi kabla mwenye dhambi huyo hajasikia shauku ya kuja kwa Kristo. "Maana dhambi ni uvunjaji wa Sheria [Amri Kumi]"

(1 Yohana 3:4, AJKK). "Walakini singalitambua dhambi ila kwa Sheria [Amri Kumi]" (Warumi 7:7). Amri ilipokuja katika dhamiri ya Paulo, dhambi ilihuika, naye akafa. Akajiona mwenyewe kuwa amekwisha hukumiwa kwa Sheria ile ya Mungu [Amri Kumi]. Mwenye dhambi hawezi kujua hatia yake mpaka hapo atakapoelewa dhambi hiyo inatokana [inasababishwa] na nini. Haiwezekani kabisa kwa mtu ye yote kupata uzoefu wa utakaso ule wa Biblia wakati yeye anaendelea kusadiki kwamba kama anamwamini Kristo, basi, si kitu kwake kama anaitii Sheria ya Mungu [Amri Kumi] au kama anaivunja.

Wale wanaodai kuitunza Sheria ya Mungu [Amri Kumi] wakati moyoni mwao bado wanajifurahisha na dhambi wanashutumiwa na yule Shahidi wa Kweli [Kristo]. Wanadai kwamba wao ni matajiri katika maarifa ya kujua ile kweli [Yoh.17:17; Zab. 119:142]; lakini hawapatani na kanuni zake takatifu. Kweli hiyo haiwatakasi maisha yao. Neno la Mungu linatangaza kwamba yule anayekiri kwamba anazishika amri [kumi] ambaye maisha yake yanapingana na imani yake ni kipofu, mnyonge, maskini, na uchi.

Sheria ya Mungu ni kioo kinachomwonyesha kabisa jinsi mtu huyo alivyo, na kuweka mbele yake kielelezo sahihi. Wengine watageukia kando na kuisahau picha hiyo, wakati wengine watatumia lugha ya matusi dhidi ya Sheria hiyo [Amri Kumi], kana kwamba hiyo ndiyo njia ya kuziponya kasoro walizo nazo katika tabia yao. Bado wengine wanaoshutumiwa na Sheria hiyo watatubia maasi yao na kwa njia ya imani katika wema wake Kristo, watakamilisha ujenzi wa tabia yao ya Kikristo. [Yakobo 1:22-25.]

Watahukumiwa kwa Nuru ile Wanayoikataa

Ulimwengu wote una hatia mbele za macho ya Mungu kwa kuivunja Sheria yake [Amri Kumi]. Kwa kuwa watu wengi sana wataendelea kuivunja, na hivyo kuendelea kuwa na uadui na Mungu, hiyo haiwezi kuwa sababu ya kuwafanya wasiweze kuungama wenyewe ya kuwa wanayo hatia, kisha kugeuka na kuwa watii. Kwa mtazamaji wa viwi hivi tu [asiyechunguza mambo], watu wale ambao kwa asili ni [wamezaliwa] wema, wameelimika na kuwa waungwana, wanaweza kuonekana kwake kuwa ni wakamilifu katika maisha yao. "Maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali BWANA huutazama moyo" (1 Samweli 16:7). Hakuna mtu ye yote anayeweza kuona ufalme wa mbinguni, isipokuwa kama kweli zile zinazoleta uzima zilizo katika Neno la Mungu, zinapoingia katika dhamiri yake, zinapokewa naye kwa ufahamu, kisha zinatekelezwa kwa uaminifu katika maisha ya mtu huyo. Kwa wengine, kweli hizo zina mvuto fulani kwa sababu ni mpya kwao, lakini hazikubaliki kwao kama Neno la Mungu. Wale wasioipokea nuru inapoletwa mbele yao watahukumiwa kwayo.

Katika kila kusanyiko la watu humu nchini kuna watu ambao hawajaridhika, wenye njaa na kiu kwa ajili ya kupata wokovu. Mchana na usiku mzigo ulio ndani ya mioyo yao ni huu, Nifanye nini nipate kuokoka? Wanasikiliza kwa shauku mahubiri yanayopendwa na watu wengi, wakitumainia kujifunza jinsi wanavyoweza kuhesabiwa haki mbele zake Mungu. Lakini mara nyingi mno wanasikia tu hotuba inayofurahisha, yaani, ufasaha wa maneno. Kuna mioyo yenye huzuni na

yenye kukata tamaa katika kila kusanyiko la kidini. Mchungaji huwaambia wasikilizaji wake kwamba hawawezi kuishika Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. "Haimfungi mtu ye yote siku zetu hizi," anasema. "Ni lazima mmwamini Kristo; yeye atawaokoa; aminini tu." Hivyo anawafundisha kuifanya hisia yao [msisimko] kuwa ndicho kigezo, wala hawapi imani iliyojengwa juu ya akili. Mchungaji huyo anaweza kudai kwamba yeye ni mkweli kabisa, walakini anajaribu kuinyamazisha dhamiri inayosumbuka ndani [ya watu hao] kwa kuipa tumaini la uongo.

Sumu ya Kiroho Iliyopakwa Sukari kwa Nje

Wengi wanashawishika kufikiri kwamba wao wako katika njia ile iendayo mbinguni ati kwa sababu tu wanakiri kumwamini Kristo, wakati wanaikataa Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Lakini hao watagundua mwishoni kwamba walikuwa katika njia ile iendayo kwenye uharibifu badala ya ile iendayo mbinguni. Sumu ya kiroho inapakwa sukari kwa nje kwa njia ya fundisho [potofu] la utakaso, na kuwapa watu waimeze. Maelfu kwa hamu kubwa huimeza, wakijisikia ya kwamba ikiwa wao ni waaminifu tu katika imani yao hiyo, basi, watakuwa salama. Lakini uaminifu huo hautaweza kamwe kuligeuza kosa [fundisho potofu] kuwa kweli. Mtu anaweza kumeza sumu, akidhani kwamba ni chakula; lakini uaminifu wake [katika kuamini hivyo] hautaweza kumwokoia kutokana na madhara ya sumu hiyo aliyomeza.

Mungu ametupa sisi Neno lake kuwa kiongozi wetu. Kristo amesema, "Mwayachunguza [Chunguzeni] Maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia" (Yohana 5:39, KJV). Aliwaombea wanafunzi wake, akisema, "Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli" (Yohana 17:17). Paulo asema hivi, "Kweli, mimi mwenyewe naliona ndani ya nafsi yangu kwamba yanipasa kutenda mambo mengi yaliyopingamana na jina lake Yesu Mnazareti" (Matendo ya Mitume 26:9). Lakini imani hiyo haikuifanya njia yake iwe ya kweli. Paulo alipoipokea injili ya Yesu Kristo, ilimfanya kiumbe kipya. Alibadilika kabisa; kweli iliyopandwa moyoni mwake ilimpatia imani ile na ujasiri ule aliokuwa nao kama mfuasi wake Kristo hata upinzani wo wote ule haukuweza kumtikisa, wala mateso kumtia hofu.

Watu wanaweza kutoa udhuru wo wote wanaotaka kama sababu ya kuikataa Sheria ya Mungu [Amri Kumi]; lakini hakuna udhuru wo wote utakaokubaliwa katika siku ile ya hukumu [ambayo inaendelea hivi sasa huko mbinguni]. Wale wanaoshindana na Mungu na kuzitia nguvu nafsi zao zenye hatia kwa kuendelea kuivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi], hivi punde watalazimika kukabiliana na Mtoa-Sheria Mkuu juu ya Sheria yake iliyoovunjwa [Amri Kumi].

Siku ya kisasi cha Mungu yaja ----- siku ile ya ghadhabu yake kali sana. Ni nani atakayesimama [ata kayestahimili] siku ile ya kuja kwake? Wanadamu wameifanya mioyo yao kuwa migumu kwa kumpinga Roho wa Mungu, lakini mishale ya ghadhabu yake itapenya mpaka ndani ya mioyo yao mahali pale iliposhindwa kupenya mishale ile ya kuwathibitishia dhambi zao. Si mbali kuanzia sasa Mungu ataondoka kuja kumshughulikia mwenye dhambi [yule asiyetaka kutubu]. Je! yule mchungaji wake wa uongo atamkinga mvunja sheria [Amri Kumi] huyo siku ile?

Je! anaweza kusamehewa yule aliyeandamana na mkutano katika njia ile ya uasi? [Kutoka 23:2].
Je! kule kupendwa [kwa fundisho hilo potofu] na watu wengi au idadi kubwa [ya waumini] kutaweza kumfanya mtu ye yote asiwe na hatia? Haya ndiyo maswali ambayo wale walio wavivu na wasiojali [kusoma Neno la Mungu kujua linavyosema juu ya Sheria yake] wanapaswa kuyatafakari na kukata shauri wao wenyewe juu ya kile watakachofanya.

SURA YA 3

Kristo Ni Haki Yetu

(Hotuba ya mwaka 1883)

Hotuba ya asubuhi kwa wachungaji wakati wa kikao cha Konferensi Kuu (General Conference) kilichofanyika katika mwezi wa Novemba, 1883 kule Battle Creek, Michigan. Imechapishwa katika kitabu cha Gospel Workers [Wajumbe wa Injili] (toleo la 1892, uk. 411-415), na katika kitabu cha kwanza cha Selected Messages, uk. 350-354.

"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote"

(1 Yohana 1:9).

Mungu anataka sisi tuziungame dhambi zetu na kuinyenyekeza mioyo yetu mbele zake; lakini kwa wakati uo huo inatupasa kumwamini yeye kama Baba yetu mwenye huruma, ambaye hatawaacha wale wanaomtumainia. Wengi wetu tunatembea kwa kuona wala sio kwa imani. Tunayaamini mambo yale yanayoonekana, lakini hatuzithamini ahadi zake za thamani zilizotolewa kwetu katika Neno la Mungu; na, hata hivyo, hatuwezi kumvunjia Mungu heshima kwa dhahiri kuliko kujionyesha kwake kuwa sisi hatuyaamini yale asemayo kwetu, na kwamba tuna mashaka iwapo Bwana anasema kweli kwetu ama anatudanganya.

Mungu hatuachi [hatutupi] kwa sababu ya dhambi zetu. Twaweza kufanya makosa [dhambi] na kumhuzunisha Roho wake, lakini tunapotubu na kuja kwake tukiwa na mioyo iliyopondeka, yeye hawezi kukataa kutupokea. Kuna vipingamizi vinavyopaswa kuondolewa. Hisia mbaya zimetunzwa moyoni, na kumekuwapo na kiburi, roho ya kujitosheleza wenyewe, kukosa uvumilivu, na manung'uniko. Hayo yote yanatutenga sisi mbali na Mungu. Ni lazima dhambi zetu ziungamwe; ni lazima pawepo na kazi ya neema yenye kina ndani ya moyo wetu. Wale wanaojiona kuwa wadhaifu na wenye kukata tamaa wanaweza kuwa watu wa Mungu wenye nguvu, tena wanaweza kumfanyia Bwana kazi nzuri sana. Lakini hawana budi kufanya kazi hiyo wakiwa na msimamo wa hali ya juu; wanapaswa kuongozwa na makusudi ya moyo yasiyokuwa na ubinafsi wo wote ndani yake.

Wema Wake Kristo Ndilo Tumaini Letu La Pekee

Yatupasa kujifunza katika shule yake Kristo. Hakuna kitu cho chote, isipokuwa haki yake, kinachoweza kutustahilisha sisi kupata mmojawapo wa mibaraka ya agano lake la neema. Kwa muda mrefu tumetamani na kujaribu kuipata mibaraka hiyo, lakini hatujaipata kwa sababu tumekuwa na wazo kwamba sisi tungeweza kufanya kitu fulani kustahili kuipata. Hatujaacha kujiangalia wenyewe na kuangalia mbali, na kuamini kwamba Yesu ni Mwokozi wetu aliye hai. Haitupasi kujifikiria wenyewe kwamba matendo yetu mema na wema wetu vitatuokoa; neema yake Kristo ndilo tumaini letu la pekee la wokovu. Kupitia kwa nabii wake Bwana anaahidi, akisema, "Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie BWANA, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa" (Isaya 55:7). Yatupasa kuiamini ahadi hiyo iliyo wazi, wala tusikubali kuwa na hisia [kujisikia ndani yetu] badala ya kuwa na imani. Tunapomtumainia Mungu kabisa, tunapotegemea wema wake Yesu kama Mwokozi wetu anayesamehe dhambi, ndipo tutaweza kupokea msaada wote tunaoweza kuutaka.

Tunajiangalia wenyewe, kana kwamba sisi tulikuwa na uwezo wa kujiokoa wenyewe; lakini Yesu alikuja kwa ajili yetu kwa sababu hatukuwa na uwezo wo wote wa kufanya hivyo. Ndani yake ndimo tumaini letu limo, kuhesabiwa haki kwetu, yaani, haki yetu. Tusife moyo na kuogopa kwamba hatuna Mwokozi ama kwamba hana mawazo ya rehema kwetu. Wakati huu huu anaendelea na kazi kwa ajili yetu, akitualika kwenda kwake katika udhaifu wetu na kuokolewa. Tunamwaibisha sana kwa kutokuamini kwetu. Inashangaza sana jinsi tunavyomtendea Rafiki yetu aliye mwema sana kwetu, jinsi tulivyo na imani ndogo sana kwake yeye awezaye kutuokoa kabisa na yeye aliyetupa sisi ushahidi wa kila namna wa upendo wake mkuu.

Enyi ndugu zangu, je! mnatazamia kwamba wema wenu utawapatia sifa ya kupata upendeleo wa Mungu, mkifikiri kwamba inawapasa kuwa huru mbali na dhambi kabla hamjautegemea uweza wake wa kuokoa? Kama hilo ndilo pambano linaloendelea moyoni mwenu, naogopa kwamba hamtapata nguvu yo yote na hatimaye mtakatishwa tamaa.

Tazama Uishi

Kule jangwani, Bwana alipoziruhusu zile nyoka zenye sumu kuwauma Waisraeli wale waasi, Musa aliagizwa kumwinua [juu ya mti] nyoka yule wa shaba na kuwaamuru wote waliojeruhiwa kumtazama [nyoka yule] na kuishi. Lakini wengi hawakuona msaada wo wote katika uponyaji ule uliowekwa na Mbingu. Wafu na wale waliokuwa wanaendelea kufa waliwazunguka pande zote, nao walijua kwamba bila msaada wa Mungu mwisho wao ulikuwa umefika hakika; lakini wao wakaendelea [tu] kuomboleza kwa ajili ya majeraha yao, maumivu yao, na kifo chao kilichokuwa

cha hakika, mpaka nguvu zao zilipowaishia kabisa, na macho yao yakawa na utando kama kioo, ambapo wangeweza kupata uponyaji papo hapo [kwa kutazama tu].

"Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye" (Yohana 3:14,15). Iwapo wewe unazitambua dhambi zako, basi, usitumie nguvu zako zote kuomboleza juu yake, lakini tazama uishi. Yesu peke yake ndiye Mwokozi wetu; na japokuwa mamilioni wanaohitaji kuponywa wataukataa msaada wake huo alioutoa, hakuna hata mmoja anayeutumainia wema wake [Kristo] atakayeachwa aangamie. Tunapotambua udhaifu wetu pasipo kuwa na Kristo, basi, hatupaswi kukata tamaa; yatupasa kumtegemea Mwokozi yule aliyesulibiwa na kufufuka. Wewe uliye maskini, uliye mgonjwa wa dhambi, uliyekata tamaa, tazama uishi. Yesu ametoa ahadi katika neno lake; atawaokoa wale wote wanaokwenda kwake.

Njoo kwa Yesu, upokee raha na pumziko. Unaweza kuupokea mbaraka huo hata sasa hivi. Shetani anakushawishi akikuambia kwamba wewe u dhaifu wala huwezi kujiletea mbaraka huo mwenyewe. Ni kweli; wewe u dhaifu. Lakini mwinue Yesu juu mbele yake [Shetani], ukisema: "Ninaye Mwokozi aliyefufuka. Yeye ndiye ninayemtumainia, naye hatavumilia kuniacha mimi nikiwa nimefadhaika. Katika jina lake mimi naushangilia ushindi. Yeye ndiye haki yangu na kilemba [taji] cha furaha yangu." Hebu na asiwepo ye yote hapa anayeona kwamba shauri lake halina matumaini yo yote, kwa maana hivyo sivyo lilivyo. Unaweza kujiona kuwa wewe u mwenye dhambi wala huna la kufanya kabisa, lakini ni kwa sababu iyo hiyo wewe unamhitaji Mwokozi. Kama wewe unazo dhambi unazotakiwa kuziungama, basi, usipoteze wakati. Dakika hizi ulizo nazo ni za thamani sana kwako. "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohana 1:9). Wale walio na njaa na kiu ya haki watashibishwa, maana Yesu ameahidi hivyo. Ni Mwokozi wa thamani! Mikono yake imenyoshwa ili kutupokea, na moyo wake mkuu wa upendo unangojea kutubariki.

Wengine wanaonekana kujisikia kwamba ni lazima wawe katika majaribio [wajitahidi sana kupata ushindi] na waweze kumthibitishia Bwana kwamba wamefanya matengenezo, kabla hawajaanza kuudai mbaraka huo. Lakini wapendwa hao wanaweza kuudai mbaraka huo hata sasa hivi. Wanapaswa kuwa na neema yake, yaani, Roho wake Kristo, kuwasaidia katika udhaifu wao, vinginevyo, hawawezi kujenga tabia yao ya Kikristo. Yesu anapenda kutuona sisi tukija kwake jinsi tulivyo ----- yaani, tukiwa wenye dhambi, dhaifu, na wenye kumtegemea yeye.

Toba ni Kipawa cha Mungu

Toba, pamoja na msamaha, ni kipawa cha Mungu kwa njia ya Kristo. Ni kwa njia ya mvuto wa Roho Mtakatifu sisi tunahakikishiwa dhambi zetu na kusikia haja yetu ya kupata msamaha wake. Hakuna awezaye kusamehewa isipokuwa yule tu aliye na moyo wenye toba; lakini ni ile neema ya Mungu inayoufanya moyo upate kutubu. Yeye anaujua udhaifu wetu wote pamoja na upungufu wetu wote, yeye ndiye atakayetusaidia.

Baadhi ya wale wanaokuja kwa Mungu kwa njia ya toba na maungamo, na hata kuamini kwamba dhambi zao zimesamehewa, bado wanashindwa kudai ahadi za Mungu kama iwapasavyo. Hawaoni kwamba Yesu ni Mwokozi wao aliyepo wakati wote; wala hawako tayari kuziweka nafsi zao katika utunzaji wake, wala kumtegemea kwamba ataikamilisha kazi ile ya neema iliyoanza mioyoni mwao. Wanapofikiri kwamba wanajikabidhi kwa Mungu, kuna hali kubwa ya kujitegemea wenyewe. Wako watu walio waaminifu ambao kwa sehemu fulani wanajitegemea wenyewe. Hawamwangelii Mungu ili kulindwa kwa uweza wake, bali wanategemea kuwa macho kwao dhidi ya majaribu na kufanya wajibu fulani uwapasao ili wapate kukubaliwa naye. Hakuna ushindi wo wote kwa walio na imani kama hiyo. Watu hao wanasumbuka bure kufanya kazi hiyo; nafsi zao zimo katika utumwa daima, wala hawapati raha mpaka hapo watakapoiweka mizigo yao miguuni pake Yesu.

Ipo haja ya kukesha daima na kuwa na bidii katika kumcha Mungu kwa upendo, lakini mambo hayo yatakuja yenyewe wakati mtu huyo atakapolindwa kwa uweza wa Mungu kwa njia ya imani. Sisi hatuwezi kufanya neno lo lote, yaani, hatuwezi kabisa kufanya neno lo lote, litakalotupatia sifa ya kupewa upendeleo wa Mungu. Haitupasi kabisa kujitegemea wenyewe au kuyategemea matendo yetu mema; lakini sisi, kama viumbe vinavyofanya makosa na dhambi, tunapokuja kwake Kristo, tunaweza kupata pumziko katika pendo lake. Mungu atamkubali kila mmoja anayekuja kwake akiutumainia kabisa wema ule wa Mwokozi yule aliyesulibiwa. Upendo utabubujika moyoni mwake. Huenda pasiwe na hisia ya [kujisikia] furaha ndani yake, lakini limo tumaini la kudumu, lenye kuleta amani. Kila mzigo unakuwa mwepesi; kwa sababu nira ile anayoiweka Kristo juu yetu ni nyepesi. Wajibu hugeuka na kuwa furaha, na kujitolea mhangana kunageuka na kuwa raha. Njia ambayo hapo kwanza ilionekana kuwa imefunikwa na giza sasa inang'aa kwa miali itokayo kwa lile Jua la Haki [Kristo]. Huko ndiko kwenda katika nuru kama Kristo alivyo katika nuru.

SURA YA 4

Ellen White

Aweka Msimamo Ulio Wazi

Sehemu ya hotuba yake iliyotolewa kule Worcester,

Massachusetts, Julai 31, 1885, yenye kichwa hiki:

"Kipimo Sahihi cha Haki." Ilichapishwa katika

gazeti la Review and Herald la Agosti 25, 1885.

Swali linalopaswa kuulizwa sasa ni hili, Je! wale wanaokiri kuwa ni wafuasi wake Kristo wanatimiza masharti ambayo kwayo mbaraka huo umetamkwa? Je! wanajitenga kiroho na kimatendo na ulimwengu huu? Ni vigumu jinsi gani kutoka na kujitenga na mazoea pamoja na desturi za ulimwengu huu! Walakini tujihadhari Shetani asipate kutushawishi kwa werevu wake na kutudanganya kwa maonyesho yake [miujiza] ya uongo. Mambo yale ya milele yanahusika hapa.

Madai ya Mungu ni lazima yachukue nafasi ya kwanza; matakwa yake hayana budi kupewa kipaumbele mawazoni mwetu.

Kila mtoto wa Adamu aliyeanguka [dhambini] anapaswa kuwa mtiifu kwa matakwa yote ya Mungu kwa neema yake Kristo inayobadilisha maisha yetu. Wengi hufumba macho yao wasitake kuyaangalia mafundisho ya Neno lake yaliyo dhahiri kabisa kwa sababu msalaba unasimama [ukiwakabili] moja kwa moja mbele ya njia yao. Kama watapaswa kuubeba, basi, wataonekana kuwa ni watu wa pekee [wasiokuwa wa kawaida] katika macho ya ulimwengu huu; nao wanasitaita na kuona mashaka na kutafuta udhuru fulani ambao kwa huo wanaweza kuukwepa msalaba huo. Shetani yu tayari wakati wote, naye anawapa sababu za kuaminika kwa nini isingekuwa vizuri sana kwao kulitii Neno la Mungu kama linavyosomeka. Hivyo ndivyo watu wanavyodanganyika na kuangamia.

Madanganyo Yanayofanikiwa

Mojawapo la madanganyo ya Shetani yanayofanikiwa sana ni lile la kuwafanya watu wote madai kwamba wao wametakaswa, wakati ule ule wanapoishi kama waasi kwa amri [kumi] za Mungu. Hao wanaelezwa na Yesu kama ni wale watakaosema, "Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?"

Naam, wale wanaodai kwamba wametakaswa wana maneno mengi ya kusema juu ya kuokolewa kwa damu ya Yesu, lakini utakaso wao hautokani na ile kweli kama ilivyo ndani ya Yesu. Wakati ule ule wanapodai kumwamini, na kuonekana wakifanya miujiza mingi kwa jina lake, wanaidharau Sheria ya Baba yake [Amri Kumi] na kutumika kama mawakala wa yule adui mkuu wa wanadamu na kuendeleza kazi ile aliyoianza kule Edeni, yaani, ile ya kutoa udhuru unaonekana kama ni wa kweli ili wasiweze kumtii Mungu kwa ukamilifu. Kazi yao ya kuwaongoza watu kumvunjia Mungu heshima yake kwa kuidharau Sheria yake [Amri Kumi] siku moja itafunuliwa mbele yao pamoja na matokeo yake halisi.

Masharti ya uzima wa milele yameelezwa kwa wazi kabisa katika Neno la Mungu hata hakuna haja kwa mtu ye yote kupotea, isipokuwa kama wao wenyewe wanachagua mafundisho hayo potofu badala ya ile kweli kwa sababu mioyo yao ambayo haijatakaswa inapenda giza kuliko nuru.

Mwana-sheria yule aliyekuja kwa Yesu kumwuliza swali hili, "Nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" alifikiri kwamba atamnasa Kristo, lakini Yesu alimtupia mzigo huo mwana-sheria yule. "Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje? Akajibu akasema, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako." Ndipo Kristo akamwambia, "Umejibu vema; fanya hivi nawe utaishi" (Luka 10:25-28). Maneno haya yanakidhi kesi za watu wote. Je! tuko tayari kutimiza masharti yake? Je! tutamtii Mungu na kuzishika amri zake [kumi]? Je! tutakuwa watendaji wa Neno wala si wasikilizaji tu? Sheria ya Mungu haibadiliki, tena ni thabiti kama ilivyo tabia yake. Yo yote yale wanadamu wanayoweza kusema au kutenda ili kuitangua

[kuzifutilia mbali Amri Kumi], hayawezi kuyageuza madai yake [sheria hiyo], wala kuwaachilia huru ili wasiwajibike kuitii.

Tunahitaji kuelimishwa na Mbingu kila siku; tunapaswa kuomba kama alivyofanya Daudi, aliposema, "Unifumbue macho yangu niyatazame maajabu yatokayo katika Sheria yako [Amri Kumi]" (Zaburi 119:18). Mungu atakuwa na watu wake ambao wataitetea heshima yake kwa kuziheshimu amri zake zote [kumi]; na amri zake [kumi] si nzito, si kongwa la utumwa. Daudi, katika siku zake, aliomba, akisema, "Wakati umewadia BWANA atende kazi; kwa kuwa wameitangua Sheria yako [Amri Kumi]" (fungu la 126).

Hakuna hata mmoja wetu awezaye kumudu kumwaibisha Mungu kwa kuendelea kuivunja Sheria yake [Amri Kumi]. Kuiacha Biblia na kujitoa wenyewe kutafuta hazina ya ulimwengu huu ni hasara kubwa mno isiyokadirika. Umilele peke yake utafunua mhanga mkubwa waliojitolea wengi ili kuipata heshima ya ulimwengu huu pamoja na manufaa ya ulimwengu huu, kwa hasara ya nafsi zao, yaani, hasara ya utajiri ule wa milele. Wangaliweza kuupata uzima unaolingana na kiwango kile cha uzima alio nao Mungu; kwa maana Yesu alikufa ili kuwaletea karibu sana nao mibaraka ile na hazina zile za mbinguni, ili wasihesabiwe katika kipimo kile cha juu cha umilele kuwa wao ni maskini na wanyonge, tena kuwa ni watu wanaotia huruma.

Hakuna Anayeingia Huko Kama Yeye ni Mvunjaji wa Amri [Kumi]

Hakuna ye yote aliyepata nuru ya ile kweli atakayeingia katika mji ule wa Mungu kama yeye ni mvunjaji wa amri [kumi]. Sheria yake [Amri Kumi] ndiyo msingi wa Serikali yake hapa duniani na kule mbinguni. Kama wameikanyaga Sheria yake [Amri Kumi] chini ya miguu yao hapa duniani na kuidharau wakati wanajua kile wanachofanya, basi, hao hawataweza kuchukuliwa kwenda mbinguni ili wakaendeleo kufanya kazi ile ile [ya kuvunja amri kumi] kule; hapatakuwa na badiliko lo lote katika tabia [aliyo nayo mtu] hapo Yesu atakapokuja.

Kazi ya kujenga tabia nzuri inapaswa kuendelea katika saa hizi za muda wetu wa majaribio. Siku kwa siku matendo yao yanaandikwa katika vitabu vile vya mbinguni, na katika siku ile kuu ya Mungu watalipwa kwa kadiri matendo yao yalivyokuwa. Wakati huo ndipo itakapoonekana ni nani anayeupokea mbaraka huo. "Heri wale wazishikao amri zake [kumi], wawe na haki kuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake" (Ufunuo 22:14, Tafsiri ya toleo la King James).

Wale wanaofanya mashambulio juu ya Sheria ya Mungu [Amri Kumi] wanapigana vita na Mungu Mwenyewe; na wengi waliojazwa na uchungu mwingi sana dhidi ya watu wa Mungu wazishikao amri zake [kumi], ndio wanaojisifu mno kuwa wao ndio wanaoishi maisha matakatifu, yaani, maisha yasiyokuwa na dhambi. Jambo hilo linaweza kuelezwa kwa njia moja tu: hao hawana kioo [Amri Kumi - Yak.1:22-25; 2:10-12] kile cha kujiangalia wenyewe na kugundua kasoro walizo nazo katika tabia zao. Si Yusufu, wala Danieli, wala mmojawapo wa mitume wale aliyedai kwamba hana dhambi. Watu wale walioishi karibu sana na Mungu, watu ambao

wangeweza kujitoa maisha yao mhanga kuliko kumtendea dhambi kwa makusudi, watu wale ambao Mungu amewaheshimu kwa kuwapa nuru yake ya mbinguni pamoja na uweza wake, wamekiri wenyewe ya kuwa wao ni wenye dhambi, wasiostahili kupata fadhili zake kuu. Wameuona udhaifu wao, nao, wakiwa na huzuni kwa ajili ya dhambi zao, wamejaribu kukiiga Kiolezo chao, yaani, Yesu Kristo.

Makundi ni Mawili Tu ----- Watiifu na Waasi

Patakuwa na makundi mawili tu duniani, watoto watiifu wa Mungu na wale wasiotii [waasi]. Siku moja Kristo aliweka mbele ya wasikilizaji wake kazi ile ya hukumu kwa maneno haya: "Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake; na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi; atawaweka kondoo mkono wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa kushoto.

"Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninyweshwa; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika, nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia.

"Ndipo wenye haki watakomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunyweshwa? Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia? Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi" (Mathayo 25:31-40).

Kwa njia hiyo Kristo anayafungamanisha mambo yake yale ayapendayo pamoja na yale ya wanadamu wale wanaoteseka. Kila jambo wanalotendewa watoto wake analiangalia kama ametendewa yeye mwenyewe. Wale wanaodai kwamba wanao utakaso wa kisasa wangeweza kuja mbele yake wakijisifu, na kusema, "Bwana, Bwana, hivi wewe hutujui sisi? Je, hatujafanya unabii kwa jina lako? na katika jina lako kutoa pepo? na katika jina lako kufanya miujiza mingi?" Watu hao wanaoelezwa hapo, wanaotoa madai hayo ya kinafiki, wakionekana kumweka Yesu katika mambo yao yote waliyofanya, ni mfano halisi wa wale wanaodai kwamba wanao utakaso wa kisasa lakini ambao wanaendelea kuipiga vita Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Kristo anawaita hao kuwa ni watenda maovu kwa sababu hao ni wadanganyifu, wakiwa wamejivika mavazi ya haki kuficha tabia zao zenye kombo [kasoro], yaani, uovu ule walio nao ndani ya mioyo yao michafu.

Shetani ameshuka chini katika siku hizi za mwisho akiwa na madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea. Kwa uweza wa fahari yake ya kishetani anafanya miujiza mbele ya macho ya manabii hao wa uongo, na mbele ya wanadamu, akidai kwamba yeye ni Kristo Mwenyewe hasa. Shetani anawapa uwezo wake wale wanaomsaidia katika kuendeleza madanganyo yake; kwa hiyo, wale wanaodai kuwa wanao uwezo mkubwa wa Mungu wanaweza kutambuliwa tu kwa njia ya

yule Mgunduzi Mkuu [Msema Kweli], yaani, Sheria yake Yehova [Amri Kumi - Kutoka 20:3-17; Isaya 8:20]. Bwana anatumia sisi kwamba kama pangukuwa na uwezekano [hao manabii wa uongo] wangeweza kuwadanganya yamkini hata walio wateule. Mavazi ya kondoo waliyojivika yanaonekana kuwa ni mavazi yao halisi, yaani, halisi kabisa kiasi kwamba mbwa-mwitu huyo anaweza kutambuliwa tu kama sisi tutakwenda kuiangalia Kanuni ile Kuu ya Maadili [Amri Kumi] na kuwagundua kuwa hao ni wavunjaji wa Sheria ya Yehova [Amri Kumi].

Kama Ulipata Kuwapo Wakati ni SASA

Kama ulipata kuwapo wakati ambapo sisi tulihitaji sana imani na ufahamu wa kiroho, basi, wakati huo ni sasa. Wale wanaokeshwa na kuomba na kuyachunguza Maandiko kila siku wakiwa na shauku ya dhati kujua na kufanya mapenzi ya Mungu hawatapotoshwa kwa madanganyo yote yote yale ya Shetani. Hao ndio pekee yao watakaokitambua kisingizio wanachotumia watu wale wenye hila ili kuwadanganya watu na kuwanasa. Muda mwingi sana na mawazo hutolewa kwa mambo ya ulimwengu huu, juu ya mavazi na kula na kunywa, hata haubaki muda wote kwa ajili ya maombi na kujifunza Maandiko.

Tunataka kujua kweli kwa kila pointi [jambo], tena yatupasa kuitafuta kama vile inavyotafutwa hazina ile iliyositirika. Sahani za chakula cha hadithi za uongo hugawiwa kwetu toka kila upande, na watu wanachagua kuamini makosa [mafundisho potofu] badala ya ile kweli, kwa sababu kuikubali ile kweli kunaambatana na msalaba. Nafsi haina budi kukanwa; nafsi ni lazima isulibishwe. Kwa hiyo, Shetani analeta kwao njia rahisi kwa kuitangua Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Mungu anapomwacha mwanadamu kufuata njia yake mwenyewe, kwake [mtu huyo] ndiyo saa ya giza kuu katika maisha yake. Kwa mtoto yule aliye mkaidi, yaani, asiyetaka kutii, kuachwa afuate njia yake mwenyewe, yaani, afuate mwelekeo wa mawazo yake mwenyewe na kujikusanyia karibu naye mawingu mazito ya hukumu ya Mungu, ni jambo la kutisha mno.

Walakini Shetani anao mawakala wake ambao wana kiburi mno hata hawataki kutubu, ambao kila wakati wanafanya kazi ya kuibomoa kazi ya Yehova na kuikanyaga chini ya miguu yao. Ni siku ya huzuni na kukata tamaa ilioje kwa watu hao watakapokutana na kazi yao pamoja na mzungu wake wa matokeo! Watu wale ambao wangeweza kuokolewa na Yesu Kristo wamepotea kutokana na mafundisho yao na mvuto wao.

Kristo aliwafia hao ili wapate uzima. Alifungua njia mbele yao ambayo kwayo wangeweza kuishika Sheria ya Mungu [Amri Kumi] kwa njia ya wema wake. Kristo asema hivi, "Nayajua matendo yako. Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga" (Ufunuo 3:8). Kwa juhudi kubwa jinsi gani watu wanafanya kazi ya kuufunga mlango huo; lakini hawawezi. Ushuhuda wa Yohana ni huu, "Kisha Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na Sanduku la Agano lake [Amri Kumi] likaonekana ndani ya hekalu lake" (Ufunuo 11:19). Chini ya kiti cha rehema, ndani ya sanduku hilo, mlikuwa na mbao mbili za mawe, zikiwa zimeandikwa Sheria ya Yehova [Amri Kumi]. Watu wa Mungu waaminifu waliiona nuru iliyowaangazia kutoka katika Sheria ile, ambayo ilipaswa kutolewa kwa ulimwengu mzima. Na

kwa hivi sasa shughuli kubwa ya Shetani ni kuufunga mlango huo wa nuru; lakini Yesu asema kwamba hakuna awezaye kuufunga. Watu wataipa kisogo nuru hiyo, wataikana hadharani, na kuidharau, lakini yenyewe bado ingali iking'aa kwa mionzi miangavu, inayoonekana wazi ili kuwatia moyo na kuwaletea mibaraka wale wote watakaoiona.

Watoto wa Mungu watakabiliwa na pambano kali sana kutoka kwa yule adui wa wanadamu, nalo litazidi kuwa kali mno kadiri tunavyokaribia mwisho wa pambano hilo. Lakini Bwana atawasaidia wale watakaosimama kidete kuitetea kweli yake.

SURA YA 5

Imani na Matendo

Hotuba ya asubuhi iliyotolewa pale Basel, Uswisi
(Switzerland), Septemba 17, 1885. Ilichapishwa
katika gazeti la Signs of the Times la Juni 16, 1890.

"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao" (Waebrania 11:6). Wako wengi katika ulimwengu wa Kikristo wanaodai kwamba yale yote yanayotakiwa ili kuokolewa ni kuwa na imani; kwamba matendo si kitu, ila imani peke yake ndiyo ya lazima. Lakini Neno la Mungu linatambia sisi kwamba imani pasipo matendo imekufa. Wengi wanakataa kuzitii amri [kumi] za Mungu, ila wanaikuza sana imani. Lakini basi, imani lazima iwe na msingi wake.

Ahadi zote za Mungu zimetolewa kwa masharti. Iwapo tunafanya mapenzi yake, iwapo tunakwenda katika nuru yake, basi, hapo ndipo tunaweza kuomba lo lote tutakalo, nalo tutatendewa. Wakati sisi tunajitahidi kwa bidii kuwa watiifu, Mungu atazisikia dua zetu; lakini hataweza kutubariki sisi katika uasi wetu. Ikiwa tutachagua kutozitia amri zake [kumi], basi, tunaweza kupiga kelele, tukisema, "Imani, imani, uwe na imani peke yake," na jibu hili litatujia kutoka katika Neno imara la Mungu, likisema, "Imani pasipo matendo imekufa" (Yakobo 2:20,26). Imani kama hiyo itakuwa tu kama shaba iliayo na upatu uvumao. Ili kuweza kupata mafao ya neema ya Mungu ni lazima tufanye sehemu yetu; tunapaswa kufanya kazi kwa uaminifu na kuzaa matunda yapasayo toba.

Sisi ni watenda kazi pamoja na Mungu. Usikae kivivu, ukiwa unangojea tukio moja kubwa, ili kumfanyia Bwana kazi kubwa. Usiache kufanya kazi inayokukabili moja kwa moja njiani mwako, lakini unatakiwa kuzitumia vizuri zaidi nafasi ndogo ndogo zinazojitokeza kukuzunguka....

Kupigana Mieleka, Kufanya Kazi, na Kujitahidi

Yatupasa kufanya yote yale yanayowezekana kwa upande wetu kupiga vita vile vizuri vya imani. Yatupasa kupigana mieleka, kufanya kazi, kujitahidi, kusumbuka kuingia katika mlango ule ulio mwembamba. Yatupasa kumweka Bwana mbele yetu daima. Tukiwa na mikono safi, tukiwa na mioyo safi, yatupasa kujaribu kumheshimu Mungu katika njia zetu zote. Msaada umetolewa kwetu ndani yake yeye aliye na uweza wa kuokoa. Roho yule wa kweli na nuru atatuhisha na kutufanya upya kwa utendaji wake wa siri [usioweza kuelezeka]; kwa kuwa maendeleo yetu yote ya kiroho yanatoka kwa Mungu, si ndani yetu wenyewe. Mtenda kazi wa kweli atakuwa na nguvu ya Mungu ya kumsaidia, lakini yule aliye mzembe hataweza kusaidiwa na Roho wa Mungu.

Kwa njia moja tu sisi tunaachwa kutegemea nguvu zetu wenyewe; yatupasa kujitahidi kwa nguvu zetu zote kuwa na bidii na kutubu, kuitakasa mikono yetu na kuisafisha mioyo yetu kutokana na uchafu wa kila namna; yatupasa kukifikia kiwango kile cha juu kabisa, tukiamini kwamba Mungu atatusaidia katika juhudi zetu hizo. Yatupasa kutafuta kama tunataka kuona, na kutafuta kwa imani; yatupasa kubisha [kugonga mlango], ili mlango huo upate kufunguliwa kwetu. Biblia inatufundisha kwamba kila kitu kinachohusu wokovu wetu hutegemea njia yetu ya utendaji. Iwapo sisi tutapotea [tutaangamia], basi, uwajibikaji huo utakuwa ni wetu kabisa. Iwapo msaada umetolewa kwetu, na iwapo sisi tunayakubali masharti ya Mungu, basi, tunaweza kuupata uzima

ule wa milele. Yatupasa kuja kwake Kristo kwa imani, yatupasa kujitahidi kufanya imara kuitwa kwetu na uteule wetu.

Msamaha wa dhambi umeahidiwa kwake yeye atubuye na kuamini; taji ile ya uzima itazawadiwa kwake yeye atakayekuwa mwaminifu mpaka mwisho. Tunaweza kukua katika neema hiyo kwa kuendelea kukua katika neema ambayo tayari tunayo. Yatupasa kujitunza wenyewe tusitiwe mawaa na ulimwengu huu kama tutataka kuonekana kuwa hatuna lawama katika siku ile ya Mungu. Imani na matendo huenda bega kwa bega; hufanya kazi yao kwa ulinganifu katika kazi ile ya kutupatia ushindi. Matendo pasipo imani yamekufa, na imani pasipo matendo imekufa. Matendo kamwe hayataweza kutuokoa; ni wema wake Kristo utakaofaa kwa ajili yetu. Kwa njia ya imani katika yeye, Kristo atazifanya juhudi zetu zote zisizokuwa na ukamilifu wote kukubalika kwa Mungu. Imani tunayotakiwa kuwa nayo si imani ile ya kutofanya kitu cho chote; imani iokoayo ni ile itendayo kazi kwa upendo na kuitakasa nafsi. Yule atakayeinua juu kwa Mungu mikono yake iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano [mashaka] atakwenda kwa akili katika mapito [njia] ya amri [kumi] za Mungu.

Iwapo sisi tunataka kupewa msamaha wa dhambi zetu, basi, yatupasa kwanza kutambua dhambi ni nini, ili tupate kutubu na kuzaa matunda yapasayo toba. Ni lazima tuwe na msingi imara kwa imani yetu; lazima ijengwe juu ya msingi wa Neno la Mungu, na matokeo yake yataonekana katika utii kwa mapenzi ya Mungu yale yaliyodhihirishwa [yaliyofunuliwa]. Asema hivi yule mtume, "... [na huo utakatifu] ambao hapana mtu atakayemwona Mungu asipokuwa nao" (Waebrania 12:14).

Imani na matendo vitatufanya sisi tuwe na uwiano sawa na kutufanya tuwe na mafanikio katika kazi ile ya kuikamilisha tabia yetu ya Kikristo. Yesu asema hivi, "Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni" (Mathayo 7:21). Akiwa anazungumza juu ya chakula cha kimwili, mtume huyo alisema, "Kwa kuwa hata wakati ule tulipokuwapo kwenu tuliwaagiza neno hili, kwamba ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi, asile chakula" (2 Wathesalonike 3:10). Sheria [kanuni] iyo hiyo hutumika kuhusiana na lishe yetu ya kiroho; iwapo mtu ye yote atataka kula mkate ule wa uzima, basi, na ajitahidi [afanye juhudi] kuupata.

Tunaishi katika kipindi cha maana na cha kutamanisha [kuisimua] sana cha historia ya ulimwengu huu. Tunahitaji imani nyingi kuliko tulivyopata kuwa nayo [huko nyuma]; tunahitaji kushikwa kwa nguvu zaidi kutoka juu. Shetani anafanya kazi yake kwa nguvu zake zote ili apate kutushinda, kwa maana yeye anajua ya kuwa ana wakati mchache tu wa kufanya kazi yake. Paulo alikuwa anaogopa na kutetemeka katika kutimiza wokovu wake; na sisi, je! tusingeogopa kwamba ahadi ile tuliyoachiwa tusije tukaonekana kuwa tumeshindwa kuitimiza, na sisi wenyewe kuonekana kuwa hatustahili kupewa uzima ule wa milele? Yatupasa kukesha na kuomba, kujitahidi kwa juhudi ile inayotuletea maumivu makali ili tupate kuingia katika mlango ule ulio mwembamba.

Yesu Anaufidia Upungufu Wetu

Hakuna udhuru wote kwa kutenda dhambi au kwa kuwa wazembe. Yesu ametangulia katika njia ile, naye anataka sisi kufuata katika nyayo zake. Yeye ameteswa, amejitoa mhanga kuliko mtu ye yote miongoni mwetu anavyoweza kufanya ili apate kutuletea wokovu ule karibu sana nasi. Hatuna haja ya kukata tamaa. Yesu alikuja katika dunia yetu kumletea mwanadamu uweza wa Mungu ili kwa neema yake, tupate kubadilishwa [tabia zetu] na kufanana naye.

Kama moyoni mwake imo nia ya kumtii Mungu, na juhudi zinafanywa naye kuelekea kwenye mwisho huo, basi, Yesu ataikubali nia yake na juhudi hiyo kuwa ndiyo huduma bora kabisa iliyotolewa na mwanadamu huyo, naye ataufidia upungufu wake [mwanadamu huyo] kwa wema wake mwenyewe wa uungu. Walakini hatawakubali wale wanaojidai kuwa wanamwamini, ila hawataki kuzitii amri [kumi] za Baba yake. Tunasikia maneno mengi kuhusu imani, lakini tunahitaji kusikia maneno mengi zaidi juu ya matendo. Wengi wanajidanganya nafsi zao wenyewe kwa kuendelea kuishi kwa kufuata dini rahisi, inayoruhusu mambo yote, yaani, isiyokuwa na msalaba.

Lakini Yesu asema hivi, "Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuata" (Mathayo 16:24).

SURA YA 6

Onyo Dhidi ya Utakaso wa Uongo

Toka katika taarifa ya "Mkutano Mkuu katika nchi ya Sweden" uliofanyika katikati ya mwezi wa Juni, 1886. Ilichapishwa katika gazeti la Review and Herald la Oktoba 5, 1886.

Wakati mikutano inaendelea kule Orebro nilishurutishwa na Roho wa Bwana kuielezea Sheria yake [Amri Kumi] kuwa ndicho kipimo kikuu [kanuni kuu] cha haki na kuwaonya watu wetu dhidi ya utakaso wa kisasa, wa uongo [bandia] ambao chimbuko lake linatokana na kuabudu mapenzi [nia] yao badala ya kunyenyekea chini ya mapenzi [nia] ya Mungu. Fundisho hilo potofu linaenea kwa kasi sana ulimwenguni kote, na sisi kama mashahidi wake Mungu tutalazimika kutoa ushuhuda dhahiri dhidi yake. Hilo ni mojawapo ya madanganyo halisi kabisa ya siku za mwisho na litaonekana kuleta majaribu kwa wote wale wanaouamini ukweli wa leo. Wale ambao imani yao haijajizatiti juu ya Neno la Mungu watakoseshwa [watadanganyika]. Na sehemu ya kusikitisha mno kuliko zote ni kwamba wachache mno miongoni mwa wale watakaokoseshwa kutokana na fundisho hilo potofu ambao wataiona tena njia ya kurudi kwenye nuru hiyo.

Biblia ndiyo kanuni ya kupimia madai ya wote wanaodai kwamba wamepokea utakaso. Yesu aliomba kwamba wanafunzi wake wapate kutakaswa kwa ile kweli, naye anasema, "Neno lako ndiyo kweli" (Yohana 17:17); ambapo Mtunga Zaburi anatangaza, akisema, "Sheria yako [Amri Kumi] ni kweli" (Zaburi 119:142). Wale wote wanaoongozwa na Mungu watayaheshimu sana Maandiko ambamo sauti yake inasikika. Kwao Biblia itakuwa ina"faa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema" (2 Timotheo 3:16,17). "Mtawatambua kwa matunda yao" (Mathayo 7:16).

Hatuna haja ya ushahidi mwingine ili kuupima utakaso wa wanadamu; kama wao wanaogopa wasije wakakosa kuyatii mapenzi yote ya Mungu [Amri Kumi], kama wanaisikiliza sauti yake kwa bidii, wakiitegemea hekima yake, na kulifanya Neno lake kuwa ndiye mtu wao wa kuwashauri, hapo ndipo, japo wao hawajisifu kwamba ni wema kuliko wote, sisi tunaweza kuwa na hakika kwamba wanatafuta kuufikia ukamilifu ule wa tabia ya Kikristo. Lakini kama hao wanaodai kuwa wanao utakatifu, hata kama wakidokeza kidogo tu kwamba hawatakiwi tena kuyachunguza Maandiko, basi, sisi hatuna haja ya kusita kutangaza kwamba utakaso wao huo ni wa bandia [uongo]. Wanategemea akili zao [ufahamu wao] wenyewe badala ya kuyatii mapenzi ya Mungu.

Kile Anachotaka Mungu

Wakati huu Mungu anataka kile kile alichotaka kwa watakatifu wale wawili kule Edeni ----- utii kamili kwa matakwa yake. Sheria yake [Amri Kumi] inaendelea kuwa ni ile ile kwa vizazi vyote. Kanuni [kipimo] kuu ya haki iliyotolewa katika Agano la Kale haijapunguzwa katika Agano Jipya. Si kazi ya Injili kupunguza nguvu ya madai ya Sheria takatifu ya Mungu [Amri Kumi] ila kuwainua wanadamu juu ili wawe mahali wanapoweza kuzishika amri zake [kumi].

Imani katika Kristo inayomwokoia mwanadamu si kama vile inavyohubiriwa na wengi. "Amini, amini," ndicho kilio chao; "mwamini tu Kristo, nawe utaokoka. Hayo ndiyo yote unayopaswa kufanya." Wakati imani ya kweli inategemea Kristo kabisa kwa wokovu, itamwongoza [yule aliye nayo] kwenye utii kamili kwa Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Imani inadhihirishwa kwa matendo. Tena, yule mtume Yohana anatangaza, akisema, "Yeye asemaye, Nimemjua [Nimeokoka], wala hazishiki amri zake [kumi], ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake" (1 Yohana 2:4).

Si salama kutegemea hisia [kujisikia moyoni] au misisimko; mambo hayo ni viongozi wasioweza kutegemewa. Sheria ya Mungu [Amri Kumi] ndiyo kanuni ya utakatifu peke yake. Ni kwa njia ya Sheria hiyo [Amri Kumi] tabia ya mtu itapimwa. Kama mtu ye yote anayeulizia wokovu angeuliza swali hili, "Nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" waalimu wa siku hizi wanaofundisha utakaso wangejibu hivi, "Amini tu kwamba Yesu anakuokoa." Lakini Yesu alipoulizwa swali hilo alimwambia, "Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje? Yule aliyeuliza swali hilo akamjibu, akisema, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote,... na jirani yako kama nafsi yako," Yesu akamwambia, "Umejibu vema; fanya hivi nawe utaishi" (Luka 10:25-29).

Utakaso wa kweli utashuhudiwa kwa heshima ile anayoionyesha mtu kwa bidii na kwa uaminifu wake kwa amri zote [kumi] za Mungu, kwa uangalifu wake katika kuikuza kila talanta aliyopewa, kwa maongezi yake yenye busara, na kwa kuonyesha katika kila tendo analotenda upole ule wa Kristo.

Utakaso Uwaongozao Watu Mbali na Biblia

Idadi fulani ya watu walihudhuria katika mkutano huu ambao walishikilia nadharia [fundisho] ile inayopendwa sana na watu kuhusu utakaso, na wakati madai ya Sheria ya Mungu yalipotolewa kwao na picha halisi ya fundisho hilo potofu kuonyeshwa, mtu mmoja alichukizwa mno hata akasimama kwa ghafula na kuondoka kwenye ukumbi huo wa mikutano. Baadaye nilisikia kwamba alikuwa ametoka Stockholm na kuja kwenye mkutano huu. Katika maongezi yake pamoja na mmoja wa wachungaji wetu alidai kwamba yeye alikuwa hana dhambi kabisa, tena akasema kwamba yeye hakuwa na haja yo yote na Biblia, kwa maana Bwana alikuwa akimwambia yeye moja kwa moja lile analopaswa kufanya; yeye alikuwa mbali sana na mafundisho ya Biblia. Je! tunaweza kutazamia nini kwa wale wanaofuata mawazo yao wenyewe kuliko kufuata Neno la Mungu kama sio kudanganyika? Wanakitupilia mbali kitu kile ambacho ndicho peke yake kinaweza kugundua makosa [mafundisho hayo potofu], je! ni kitu gani basi, kiwezacho kumzuia yule mlaghai [mdanganyifu] mkuu asipate kuwateka hao kama apendavyo yeye?

Mtu huyo analiwakilisha kundi fulani. Utakaso huo bandia [wa uongo] unawaongoza watu moja kwa moja kwenda mbali na Biblia. Dini inageuka na kuwa hadithi ya uongo. Hisia na misisimko hufanywa kuwa ndicho kipimo chao. Wakati wao hudai kwamba hawana dhambi kabisa na kujisifu kwa ajili ya haki waliyo nayo, watu hao wanaodai kuwa wanao utakaso hufundisha kwamba watu wana uhuru kuivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi], na kwamba wale wanaozitii amri zake [kumi] wameanguka kutoka katika neema. Ufafanuzi wa madai yao hayo huamsha upinzani wao na kuchochea hasira yao na dharau. Hivyo ndivyo tabia yao inavyoonekana, kwa kuwa "ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii Sheria ya Mungu [Amri Kumi], wala haiwezi kuitii (Warumi 8:7).

Mfuasi wa kweli wa Kristo hatatoa madai ya kujisifu kuwa yeye ni mtakatifu. Ni kwa njia ya Sheria ya Mungu [Amri Kumi] mwenye dhambi huhakikishiwa dhambi zake [hujiona kuwa ana hatia]. Anaiona dhambi yake mwenyewe kwa kujilinganisha na haki kamilifu inayoamriwa nayo [hiyo Sheria], na jambo hilo linamfanya awe mnyenyekevu na atubu. Anapataniwa na Mungu kwa njia ya damu yake Kristo, na kadiri anavyoendelea kutembea pamoja naye, ndivyo kadiri atakavyozidi kupata utambuzi ulio wazi zaidi juu ya utakatifu wa tabia ya Mungu ulivyo na matakwa yake yaletayo athari nyingi [mabadiliko mengi katika maisha yake]. Ataona kwa wazi zaidi kasoro zake [upungufu wake] mwenyewe, tena, ataona haja ya kuendelea kuwa na toba na imani katika damu yake Kristo.

Yule ambaye anatambua daima kuwako kwake Kristo [katika maisha yake] hawezi kujitegemea mwenyewe, wala kuwa na haki yake mwenyewe. Hakuna hata mmoja miongoni mwa manabii au mitume aliyejigamba kwamba yeye alikuwa mtakatifu. Kadiri walivyokaribia zaidi katika kazi ile ya kuikamilisha tabia yao, ndivyo kadiri walivyojiona wenyewe kuwa hawakustahili kabisa, wala hawakuwa na haki yo yote ya kwao. Lakini wale ambao ufahamu wao ni mfinyu mno kuhusu ukamilifu alio nao Yesu, yaani, wale ambao kwa kiwango kidogo mno macho yao yanamwalia yeye, hao ndio wanaotoa madai yenye nguvu kwamba wao ni wakamilifu kabisa.

SURA YA 7

Jinsi ya Kujua Kama ni Mungu Anayetuongoza

Hii ni sehemu ya hotuba yake ya asubuhi iliyotolewa kule

Copenhagen, Denmark, Julai 21, 1886, yenye kichwa

kisemacho "Mwayachunguza [Chunguzeni] Maandiko."

Ilichapishwa katika gazeti la Review and Herald,

Aprili 3, 1888.

Utakutana na watu, kama vile mimi nami nilivyopata kukutana nao, wanaodai kwamba wao wametakaswa, yaani, ni watakatifu. Basi, kuna mvuto unaoduwaza kutokana na fundisho hilo. Watakusimulia mambo ya ajabu yanayotokea mioyoni mwao ili kukuonyesha wewe ya kwamba

Bwana ndiye anayewaongoza na kuwafundisha. Lakini, je! wewe waweza kujua kama siye Bwana anayewaongoza? Vema, kipo kipimo: "Na waende kwa Sheria [Amri Kumi] na kwa ushuhuda [Biblia]; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi [wamo gizani]" (Isaya 8:20).

Kama uadui ulio ndani ya moyo wa kibinadamu unaamshwa anapotajwa Bwana, yaani, yule Yehova Mkuu, basi, wewe unaweza kujua ya kwamba mtu huyo hana uhusiano wote na Mungu. Watu wanaweza kujidai kwamba wanayo imani kuu kwa Yesu na kukuambia wewe kwamba [kwa upande wako] huna lo lote unalopaswa kufanya isipokuwa lile [tu] atakalokufanyia Kristo. Basi, wakati ule Yesu atakapowaita wafu, itategemea kabisa juu ya mwenendo wako iwapo wewe utapata ufufuo ule wa uzima wa milele au ufufuo ule wa laana [adhabu ya kutengwa na Mungu milele]. Kwa njia hiyo wanazichanganya kweli hizi na makosa [mafundisho potofu], wala hawawezi kusema kweli ni nini; nao wakiombwa kukaa chini na kuyachunguza Maandiko pamoja nawe ili waone Bwana anasemaje, [kwa upande wangu] mimi sijapata kumjua mtu awaye yote ambaye hatoi jibu kwamba hana haja ya kuyachunguza Maandiko hayo, maana Bwana amemwambia la kufanya.

Sauti ya Mungu inazungumza nasi kwa njia ya Neno lake, na sauti nyingi ziko tutakazosisikia; walakini Kristo ametuambia kwamba tujihadhari na wale watakaosema, "Tazama, Kristo yupo hapa, au yuko kule" [Mathayo 24:23-27]. Basi, tutajuaje kwamba hao hawanayo ile kweli kama sio kwa kupima kila kitu [kila fundisho] kwa Maandiko? Kristo ametuonya sisi kujihadhari na manabii wa uongo ambao watakuja kwetu katika jina lake, wakisema kwamba wao ndio yule Kristo [mwenyewe]. Kama ninyi mtachukua msimamo usemao kwamba si muhimu kwenu kuyaelewa Maandiko, basi, mtakuwa katika hatari ya kuchukuliwa mbali kwa mafundisho hayo. Kristo amesema kwamba patakuwa na kundi la watu ambao, katika siku ile ya hukumu ya kupatiliza, watasema, "Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri [waziwazi], Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu" (Mathayo 7:22,23).

Basi, sisi kwa sasa tunataka kujua dhambi maana yake nini ----- ni uvunjaji wa Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Hiyo ndiyo tafsiri [sahihi] ya dhambi peke yake iliyotolewa katika Maandiko [Soma 1 Yohana 3:4, AJKK]. Kwa hiyo, twaona kwamba wale wanaodai kuwa wanaongozwa na Mungu, na halafu wanakwenda mbali naye na mbali na Sheria yake [Amri Kumi], hao ndio wasioyachungaza Maandiko. Lakini Bwana atawaongoza watu wake; kwa maana anasema kwamba kondoo wake watamfuata watakapoisikia sauti yake [Biblia - Yoh. 10:14-16], lakini mgeni [yule asiyezungumza sawasawa na Biblia - Yoh. 10:5] hawatamfuata kabisa. Basi, yatupasa sisi kuyaelewa kabisa Maandiko [Biblia]. Hapo ndipo hatutalazimika kuuliza iwapo wale wengine wanayo ile kweli, kwa maana itaonekana katika tabia zao.

Shetani Atafanya Miujiza Yake

Wakati unakuja Shetani atakapofanya miujiza yake mbele ya macho yetu, akijidai ya kwamba yeye ndiye Kristo; na kama miguu yenu haijajikita juu ya ile kweli ya Mungu, basi, mtachukuliwa mbali kutoka kwenye msingi wenu mliokuwa nao. Usalama pekee kwenu ninyi ni kuitafuta ile kweli kama zinavyotafutwa hazina zile zilizositirika. Ichimbeni kweli kama vile ambavyo mngeweza kuzichimba hazina zilizo chini ya ardhi, kisha liwekeni Neno la Mungu, yaani, Biblia, mbele za Baba yenu aliye mbinguni, na kusema, "Unielimisha; Unifundishe kweli ni nini."

Roho wake Mtakatifu atakapoingia mioyoni mwenu, na kuitia muhuri kweli hiyo mioyoni mwenu, hapo ndipo ninyi hamtaweza kuiachilia iende zake kirahisi-rahisi tu [Mithali 23:23]. Mmejipatia uzoefu kama huo kwa kuyachunguza Maandiko kiasi kwamba kila neno limethibitishwa. Tena ni jambo la maana kwamba mwendelee daima kuyachunguza Maandiko. Yawapasa kuujaza moyo wenu na Neno la Mungu; kwa kuwa mnaweza kutengwa na kuwekwa mahali ambapo hamtakuwa na nafasi ya kukutana na watoto wa Mungu. Wakati huo ndipo mtakapozitaka hazina za Neno la Mungu zilizofichwa mioyoni mwenu, na upinzani utakapokuja na kuwazunguka, hapo ndipo mtakapohitaji kupima kila kitu kwa Maandiko hayo.

SURA YA 8

Watu wa Mungu Wazishikao Amri Zake [Kumi]

Hii ni sehemu ya hotuba yake iliyotolewa katika mji wa South Lancaster, Massachusetts, Januari 19, 1889, chini ya kichwa kisemacho "Ndani Yake Imo Nuru." Ilichapishwa katika gazeti la Review and Herald, Februari 26, 1889.

Mbingu yote kwa hamu kubwa sana imekuwa ikiwaangalia wale wanaodai kuwa ni watu wa Mungu wazishikao amri zake [kumi]. Hapa wapo watu ambao wangestahili kuzidai ahadi zote za Mungu ambazo ni nyingi; watu ambao wangestahili kusonga mbele toka utukufu hata utukufu, na toka nguvu hata nguvu nyingi zaidi; ambao wangepaswa kuwa mahali pale wanapoweza kuakisi [kurudisha] utukufu wa Mungu kwa matendo yao wanayotenda. Yesu amesema, "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni" (Mathayo 5:16).

Sisi tumepokea mibaraka ya Mungu mingi sana, lakini haitupasi kusimama hapo. Yatupasa kuikamata mionzi mitakatifu ya nuru mingi zaidi na zaidi kutoka mbinguni. Yatupasa kusimama mahali pale tunapoweza kuipokea nuru na kuiakisi [kuiangaza], katika utukufu wake, katika njia ya wengine. Hapajapata kuwapo na wakati ambapo sisi tungejisikia kuwa tunao ujasiri mwingi na matumaini mengi katika kazi [ya Mungu] kama wakati huu wa sasa. Kuna watu wengi katika ulimwengu wetu huu ambao hawazishiki wala hawajidai kuzishika amri za Mungu [kumi], na, hata hivyo, wao ndio hasa wanaoidai mibaraka yote ya Mungu. Wako tayari kuzikubali ahadi zake na kuzitumia bila kujali kutekeleza masharti ambayo juu yake zimejengwa. Hawana haki yo yote ya kupewa mibaraka yote wanayoidai.

Lakini kwa nini wale wanaozishika amri zake [kumi] wasiweze kuzishikilia ahadi hizo zilizotolewa kwa watoto hao wa Mungu? Tunaweza kuiona haki ya Kristo katika Sheria hiyo [Amri Kumi]. Katika msalaba ule wa Kalvari, "Fadhili [Neema] na Kweli [Sheria - Zab.119:142] zimekutana, Haki [Sheria - Rum.7:12] na amani [Neema au Msamaha - Lk. 2:14] zimebusiana" (Zaburi 85:10). Huo ndio mchanganyiko mzuri unaotakiwa kuonekana katika kazi yetu.

Kweli na haki ni lazima ihubiriwe pamoja na upendo wa Mungu kama ulivyofunuliwa kwetu ndani ya Yesu. Ni usafi wa maisha ulioje utakaoweza kuonekana! Ni usafishaji wa kila uchafu wa kimaadili ulioje utakaonyeshwa kuwa unahitajika [katika maisha yetu]! Kisha, hayo yatakapokuwa yamefanyika, kiburi kile cha nia yetu ambacho kimewazuia wengi sana wasiweze kuja kwenye nuru, kitayeyuka chote na kutoka nje ya mioyo yao, hapo watakapomtazama Mkombozi wao na kuona jinsi alivyo wa thamani kwao, yaani, watakapoiona rehema na huruma yake.

Kila mmoja wetu hana budi kuanguka juu ya Mwamba [Jiwe] huo na kuvunjika-vunjika [Mathayo 21:44]. Je! yuko mmoja atakayeking'ang'ania kiburi chake? Je! yuko mmoja ambaye atashindwa kuiona thamani yake Kristo? Je! upo moyo hapa usiotaka kulainishwa kwa upendo wake Yesu? Je! yupo mtu ye yote atakayebaki na chembe moja ya kujisifu mwenyewe?

Tunahitaji kumkaribia Mungu zaidi... Imekuwaje basi, kwamba mioyo yetu haijaguswa kabisa na upendo wa Mungu? Kwa nini tumekuwa na hukumu kali sana dhidi ya Baba yetu aliye mbinguni? Kutokana na nuru aliyonipa Mungu, najua kwamba Shetani amemweleza Mungu vibaya kwetu sisi kwa kila njia inayowezekana kwake. Amekitupa kivuli chake cha kishetani katika njia yetu, ili tusipate kumtambua Mungu wetu kama Mungu mwenye rehema, huruma, na wa kweli. Hii ndiyo maana mioyo yetu imeingiwa na [imekuwa migumu kama] chuma.

Kisha sisi tumezungumza sana juu ya giza lile alilotutupia juu yetu yule mwovu, nasi tumeomboleza sana kwa ajili ya hali yetu hiyo; na kwa kufanya hivyo, tumezidi tu kukitandaza

kivuli hicho juu ya watu wengine, na kile kilichotujeruhi sisi kimewadhuru nao. Tulipotamka maneno yetu yale yaliyojaa mashaka, wengine nao wamefunikwa na giza na mashaka hayo.

Hatuwezi kumudu kuendelea kuifanya kazi hiyo. Kwa njia hiyo sisi tunamweka Baba yetu aliye mbinguni katika nuru mbaya (yaani, isiyokuwa ya kweli). Hayo yote hayana budi kubadilika. Yatupasa kuikusanya mionzi ya kweli ile ya Mungu na kuiacha nuru yetu kuangaza juu ya njia ya wengine iliyotiwa giza. Nuru ile ya mbinguni inaangaza kwa wale watakaomfuata Kristo, Nuru ya Ulimwengu. Asema hivi, "Yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima " (Yohana 8:12).

Ni sifa gani mnayotoa kwa ulimwengu huu juu ya dini hiyo ya Kristo kama ninyi mtaendelea kunung'unika na kulalamika na kujazwa na huzuni nyingi? Wale wanaozishika amri za Mungu [kumi] wangepaswa kudhihirisha kwamba ile kweli [waliyo nayo] inazitakasa nafsi zao, inayaadilisha na kuyatakasa mawazo yao, na kukuza tabia na maisha yao. Kristo amekufa ili sura ya Mungu kimaadili ipate kurejeshwa mioyoni mwetu na ipate kuangaza kwa wale wanaotuzunguka.

Tunahitaji kunywa maji ya chemchemi ile ya uzima kwa kina kirefu zaidi na zaidi. Mimi natumaini kwamba hakuna hata mtu mmoja atakayeridhika bila kufanya kazi kamilifu kwa ajili ya maisha yake ya milele, na kuanzia wakati huu wa sasa na kuendelea, kwa njia ya maadili yetu na mfano wetu, ionekane kwamba ninyi ni wawakilishi wake Kristo. Mnaweza kutoa ushuhuda wenu ulio hai; mkisema: "Sikilizeni kile alichoitendea nafsi yangu, Bwana!" Bwana bado yu tayari kutoa mibaraka mikubwa zaidi kwetu.

Aliruhusu wema wake wote kupita mbele ya Musa; aliitangaza tabia yake kwake kwamba yeye ni Mungu mwenye rehema nyingi, si mwepesi wa hasira [mvumilivu], mwenye fadhili ----- mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi. Musa alitakiwa kuiwakilisha tabia hiyo kwa wana wa Israeli, nasi yatupasa kufanya vivyo hivyo.

Yatupasa kutoka na kuzitangaza fadhili zake Mungu na kueleza waziwazi jinsi tabia yake ilivyo hasa mbele ya watu. Yatupasa kuurudisha mwanga ule wa utukufu wake. Je! sisi tumefanya hivyo kwa wakati uliopita? Je! tumeidhihirisha tabia ya Bwana wetu kwa maadili na mfano wetu? Je! sisi hatujajiunga na kazi ile ya adui wa roho za watu na kumweleza vibaya Baba yetu wa mbinguni? Je! hatujatoa hukumu juu ya ndugu zetu, tukiwa tunayakosoa maneno na matendo yao? Basi, upendo wa Mungu haujatawazwa ndani ya mioyo yetu. Hebu na tufanye matengenezo yaliyo dhahiri.

SURA YA 9

Kiwango cha Imani Yetu

Hotuba iliyotolewa na Ellen G. White pale Ottawa,
Kansas, siku ya Sabato, Mei 11, 1889, miezi michache
tu baada ya Kikao cha Minneapolis, akilifafanua somo
hili kwa njia rahisi inayoweza kutekelezwa. Imo katika
jalada kama Manuscript 1, 1899.

Fungu Kuu: Yohana 3:1-16 (Lilisomwa na mnenaji).

Kama hakuna kitu kingine zaidi katika Maandiko yote kinachoionyesha wazi njia ya kwenda mbinguni, basi, tunacho hapo juu katika maneno hayo. Yanatuambia kile tunachopaswa kufanya ili tupate kuokoka. Nami nataka kuwaambia, Enyi rafiki zangu, ya kwamba jambo hilo linagonga moja kwa moja kwenye mzizi wa kazi ile ya juu juu inayofanyika katika ulimwengu huu wa kidini. Yanapambana moja kwa moja na wazo lile lisemalo kwamba unaweza kuwa mtoto wa Mungu pasipo kuwa na badiliko lo lote katika maisha yako. Kuna badiliko dhahiri linalofanyika ndani yetu iwapo kweli ile ya Mungu imepewa nafasi [ya kufanya kazi yake] ndani ya mioyo yetu, kwa maana ina uwezo ule utakasao juu ya maisha yetu na juu ya tabia yetu. Tunapoyaona matunda ya haki ndani ya wale wanaodai kuwa wanayo kweli hiyo ya hali ya juu, kama sisi tunavyodai kuwa tunayo, hapo ndipo patakuwa na njia ya utendaji wetu itakayoshuhudia kwamba sisi tumejifunza kwake Kristo.

Kristo, Tumaini la Israeli, alipoangikwa msalabani na kuinuliwa juu kama alivyomwambia Nikodemo ya kwamba angefanyiwa hivyo, tumaini la wanafunzi wake likafa pamoja na Yesu. Walishindwa kulieleza jambo hilo. Hawakuweza kuelewa yale yote aliyokuwa amewaambia Kristo mapema kuhusu jambo hilo.

Lakini baada ya Ufufuo wake matumaini na imani yao ikafufuka, kisha wakatoka na kumtangaza Kristo akiwa amesulibiwa. Wakasimulia jinsi Bwana wao wa uzima na utukufu alivyokamatwa kwa mikomo miovu na kusulibiwa, lakini kwamba alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu. Na hivyo kwa ujasiri mkubwa wakayanena maneno ya uzima ambayo watu wengi walishangaa sana kuyasikia.

Mafarisayo pamoja na wale waliowasikia wakimtangaza Kristo kwa ujasiri kuwa ndiye Masihi wakawaona hao kuwa walikuwa na Kristo na kujifunza kwake. Walisema kama vile Yesu alivyosema. Jambo hilo likawahakikishia mioyoni mwao kwamba hao walikuwa wamejifunza kwa Yesu. Imekuwaje basi, kwa wanafunzi wake katika vizazi vyote vya dunia hii? Kumbema! wamejifunza kwa Yesu; wamekuwa katika shule yake; wamekuwa wanafunzi wake, nao wamejifunza masomo yale yaliyotolewa na Kristo kuhusu uhusiano ule ulio hai unaomwunganisha mwanadamu na Mungu. Imani iliyo hai ni ya muhimu kwa wokovu wetu ili tupate kuushikilia wema unaotokana na damu yake Mwokozi wetu yule aliyesulibiwa na kufufuka, yaani, Yesu Kristo, Haki yetu.

Inaonekana kana kwamba ipo hali ya hewa yenye mawingu-wingu ambayo imejikusanya kuizunguka nafsi ya mtu na kuufunga mlango ndani ya moyo wake. Ni jambo lisilowezekana kabisa kupenya hali hiyo ya hewa iliyojaa mashaka na kutokuamini. Haiwezekani kabisa kuiamsha shauku yake kuu apate kujua kile anachopaswa kufanya ili apate kuokoka.

Urahisi wa Kuokolewa

Yule anayetaka kuishikilia Haki ya Kristo hana haja ya kungoja hata kwa dakika moja ili apate kuzifuta dhambi zake yeye mwenyewe. Hana haja ya kungoja mpaka afanye toba inayofaa kabla hajaipokea Haki yake Kristo. Hatulielewi vizuri suala hilo la wokovu. Lenyewe ni rahisi kama ABC. Lakini sisi hatulielewi.

Inakuwa-kuwaje basi, ya kwamba mtu huyo anaweza kutubu! Je, jambo hilo linatokana na nafsi yake mwenyewe? Hapana; kwa sababu moyo wake wa asili una uadui na Mungu. Basi, moyo huo wa asili waweza kujiamsha wenyewe hata ukaweza kutubu wakati hauna uwezo wa wote wa kufanya hivyo? Ni kitu gani kinachomfikisha mtu kwenye toba? Ni Yesu Kristo. Anamfikishaje mtu huyo kwenye toba? Kuna njia elfu ambazo anaweza kutumia ili kuileta hali hiyo [moyoni mwake].

Mungu yule wa mbinguni anafanya kazi yake ndani ya mioyo ya wanadamu wakati wote. Mwaliko umetolewa katika Neno la Mungu, wala si humo tu ulimotolewa, bali umetolewa na wale wote wanaomwamini Kristo na wanaomdhihirisha Kristo katika tabia zao. Huenda wasitoe mahubiri yo yote; huenda wasimjue mtu huyo moja kwa moja na kuzungumza naye kuhusu hali yake ya kutokuwa na toba, lakini mtu kama huyo anapokutana na mmojawapo wa wafuasi wa Yesu Kristo anaona kwamba kuna kitu fulani ndani ya huyo ambacho yeye hanacho. Mafarisayo waliona ya kuwa palikuwa na kitu fulani ndani ya wanafunzi wale ambacho wao hawakuweza kukieleza. Waliona kitu fulani cha ajabu na moyoni mwao wakathibitishiwa ya kwamba wanafunzi wale walikuwa wakimsikiliza Yesu na ya kwamba walikuwa wamejifunza mafundisho yao kutoka kwake.

Kuna mivuto inayoendelea wakati wote ndani ya moyo wa mwanadamu. Kuna hali fulani inayouzunguka moyo huo wa kibinadamu na hali hiyo huenda ikawa hali ya kimbingu ama hali ya kishetani. Kuna njia mbili zilizo dhahiri. Ama sisi tuko upande wake Kristo katika hoja hii ama tuko upande wake yule adui. Na kama sisi tunapata daima mionzi ya nuru ile ya Mungu itokayo kule kwenye utukufu, basi, malaika wa Mungu wanatuzunguka, tena kuna hali fulani inayouzunguka moyo wetu wa kibinadamu. Mwelekeo wetu halisi, maneno yetu yale yale hasa, hushuhudia kuongoka halisi kwa wale wote wanaokuja katika mazingira ya mvuto wetu. "Na Roho na Bibi-Arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! Naye mwenye kiu na aje."

Basi, kwa kuwa sisi ni matawi ya Mzabibu ule ulio Hai, tutapata lishe yetu kutokana na utomvu ule unaopita katika Mzabibu huo. Unapita wakati wote kwenda kwenye kila tawi, na kila tawi litazaa matunda yake kwa utukufu wake Mungu. "Ni mapenzi ya Baba yenu" "kwamba mzae [matunda] sana." Sasa basi, msimamo wetu ni upi? Ni lazima uwe msimamo ule wa imani ile iliyo hai.

Huwezi Kufikiri na Kutafuta Sababu

"Mimi nataka," asema mtu mmoja, "kufikiri na kutafuta sababu ya jambo hili." Vema, fikiri na kutafuta sababu kama utaweza. "Upepo unavuma upendako," nawe unaisikia sauti yake, lakini

huwezi kuueleza [upepo huo]. Na zaidi sana wewe huwezi kueleza mambo ya Mungu yanayotokea katika moyo wa mwanadamu. Huwezi kuifafanua imani ile inayoushikilia vizuri wema ule utokanao na damu ya Mwokozi yule aliyesulibiwa na kufufuka, ambayo inakuletea haki ya Kristo katika maisha yako. Wewe ukiwa umevikwa haki yake Kristo, na sio haki yako, basi, hutaweza kutegemea kile unachoweza kufanya wala kile utakachofanya. Je, wewe hujui kwamba huwezi kufanya neno lo lote pasipo Kristo? "Maana pasipo mimi," yeye asema, "ninyi hamwezi kufanya neno lo lote" (Yohana 15:5).

Unapoketi mezani [kumbuka kwamba] chakula kile unachokula ni ufunuo wa upendo wake Kristo. Na kule kuisikiliza kweli ya maneno ya Mungu kutoka mimbarani ni ujumbe uliotumwa kwetu kututangazia maneno yale ya uzima.

Ni akina nani miongoni mwenu waliokuwa wakiyakusanya mashaka yote pamoja na hoja zote kwa kadiri ile mliyoweza kukusanya na kulundika dhidi ya haki ile ya Kristo? Ni akina nani waliokuwa wakifanya hivyo? Je, ninyi mko upande gani?

Je, hivi ninyi mmekuwa mkizizingatia kweli hizi za thamani pointi kwa pointi kama vile zilivyotolewa? Au mmekuwa mkifikiri kwamba mnaweza kufuata mawazo yenu wenyewe na kulisoma na kulipima Neno la Mungu kwa maoni na nadharia zenu wenyewe? Au mtayachukua maoni yenu pamoja na nadharia zenu na kwenda nazo kwenye Neno la Mungu na kuyaruhusu Maandiko hayo yaliyo hai kuwafunulia ninyi mapungufu na makasoro yenu na kuwaonyesha ninyi mahali yalipo katika maoni na nadharia zenu hizo? Hatuwezi kuchukua msimamo ule usemao kwamba tutalikosoa Neno la Mungu [likienda kinyume na maoni yetu] kwa sababu sisi tuliamini hivi na vile. "Na waende kwa Sheria [Amri Kumi] na kwa ushuhuda [Biblia]; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi [wamo gizani]" (Isaya 8:20).

Kama palikuwa na watu walioihitaji nuru sana, basi, ni wale wanaoishi katika siku zile zile hasa za kufungia historia ya ulimwengu huu. Sisi tunataka kujua Maandiko yanasemaje. Tunataka kuja kwenye Maandiko hayo ya Mungu yaliyo hai. Tunaihitaji imani ile iliyo hai inayoushika kwa nguvu mkono ule wa uweza wake Mungu, tena tunataka kumtegemea Yesu Kristo, Haki yetu, kwa moyo wetu wote. Nasi twaweza kufanya hivyo. Naam, twafanya hivyo kwa faida yetu katika mambo yale moyo wetu unayoyapenda.

Ninyi mnaweza kuunganishwa na Mzabibu huo Hai. Kila kiungo cha mwili wenu wote kinaweza kuunganishwa na Mzabibu huo, na utomvu na lishe itokayo katika Mzabibu huo italilisha tawi lile lililo katika Mzabibu huo, mpaka ninyi mtakapokuwa katika umoja na Kristo kama yeye alivyokuwa umoja na Baba yake. Kwa njia hiyo mibaraka yake itatolewa kwenu. Lakini, ndugu, sisi hatujawa na imani hiyo. Tumemwaibisha sana Mungu kwa muda mrefu kwa kutokuamini kwetu.

Imani ya Mtu yule Aliyepooza

Nitamtaja mtu yule aliyepooza, ambaye alikuwa hajavitumia viungo vyake kwa miaka mingi sana. Alikuwa pale. Makuhani, wakuu, na waandishi walikuwa wameichunguza hali yake na kutangaza kwamba ilikuwa haina matumaini yo yote. Walimwambia kwamba alikuwa amejiletea mwenyewe hali ile kwa dhambi yake, na ya kwamba hapakuwa na matumaini yo yote kwake [ya kupona]. Lakini habari iletwa kwake kwamba palikuwa na mtu aliyeitwa Yesu, aliyekuwa anafanya miujiza mikubwa. Alikuwa anaponya wagonjwa, tena alikuwa amewafufua hata wafu. "Lakini mimi nawezaje kwenda kwake?" akasema.

"Tutakubeba kwenda kwa Yesu," rafiki zake wakajibu, "tutakupeleka mbele yake kabisa; tumesikia kwamba amekuja mahali fulani."

Basi wakamchukua yule mtu aliyekuwa hana matumaini yo yote kwenda naye mahali walipojua kwamba Yesu yupo. Lakini umati mkubwa wa watu ulikuwa umelizunguka jengo lile na kusongamana sana mahali pale alipokuwapo Yesu hata hapakuwa na nafasi yo yote kwao, si zaidi ya kufika mlangoni tu. Wangefanya nini, basi? Yule aliyepooza akatoa shauri kwamba watoboe dari kwa kutoa vigae na kumshusha chini kupitia darini.

Hivyo ndivyo alivyoionyesha imani yake itokayo moyoni. Wakafanya hivyo, naye akawekwa mbele ya Yesu kabisa, mahali alipoweza kumtazama. Na Yesu alipomwangaalia, akamhurumia, kisha akamwambia, "Mwanangu, umesamehewa dhambi zako" (Marko 2:5). Naam, ni furaha ilioje! Yesu alijua kile alichokihitaji hasa mtu yule aliyekuwa mgonjwa. Alijua kwamba ameteseka sana kwa sababu ya kusumbuliwa na dhamiri yake, basi, akamwambia, "Umesamehewa dhambi zako." Ni faraja ilioje iliyokuja mawazoni mwake! Ni matumaini yaliyoje yaliyoujaza moyo wake!

Ndipo hisia hizi zikainuka ndani ya mioyo ya wale Mafarisayo, "Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu?"

Ndipo Yesu akawaambia, "Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri [anayo mamlaka] duniani ya kusamehe dhambi, (akamwambia yule mwenye kupooza), Nakuambia, Ondoka, ujitwike kitanda chako ukaende zako nyumbani kwako" (Luka 5:24). Nini? ajitwike kitanda chake kwa mikono yake ile iliyopooza! Je, alifanya nini yeye? Kumbe! yeye akafanya kama vile alivyoagizwa. Akafanya kile Bwana alichomwambia kufanya. Uwezo wa nia yake uliviwezesha kujongea viungo vyake vile vilivyokuwa vimepooza pamoja na mikono yake, navyo vikaanza kufanya kazi, wakati vilikuwa havijafanya kazi kwa muda mrefu sana. Maonyesho hayo yalionyesha mbele ya watu kwamba palikuwa na mtu Mmoja katikati yao ambaye hakuweza tu kusamehe dhambi bali aliweza kuwaponya wagonjwa wao.

Lakini ushahidi ule mwingi uliotolewa kwa wale Mafarisayo haukuwaongoa. Watu wanaweza kujifungia wenyewe katika hali yao ya kutokuamini, mashaka, na ukafiri hata kufufuliwa kwa wafu hakuwezi kuwagusa mioyo yao ili wapate kusadiki. Kwa sababu ya kutokuamini kwao wangukuwa katika hali ile ile ya kutokuamini, wasiweze kusadiki, yaani, wasiweze kuongoka. Lakini wale wote waliokuwa na mioyo inayoipokea kweli na walio na masikio ya kusikia, wakamtukuza Mungu. Wakapaza sauti zao kwa mshangao, wakisema "Namna hii hatujapata kuiona kamwe."

Jibu kwa Mtu yule Aliyekuwa Hawezi

Pale alikuwa [amelala] mtu yule aliyekuwa hawezi, na Kristo alipozungumza naye, yeye akamsimulia kisa cha kusikitisha kuhusu jinsi kila mara alipotaka kuingia majini ili kuponywa, mtu mwingine alishuka mbele yake. Kristo akamwuliza swali hili, "Wataka kuwa mzima?" (Yohana 5:6). Ni swali gani hilo! alikuwa pale kwa kusudi hilo, lakini Kristo alitaka kuiamsha tamaa iliyokuwa ndani ya moyo wa mtu yule na kutaka mwenyewe aseme kuwa anataka kuwa mzima. Ndipo Kristo alipomwamuru kusimama, kujitwika godoro lake na kwenda zake, naye akafanya kama vile Kristo alivyomwambia kufanya. Hakusema, "Mbona mimi nimekuwa hapa kwa miaka thelathini wala sijatembea hatua hata moja kwa muda wote ule." Hakukataa na kuanza kutoa hoja zake, bali alifanya kama vile tu alivyoambiwa kufanya. Akajitwika godoro lake, akaenda zake na tangu wakati ule alikuwa amepona kabisa.

Hiyo ndiyo imani tunayoihitaji. Lakini ukisimama na kuanza kueleza kila kitu na kutoa sababu ya kila pointi, basi wewe utakufa katika dhambi zako, kwa sababu hutaweza kuridhika.

Nyoka ya Shaba

Hapa kuna mfano mwingine aliotoa Kristo mbele ya Nikodemo ----- nyoka yule aliyeinuliwa jangwani ----- na kumtangazia, akisema, "Vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa" (Yohana 3:14). Naye atakapoinuliwa, atawavuta watu wote kwake, "ili kila mtu aminiye asipotee [asiangamie], bali awe na uzima wa milele" (fungu la 16). Hebu sasa umwangelie tu yule nyoka wa shaba. Wana wa Israeli walikuwa hawajatambua kwamba Mungu ndiye aliyekuwa akiwalinda kwa njia ya malaika zake, waliotumwa kuwa msaada kwao na ulinzi wao. Watu wale walikuwa hawajaangamizwa na nyoka wale katika safari yao ile ndefu mle jangwani. Walikuwa ni watu wasio na shukrani.

Sisi ndivyo tulivyo. Hatuzitambui hatari elfu moja ambazo Baba yetu wa mbinguni ametuepusha nazo. Hatujautambua mbaraka wake mkubwa aliotupa sisi kwa kutupa chakula na mavazi, kwa kuyaokoa maisha yetu kwa kuwatuma malaika zake walinzi kutulinda. Tungekuwa na shukrani kila siku kwa mambo hayo. Tulipaswa kuwa na shukrani iliyochochewa ndani ya mioyo yetu na kuja kila siku kwa Mungu na sadaka yetu ya shukrani. Tungepaswa kukusanyika kwenye madhabahu yetu ya kifamilia [maombi ya nyumbani mwetu] kila siku na kumsifu kwa ulinzi na utunzaji wake juu yetu. Wana wa Israeli walikuwa vipofu hata wasiweze kuona kwamba ni Mungu aliyekuwa anawalinda kutokana na wadudu [nyoka] wale wenye sumu. Lakini alipouondoa mkono wake [wa ulinzi] waliweza kuwauma.

Ni nini basi? Kumbé! ni Kristo mwenyewe aliyemwambia Musa kusimamisha mti ule na kutengeneza nyoka ya shaba na kumtundika juu ya mti ule na kumwinua machoni pa wana wa

Israeli, ili kila mmoja aliyemtazama apate kuishi. Hawakuwa na kazi kubwa ya kufanya. Walitakiwa kutazama kwa sababu Mungu alisema wafanye hivyo.

Hebu, basi, na tuseme wao wangesimama na kuanza kufikiri na kutafuta sababu, na kusema, "Mbona haiwezekani kabisa kwamba kwa kumtazama tu nyoka yule wa shaba sisi tutaponywa! Hamna uhai ndani yake!" Lakini basi, mtazamo ule wa imani uliwaponya kama vile Mungu alivyokuwa amewaambia kuwa ungewaponya. Wale waliotazama wakaishi. wale waliosimama na kutoa hoja zao na ufafanuzi wao juu yake, wakafa.

Tunatakiwa tufanye nini basi? Tazama uishi. "Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo na Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa" (Yohana 3:14). Sababu? Ili wale wanaomtazama "wasipotee [wasiangamie], bali [w]awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

Ni imani ya aina gani hiyo? Je! ni kuamini tu, au ni imani ile ya kukiri tu? Wapo wengi hapa walio na imani kama hiyo. Wewe unaamini kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu; lakini, je! wewe binafsi unayo imani kuhusu wokovu wako? Je! unaamini kwamba Yesu ni Mwokozi wako? kwamba alikufa juu ya msalaba ule wa Kalvari kukukomboza wewe? kwamba amekupa wewe kipawa kile cha uzima wa milele ukimwamini?

Hiyo Ndiyo Haki kwa Imani

Na kuamini maana yake ni nini, basi? Ni kukubali kabisa kwamba Yesu alikufa kama kafara yetu; kwamba akawa laana kwa ajili yetu, akazichukua dhambi zetu na kuzibeba yeye mwenyewe, na kutuhesabia sisi haki yake mwenyewe. Kwa hiyo, sisi tunaaidai haki yake Kristo, tunaamini, nayo inakuwa haki yetu sisi. Yeye ndiye Mwokozi wetu. Anatuokoa sisi kwa sababu yeye alisema atafanya hivyo. Je! tutaanza kutafuta maelezo yote kuhusu namna atakavyoweza kutuokoa? Je! tunao wema ndani yetu wenyewe ambao utatufanya tuwe wema zaidi na kutusafisha madoa na mawaa yote ya dhambi zetu, na kutuwezesha wakati huo kuja mbele zake Mungu? Hatuwezi kabisa kufanya hivyo.

Je! wewe hujui kwamba yule mwanaume kijana aliyekuja kwa Kristo na kumwuliza afanye nini ili aupate uzima, Kristo alimwambia kuzishika zile amri [kumi]. Yeye [kijana] akasema, "Hizo zote nimezishika." Basi, Bwana akataka kulileta fundisho lile mpaka ndani kabisa ya moyo wake. "Nimepungukiwa na nini tena?" (Mathayo 19:20). Yeye hakuona kwamba palikuwa na kitu kilichokwenda kombo kwake wala sababu ya kutopata uzima wa milele. "Haya yote nimeyashika," akasema. Basi, Yesu akakigusa kiini cha maadili yake potofu kilichokuwa ndani ya moyo wake. Akamwambia, "Njoo unifuata, nawe utapata uzima huo."

Yeye alifanya nini? Akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.

Basi, huyo alikuwa hajazishika amri [kumi] hata kidogo. Yeye angeweza kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi wake na kuipokea haki yake. Kisha, wakati ule ambapo angekuwa na haki

ya Kristo, ndipo angeweza kuishika Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Kijana huyo mtawala asingeweza kuikanyaga Sheria ile chini ya miguu yake. Alipaswa kuiheshimu; alipaswa kuipenda. Hapo ndipo Kristo angeleta uweza wake wa uungu na kuuchanganya pamoja na juhudi za mwanadamu huyo. Kristo alitwaa ubinadamu kwa ajili yetu. Aliufunika uungu wake, kisha uungu na ubinadamu vikaunganishwa pamoja. Alionyesha kwamba Sheria ile [Amri Kumi] Shetani aliyosema haiwezi kutunzwa, ingeweza kutunzwa. Kristo alitwaa ubinadamu ili kuweza kusimama katika ulimwengu wetu, kuonyesha kwamba Shetani alikuwa amesema uongo. Alitwaa ubinadamu ili kuonyesha kwamba uungu unapounganishwa na ubinadamu, utamwezesha mwanadamu kuishika Sheria ya Yehova [Amri Kumi]. Ukiutenganisha ubinadamu mbali na uungu, hapo ndipo wewe unaweza kufanya kazi bure ukijaribu kujipatia haki yako mwenyewe kuanzia sasa mpaka hapo atakapokuja, na [kazi hiyo] itakuwa si cho chote bali kushindwa kutupu.

Kwa njia ya imani ile iliyo hai, kwa maombi ya dhati kwa Mungu, na kwa kutegemea wema wake Kristo, sisi tunavikwa haki yake, na kuokolewa. "Naam," wengine husema, "tunaokolewa ili tusifanye cho chote. Kwa kweli, mimi nimeokoka. Sihitaji kuishika Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Nimeokolewa kwa haki ya Yesu Kristo." Kristo alikuja katika dunia yetu hii kuwarudisha wanadamu wote katika utii kwa Mungu. Kuchukua msimamo kwamba wewe unaweza kuivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi], ati kwa sababu Kristo amemaliza yote, huo ni msimamo unaoelekea mautini, kwa kuwa wewe utakuwa ni mvunjaji wa Sheria kabisa kama mtu mwingine ye yote.

Basi, inakuwaje? Ni kule kusikia na kuona kwamba ikiwa wewe unayo haki ya Kristo ambayo unayo kwa imani, yaani, haki ile iliyotolewa kwa juhudi zake na uweza wake wa uungu, basi, unaweza kuzishika amri [kumi] za Mungu [kwa uweza wake].

Hatuokolewi kwa Kukaa Kivivu

Basi, tunaihitaji imani hiyo sasa. Lakini, je! mwanadamu ataokolewa ili aendelee kukaa kivivu? Je! ataokolewa kwa kukaa bila kufanya kitu cho chote? Kamwe, kamwe! Anapaswa kuwa mfanya kazi pamoja na Yesu Kristo. Hawezi kujiokoa mwenyewe. "Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu" (1 Wakorintho 3:9). Basi, inakuwa-kuwaje? Mbingu yote inafanya kazi ili kuwainua wanadamu kutoka katika aibu ya dhambi. Mbingu yote iko wazi kwa wakazi wa dunia hii. Malaika wa Mungu wanatumwa kuja kuwahudumia wale watakaourithi wokovu. "Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema" (Wafilipi 2:13).

Tena, ni imani ile itendayo kazi ambayo wewe unaihitaji. Inafanyaje kazi yake? Inafanya kazi yake kwa njia ya upendo. Upendo gani? Ni upendo ule unaoangaza kutoka kwenye msalaba ule wa Kalvari. Umesimamishwa katikati ya dunia na mbingu, na wokovu unapatikana kwa kuutazama msalaba huo. Baba ameukubali, na jeshi lile la malaika walikuja kwenye msalaba huo, na Mungu mwenyewe aliinama chini na kuikubali kafara iliyotolewa pale. Huo unatoa jibu kwa madai ya Mbingu, na mwanadamu anaweza kuokolewa kwa njia ya Yesu Kristo, iwapo tu sisi

tutakuwa na imani katika yeye. Mwanadamu anapatanishwa na Mungu, na Mungu anapatanishwa na mwanadamu, kupitia katika kafara hiyo itoshayo kabisa, iliyo kamilifu na nzima.

Basi, ndugu zangu, tunahitaji imani; tunataka kuifundisha roho yetu kuwa na imani; tunataka kila hatua tunayochukua iwe ni hatua ya imani. Tunahitaji kuwa na imani katika kafara hiyo iliyotolewa kwa ajili yetu. "Fadhili na kweli zimekutana, Haki na amani zimebusiana" (Zaburi 85:10). Basi, tunapouona mwonzi wa nuru hii tunataka kuushika. Yule mwovu anafanya kazi kinyume na huo [mwonzi] wakati wote. Ni imani itendayo kazi kwa upendo [Gal. 5:6] ambayo inashuhudiwa na Yesu Kristo juu ya msalaba ule wa Kalvari. Ni upendo wake aliokuwa nao kwa ajili ya roho yangu mimi. Kristo amekufa kwa ajili yangu mimi. Ameninunua kwa gharama kubwa mno, naye amelipa fidia kwa kila kitu [kilicho ndani yangu] ambacho ni chukizo kwake. Yanipasa kuwa mfanya kazi pamoja naye. Yanipasa mimi mwenyewe kuichukua nira yake na kuiweka juu yangu. Yanipasa kuivaa nira yake Kristo. Yanipasa kuibeba mizigo yake. Yanipasa kuwafundisha wengine jinsi wanavyoweza kuinuliwa juu kutoka katika hali ya dhambi ambayo mimi nilikuwa nayo na kuweza kuishikilia haki ile iliyo ndani yake Kristo Yesu kwa njia ya imani iliyo hai. Hiyo ndiyo njia pekee ambayo kwayo mwenye dhambi anaweza kuokolewa.

Huwezi Kujiokoa Mwenyewe

Basi, wewe unaweza kuing'ang'ania haki yako mwenyewe, nawe unaweza kufikiri kwamba umejaribu kufanya karibu kile kilicho sawa, na kwamba, hata hivyo, wewe utaokolewa kwa kufanya hivyo. Wewe unashindwa kuona kwamba ni Kristo anayefanya hayo yote. "Lazima nitubu kwanza," wengine husema. "Yanipasa kwenda mbali sana [kujitahidi sana] nikiwa najitegemea mwenyewe bila kusaidiwa na Kristo, halafu Kristo ndipo atakapokutana nami na kunikubali."

Huwezi kuwa na wazo hata moja bila Kristo. Huwezi kuwa na mwelekeo wa kuja kwake isipokuwa kama yeye ameiamsha mivuto yake na kutia muhuri wa Roho wake katika moyo wa mwanadamu. Na kama kuna mtu ye yote juu ya uso wa dunia hii ambaye anao mwelekeo wake uwao wote kwa Mungu, basi, ni kwa sababu ya mivuto mingi inayowekwa kufanya kazi ili kuyageuza mawazo yake na moyo wake. Mivuto hiyo inamtaka [mtu huyo] kumtii Mungu na kuitambua kazi kubwa ambayo Mungu amemfanyia.

Basi na tuiseme kamwe kwamba sisi [kwa uwezo wetu] wenyewe tunaweza kutubu, na ndipo Kristo atatusamehe. La, hayo si kweli. Ni wema wake Mungu unaotuongoza kwa uweza wake kufikia toba. Kwa hiyo, yote hutokana na Yesu Kristo, kila kitu chatoka kwake, na ninyi mnatakiwa tu kumrudishia Mungu utukufu wake. Mbona hamna mwamko zaidi mnapokusanyika pamoja katika mikutano yenu? Kwa nini ninyi hamna mvuto ule unaohuisha wa Roho wa Mungu wakati upendo wake Kristo na wokovu wake unapohubiriwa kwenu? Ni kwa sababu ninyi hamwoni kwamba Kristo ni wa kwanza na wa mwisho na bora kuliko wote, kisha yeye ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho, yeye ndiye Mwanzilishi hasa na Mtimizaji wa imani yetu. Ninyi hamlitambui hilo, na, kwa hiyo, ninyi mnabaki katika dhambi zenu. Mbona basi iwe hivyo? Ni

kwa sababu mahali hapo Shetani anapigana mieleka na kupigana vita ili kujipatia roho za watu. Anakitupa kivuli chake cha kishetani mbele yetu kukingama na njia yetu, na yale yote mnayoweza kuyaona [kuanzia hapo] hutoka kwa yule adui na uwezo wake.

Geuzeni macho yenu kumwanguka yule Mmoja aliye na uwezo wa kuokoa kabisa, wala msiuangalie uwezo wake [Shetani]. Mbona imani yenu haikipenyi kivuli hicho [cha Shetani] kwenda mahali pale Kristo alipo? Yeye ameteka mateka na kuwapa vipawa wanadamu. Atawafundisheni kwamba Shetani anadai kuwa ni mali yake kila mtu asiyejiunga naye [Kristo].

Jambo la Maana Sana Katika Pambano Kuu

Shetani ndiye mwanzilishi wa mauti. Kristo alifanya nini baada ya kumweka Shetani chini ya utawala wa mauti? Maneno ya Kristo ya mwisho kabisa alipokuwa akikata roho pale msalabani yalikuwa ni haya: "Imekwisha" (Yohana 19:30). Shetani akajiona ya kuwa alikuwa amevuka mpaka wake. Kifo chake Kristo kilikamilisha kifo cha Shetani na kuufunua uzima wa milele.

Kristo alifanya nini baada ya kufufuka kutoka kwa wafu? Aliitwaa mamlaka yake na kuishikilia fimbo yake ya kifalme. Aliyafungua makaburi na kuwatoa mateka wengi, akimshuhudia kila mmoja aliye katika ulimwengu wetu huu pamoja na viumbe vyote kwamba yeye alikuwa na mamlaka juu ya mauti na kwamba alikuwa amewaokoa mateka wale na mauti hiyo.

Si wote waliomwamini Yesu waliofufuliwa wakati ule. Ilikuwa ni sampuli [malimbuko] tu ya kile ambacho kingetokea [baadaye], ili sisi tupate kujua kwamba mauti na kaburi haviwezi kuwashikilia mateka [wale waliokufa] humo, kwa sababu Kristo aliwachukua na kwenda nao mbinguni [Waefeso 4:8]. Na hapo atakapokuja tena akiwa na nguvu na utukufu mwingi, atayafungua makaburi hayo [1 The. 4:16,17,(18)]. Nyumba ya kifungo chao [kaburi] itafunguliwa, na wafu watatoka tena wakiwa na mwili ule wa utukufu usioweza kufa.

Hapa wapo mateka [nyara] aliowachukua Kristo kwenda nao juu kuwaonyesha kwa ulimwengu ule wa mbinguni na kwa dunia zile nyingine [zenye watu - Ayubu 1:6-8] alizoziumba Mungu. Upendo wote waliokuwa nao kwa Lusifa [Shetani], ambaye alikuwa kerubi afunikaye [Eze. 28:14-17], sasa ukawa umetoweka kabisa. Mungu akampa nafasi ya kuikuza tabia yake. Kama [Mungu] angekuwa hajafanya hivyo, basi, wangekuwapo wale walioyaona mashtaka aliyoyaleta [Shetani] dhidi ya Mungu ambao wangesema kwamba [madai hayo ya Shetani] yalikuwa ya haki kwa vile alikuwa hajapewa nafasi nzuri ya kutekeleza mambo yake [aliyokusudia kufanya].

Mkuu wa Uzima na mkuu yule wa giza walikuwa wanapambana. Mkuu wa Uzima alishinda, lakini kwa gharama kubwa mno. Ushindi wake ndio wokovu wetu. Yeye ndiye Badala yetu na Mdamini wetu, na kile asemacho kwa ye yote anayeshinda huonyesha kama mtu huyo anacho cha kufanya au la. Kwa vipi? "Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi" (Ufunuo 3:21).

Sehemu Inayomhusu Mshindi

Je! hivi Mwokozi wetu hakuwa na kitu fulani cha kukishinda? Je! hakuendeleza mapambano yake dhidi ya mkuu yule wa giza mpaka hapo alipokuwa mshindi juu ya kila jambo? Hapo ndipo akaiacha kazi hiyo moja kwa moja mikononi mwa wafuasi wake. Tuna kitu fulani cha kufanya. Je! sisi hatunayo sehemu inayomhusu mshindi, yaani, ile ya kufanya kazi na kujipatia ushindi wetu? Je! hatupaswi kufuata hatua kwa hatua kumjua Bwana mpaka hapo tutakapojua kwamba matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale? Nuru yake itang'aa mpaka hapo tutakapoifikia ile nuru kali zaidi. Mnapomsihi sana Mungu wa mbinguni, mtaishika [nuru] hiyo na kuendelea kukusanya nuru kali zaidi kutoka katika Maandiko ya Mungu.

Yakobo alipata ushindi, na jina lake likabadilishwa siku ile. Ilikuwa ni wakati ule alipomshinda Mungu. Nimejawa na shukrani nyingi sana kwamba Mungu amefanya njia ili sisi tuweze kupata wokovu kamili na wa bure. Hatuna haja ya kuviangalia vivuli ambavyo Shetani anatutupia katika njia yetu. Yeye angetaka kuifunika kabisa kwetu mbingu ile pamoja na Yesu na nuru na uwezo ule wa mbinguni, na sisi tukabaki tukiwa tunazungumza juu ya uwezo wa Shetani. Lakini hatuna haja ya kuzungumza juu ya huo. Isaya anafafanua kwa njia hii: "Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa Ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa Amani" (Isaya 9:6). Je, maneno hayo hayasemi kwamba Mimi na Baba yangu tu umoja?

Mungu na atusaidie, ndugu zangu, ili tupate kuamka na kujitia nguvu sasa ili kufanya kiasi kama kile alichofanya yule aliyepooza; kufanya kiasi kile kile alichofanya mtu yule aliyekuwa hawezi, na kiasi kile kile alichofanya yule aliyekuwa na mkono wake uliopooza. Hao walifanya sawasawa na vile walivyoambiwa. Mungu na atusaidie kumwamini Mwana wa Mungu, naye aweze kutuokoa sisi kabisa, hapo ndipo tutakuwa na uzima wa milele.

Lakini wengi wenu mnafanya kana kwamba hamkuwa na uhai wa kutosha mioyoni mwenu katika kuitikia kweli hiyo. Baadhi yenu mnafanya kana kwamba mlidhani Yesu alikuwa amefungiwa katika kaburi jipya la Yusufu. Hayumo mle: Amefufuka kutoka kwa wafu, nasi tunaye Mwokozi aliye hai leo ambaye anatuomba

Basi, ongeeni juu ya upendo wake, ongeeni juu ya uweza wake, msifuni yeye. Kama mnayo sauti ya kusemea jambo lo lote, basi, zungumzeni juu ya mbingu, zungumzeni juu ya uzima ule wa milele. Nimesikia habari za watu ambao nyumbani mwao wanasema kwa sauti kubwa sana hata majirani zao wanaweza kuwasikia, lakini wanaposimama mkutanoni, husema maneno yao bila kuyatamka vizuri kana kwamba wamefumba mdomo wao ili maneno yao machache wanayosema yasiweze kusikika. Ninyi mnataka kujionyesha kwamba mmekuwa katika shule ya Kristo na kwamba mmekuwa mkifanya maendeleo fulani. "Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata wokovu" (Warumi 10:10). Ni wangapi wanaoziamini kweli zile mlizosisikia leo? Je, mnataka

kuendelea kwa miezi michache kabla hamjakiri kwamba nuru ilikuwamo ndani yake? Je, mnataka kusimama na kuanza kutoa hoja juu yake? Ninyi mtakuwa mmekufa kabla ya wakati ule.

Aminini Kwa Kuwa Mungu Amesema Hivyo

Iaminini kwa kuwa hiyo ndiyo kweli, kwa kuwa Mungu amesema hivyo, tena ishikilieni damu ile inayotupatia sifa njema ya Mwokozi wetu yule aliyesulibiwa na kufufuka. Yeye ndiye tumaini lenu la pekee, yeye ndiye haki yenu, yeye ndiye Badala yenu na Mdhamini wenu, yeye kwenu ni yote katika yote. Mnapoyatambua hayo, mnaweza kuleta kwake sadaka ya sifa zenu tu. Lakini mnapokuwa hamtaki kuja kwake Kristo na kukiri kwamba yeye anafanya yote hayo, mnapojisikia kwamba ni lazima mchukue kwanza hatua chache, na kwenda umbali kama huo [mnaoufikiria], ati ndipo Mungu akutane nanyi; kitendo hicho ni sawa kabisa na sadaka ile aliyotoa Kaini. Hakumjua Yesu, wala hakujua kwamba damu ya Yesu ingeweza kuzisafisha dhambi zake na kuifanya sadaka yake ipate kukubalika kwa Mungu. Kuna akina Kaini zaidi ya mmoja, wanaoleta sadaka zao zenye mawaa na kafara najisi, zisizokuwa na damu ya Yesu. Ninyi mnatakiwa kuja kwa Yesu Kristo kwa kila hatua mnayochukua. Mkiwa nayo damu ya Yesu yenye uwezo unaotakasa, basi, toeni dua zenu kwa Mungu na kumwomba kwa bidii, na kuzichunguza Biblia zenu kwa namna msivyopata kamwe kufanya huko nyuma.

Hoja yenyewe hasa ni hii, "Kweli ni nini?" Si miaka mingi niliyoamini inayoifanya iwe kweli. Mnapaswa kuleta imani ya kanisa lenu (Creed) na kuipima kwa Biblia na kuiacha nuru ya Biblia iifafanue imani ya kanisa lenu na kuwaonyesha wapi ina upungufu na tatizo lenyewe liko wapi. Biblia inapaswa kuwa ndiyo kanuni [kipimo] yenu, maandiko yale yaliyo hai ya Yehova yanatakiwa yawe kiongozi chenu. Yawapasa kuichimba kweli hiyo kama vile mnavyochimba hazina. Mnatakiwa kuipata hazina pale ilipo, kisha mnatakiwa kulima kwa plau kila inchi ili kuvipata vito vipya, almasi mpya, nanyi mtazipata.

Ninyi mnajua mambo yalivyo kwa upande wa mamlaka ile ya upapa. Watu hawana haki ya kuyafasiri Maandiko kwa faida yao wenyewe. Inawabidi kuwa na mtu fulani mwingine wa kuwafafanulia Maandiko hayo. Je! ninyi hamna akili? Hivi hamwezi kufikiri? Je! Mungu hajawapa watu wa kawaida uwezo wa kuamua mambo kama ule aliowapa makasisi [mapadre] na viongozi [wa dini]? Kristo, Bwana wa uzima na utukufu, alipokuja katika dunia yetu, kama wangukuwa wamemjua, basi, wasingaliweza kumsulibisha kamwe. Mungu amewaambia [watu wa kawaida] kuyachunguza Maandiko. "Kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia" (Yohana 5:39).

Mungu na atusaidie tupate kuwa wanafunzi wa Biblia. Mpaka hapo mtakapoweza kujionea wenyewe yalivyo [Maandiko hayo] na kuona maneno haya "hivi ndivyo asemavyo Bwana" katika Maandiko hayo, msimwamini mwanadamu ye yote aliye hai kuwatafsiria Biblia. Nanyi mtakapolielewa hilo, ndipo ninyi wenyewe mtajua, na kujua kwamba hiyo ndiyo kweli yake Mungu. Mtasema hivi, "Nimeisoma, nimeiona, na moyo wangu unaizingatia, na hiyo ndiyo kweli yake Mungu aliyoniambia kutoka katika Neno lake." Basi, hivi ndivyo tunavyotakiwa kuwa -----

Wakristo kila mmoja peke yake. Tunahitaji sisi wenyewe kujipatia uzoefu [wa maisha ya Kikristo], yaani, kila mmoja peke yake. Tunahitaji kuongoka, kama Wayahudi wale walivyofanya. Mkiiona nuru ndogo tu, msikatae na kusema, "Nitangoja mpaka ndugu zangu wote wawe wameiona." Mkifanya hivyo, mtaenda gizani.

Mungu na atusaidie sisi kuwa na ujuzi wa ile kweli, na iwapo ninyi mmekwisha kuiona nuru yake Mungu, basi, songeni mbele kuiendea nuru hiyo na kufunga mlango nyuma yenu kwa komeo. Msiwatumainie wanadamu; bali mwe na uzoefu hai [wa maisha ya Kikristo] ninyi wenyewe, hapo ndipo nyuso zenu zitakapong'aa kwa utukufu utokao kwa Mungu. Mmetembea pamoja naye, naye amewashika mkono. Mmepigana mieleka naye na kumsihi sana, naye ameacha nuru yake ipate kuwaangazia juu yenu.

Zungumzeni kwa Imani, Ishini kwa Imani, Tendeni kwa Imani

Basi, ndugu zangu, ninyi mmejizoeza sana kuwa na mashaka na maswali mengi hata ipo haja ya ninyi wenyewe kujielimisha mioyo yenu katika njia hii ya imani. Mnatakiwa kuzungumza kwa imani, mnatakiwa kuishi kwa imani, tena mnatakiwa kutenda kwa imani, ili mweze kupata ongezeko la imani yenu. Mkifanya mazoezi ya imani hiyo hai, mtakua na kuwa wanaume na wanawake hodari katika Kristo Yesu. Mungu na aukubali mkutano huu tunaouendesha hapa ili upate kuwa mkutano ambao kwa huo yule Jua la Haki [Kristo] anaweza kuwajia ninyi na kuangaza mioyoni mwenu kwa mionzi yake iliyo dhahiri kabisa, na kuwafanya ninyi nyote kuwa mianga katika ulimwengu huu.

Mnaweza kuwa kile alichosema wanafunzi wake wangukuwa ----- yaani, "nuru ya ulimwengu" (Mathayo 5:14). Ingewapasa ninyi kuitawanya nuru hiyo, na tumaini hilo, na imani hiyo kwa wengine. Haiwapasi ninyi kwenda katika njia yenu kumtumikia huku mkiwa mnapiga kite, kana kwamba yeye alikuwa Bwana mkali, anayeweka juu yenu mizigo mizito msiyoweza kuibeba. Hivyo sivyo mambo yalivyo. Yeye anataka ninyi mjazwe na furaha, mjazwe na mbaraka ule wa Mungu [Roho Mtakatifu], ili mpate kujua urefu na upana na kimo na kina cha upendo wa Mungu, upitao ufahamu wetu. Jina lake linapotajwa anataka lipige noti [sauti] ya do [ya ufunguo wa wimbo], na ndipo mioyo yenu itaweza kuitikia [sauti hiyo]. Hapo ndipo ninyi mnaweza kutoa shukrani na utukufu na heshima na sifa kwake Yeye aketiye katika kiti kile cha enzi na kwa Mwana-Kondoo.

Wimbo ule mnapaswa kujifunza kuuimba mkiwa mngali hapa [duniani]; na wakati ule mtakapobadilishwa kufumba na kufumbua, kwa dakika moja, yaani, kama kwa kupepesa macho, hapo ndipo mtakapojua noti gani mtaanzia kuuimba wimbo ule wa ushindi pamoja na malaika wale wa mbinguni na watakatifu wote waliokombolewa. Mapaa ya mbinguni tutayafanya yatoe

mwangwi kwa sifa na utukufu tutakaotoa. Basi, na tuyafanye mapaa yale kutoa mwangwi wake tukiwa hapa. Mahali hapa na paziamshe sifa zake mioyoni mwenu. Wakati mngali bado mnaikanyaga ardhi hii angalieni miti ile kule mirefu sana, zulia lile la kijani la mahameli [majani mabichi, na kadhalika], ndipo sifa na ziamshwe ndani ya mioyo yenu. Msifuni Mungu kwa kuwa sisi tumependelewa kukaa katika dunia hii, ambayo inapendeza hivyo kama ilivyo hasa. Tunakwenda mahali kuliko kuzuri zaidi. Dunia hii itasafishwa, na kuyeyushwa, na kuumbwa isiwe na dhambi.

Je! sisi hatuna kila kitu cha kutufanya tuwe na mawazo ya mbinguni [kila wakati]? Je! hatuna kila kitu cha kutuinua sisi kutoka katika hali hii ya kidunia na ya kupenda anasa, kutoka katika maongezi haya duni na ya kipuuzi, mizaha hii na dhihaka hizi tunazofanya, kutoa taarifa hizi za uongo, kupayuka-payuka huku, na kufikiriana vibaya? Wekeni mbali hayo yote! Ni aibu kubwa kwa kanisa! Mambo hayo huliondolea kanisa nguvu zake na kulidhoofisha.

Mazungumzo yetu na yawe matakatifu katika mazingira yake, hebu na sisi tuwe watakatifu katika mazingira yetu. Hebu na tumfurahie Mwokozi wetu wa thamani, aliyetufia ili kutukomboa sisi, na kuurudisha [kuuakisi] utukufu kwa Mungu. Hebu na tujiunge na mbingu katika sifa zetu hapa na kujiunga na nyimbo za malaika wale wa mbinguni walio katika mji ule wa Mungu wetu!

SURA YA 10

Taarifa ya E. G. White Kuhusu Itikio kwa Hotuba Yake ya Ottawa

Taarifa ya Mkutano wa Makambi uliofanyika pale
Ottawa, Kansas, iliyochapishwa katika gazeti la
Review and Herald, Julai 23, 1889, na tena katika
Selected Messages, Kitabu cha Kwanza, uk.355-358.

Katika mkutano ule uliofanyika Kansas ombi langu kwa Mungu lilikuwa kwamba nguvu ya adui ipate kuvunjiliwa mbali na kwamba watu wale waliokuwa gizani wapate kuifungua mioyo yao na akili zao kupokea ujumbe ule ambao Mungu angewapelekea, kwamba wangepata kuiona kweli, ambayo ni mpya kwa watu wengi, ikiwa ni kweli ya zamani katika mfumo mpya. Ufahamu wa watu wa Mungu umepofushwa, kwa sababu Shetani ameelezea vibaya tabia ya Mungu. Bwana wetu mwema na mwenye rehema ameelezwa mbele ya watu akiwa amevikwa sifa za tabia ya Shetani, tena wanaume na wanawake waliokuwa wakiitafuta kweli hiyo kwa muda mrefu sana wamemwangalia Mungu katika nuru potofu hata inakuwa vigumu kulitawanya wingu hilo linalouficha utukufu wake wasiweze kuuona. Wengi wamekuwa wakiishi katika hali ya mashaka, na inaonekana ya kwamba karibu haiwezekani kabisa kwao kulishikilia tumaini lile lililowekwa mbele yao katika injili yake Kristo....

Siku ya Sabato [Mei 11] kweli zilitolewa ambazo zilikuwa mpya kwa sehemu kubwa ya mkutano ule. Mambo mapya na ya zamani yaliletwa kutoka katika nyumba ya hazina ya Neno la Mungu. Kweli zikafunuliwa ambazo kwa shida mno watu waliweza kuzielewa na kuzitumia. Nuru ikawa imemulika kwa ghafula kutoka katika maneno yale aliyosema Mungu kuhusu Sheria [Amri Kumi] na Injili, kuhusiana na ukweli ule kwamba Kristo ni Haki yetu, mambo ambayo yalionekana kwa watu wale waliokuwa na njaa ya kuipata ile kweli kuwa ni nuru ya thamani mno kuweza kuipokea.

Lakini kazi zilizofanyika Sabato ile hazikuwa bure. Siku ya Jumapili asubuhi palikuwa na ushahidi dhahiri kwamba Roho wa Mungu alikuwa akileta mabadiliko makubwa katika hali ya kimaadili na kiroho ya wale waliokuwa wamekusanyika pale. Palikuwa na kujisalimisha akili [mawazo] na moyo kwa Mungu, na shuhuda za thamani zilitolewa na wale waliokuwa gizani kwa muda mrefu. Ndugu mmoja alizungumza juu ya pambano alilokuwa nalo moyoni mwake kabla ya kuipokea habari ile njema iliyosema kwamba Kristo ni Haki yetu. Pambano hilo lilikuwa kali, lakini Bwana alikuwa anatenda kazi ndani yake, na mawazo yake yakabadilika, na nguvu zake zikaimarishwa upya. Bwana aliiweka kweli ile mbele yake kwa maneno yaliyo wazi, akimfunulia ukweli kwamba Kristo peke yake ndiye Chimbuko la matumaini yote na wokovu. "Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu." "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; (nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba;) amejaa neema na kweli [Zaburi 119:142]" (Yohana 1:4,14).

Mmojawapo wa wachungaji wetu vijana alisema kwamba alikuwa amefurahia zaidi mbaraka ule na upendo wa Mungu katika mkutano ule kuliko kipindi kilichopita cha maisha yake yote. Mwingine alieleza kwamba maonjo, kuchanganyikiwa, na mapambano aliyokuwa ameyastahimili moyoni mwake yalikuwa ya aina ile iliyomfanya ajaribiwe kuacha kila kitu. Alikuwa amejisikia kuwa hapakuwa na tumaini lo lote kwake isipokuwa kama angepata neema nyingi zaidi ya Kristo, lakini katika mvuto uliotolewa na mikutano hii alipata badiliko la moyo wake, naye alikuwa na ufahamu bora wa wokovu kwa njia ya imani katika Kristo. Aliona kwamba ilikuwa ni haki yake kuhesabiwa haki kwa njia ya imani; alipata amani na Mungu wake, na kwa machozi alikiri kwamba alikuwa amepata faraja na mbaraka moyoni mwake. Katika kila mkutano wa ushuhuda zilitolewa shuhuda nyingi kuhusu amani, raha, na furaha watu waliyokuwa wamepata kwa kuipokea nuru hiyo.

Tunamshukuru Bwana kwa moyo wote kwamba tunayo nuru ya thamani kuihubiri mbele ya watu, nasi tunafurahi kwamba tunao ujumbe kwa wakati huu ambao ni Ukweli wa Leo. Habari njema isemayo kwamba Kristo ni Haki yetu imeleta faraja nyingi kwa wengi, yaani, kwa watu wengi sana, na Mungu anawaambia watu wake, anasema, "Endeleeni Mbele." Ujumbe kwa Kanisa la Laodikia unahusu hali ile tuliyo nayo. Kwa wazi jinsi gni imeonyeshwa picha ya hali ya wale wanaodhani kwamba wanayo kweli yote, wanaojivunia ujuzi walio nao wa Neno la Mungu, wakati uwezo wake utakasao haujaonekana katika maisha yao. Moto ule wa upendo wa Mungu haumo ndani ya mioyo yao, lakini ni moto uo huo wa upendo unaowafanya watu wa Mungu kuwa nuru ya ulimwengu.

Ujumbe wa Laodikia

Shahidi wa Kweli [Kristo] analiambia hivi kanisa lake lililo baridi, lililokufa, na lisilokuwa na Kristo, "Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu" (Ufunuo 3:15,16). Zingatia maneno haya yafuatayo: "Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi." Hapa wanawakilishwa watu maalum wanaojivunia mali waliyo nayo ya maarifa ya [ujuzi wa] kiroho na faida zake. Lakini hawajaitikia kwa kuipokea mibaraka ile wasiyostahili ambayo Mungu amewapa. wamekuwa wamejawa na uasi, utovu wa shukrani, na kumsahau Mungu; lakini yeye bado anaendelea kuwatendea kama vile baba mwenye upendo na msamaha anavyomtendea mwanawe mkaidi, asiye na shukrani. Wamepinga neema yake, wametumia vibaya haki zake, wamedharau nafasi nzuri alizowapa, tena wameridhika na kuzama chini katika utoshelevu wao, na utovu wao wa shukrani unaosikitisha mno, na desturi zao za ibada zisizokuwa na maana, na udanganyifu wao wa kinafiki. Wakiwa na kiburi kile cha Kifarisayo wamejigamba wenyewe mpaka imesemwa hivi juu yao, "Wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu" (fungu la 17).

Je! hivi Bwana Yesu hajawapelekea watu hao waliojitosheleza wenyewe ujumbe baada ya ujumbe wa makaripio, wa maonyo, wa kuwasihi? Je! mashauri yake hayajadharauliwa na kukataliwa? Je! wajumbe wake aliowatuma kwao [na ujumbe huo] hawajatendewa kwa dharau, na maneno yao kupokewa kana kwamba ni hadithi zisizokuwa na maana? Kristo anakiona kile ambacho mwanadamu hakioni. Anazona dhambi, ambazo, kama hazijatubiwa, zitaimaliza nguvu yote ya saburi yake Mungu ambaye si mwepesi wa hasira. Kristo hawezi kuyabeba kule juu majina ya wale walioridhika na utoshelevu wao wenyewe. Hawezi kuomba sana kwa ajili ya watu wale wasiojisikia kwamba wanahitaji msaada wake, yaani, wale wanaojidai kujua na kuwa na kila kitu.

Mkombozi wetu mkuu anajifananisha na mfanya biashara atokaye mbinguni, mwenye mali nyingi, anayetembea nyumba kwa nyumba, akizionyesha bidhaa zake za thamani nyingi, na kusema, "Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona. Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu.

Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami." (Ufunuo 3:18-20).

Hebu na tuifikirie hali yetu ilivyo mbele zake Mungu; hebu na tulitii shauri la Shahidi huyo wa kweli. Asiwepo mmoja wetu aliyejaa chuki isiyo na sababu, kama vile Wayahudi walivyokuwa nayo, nuru hii isije ikakosa kuingia mioyoni mwetu. Hebu na usiwepo umuhimu wo wote kwake Kristo kusema juu yetu kama alivyosema kwao maneno haya, "Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima" (Yohana 5:40).

Katika kila mkutano tangu Mkutano ule Mkuu (General Conference), watu wameupokea kwa hamu ujumbe huo wa thamani wa Haki yake Kristo. Tunamshukuru Mungu kwamba kuna watu wanaotambua kwamba wana haja na kitu fulani ambacho wao hawana ----- yaani, dhahabu ile ya imani na upendo, mavazi yale meupe ya Haki yake Kristo, dawa ile ya macho ya utambuzi wa kiroho. Endapo ninyi mtakuwa na vipawa hivyo vya thamani, basi, hekalu la moyo wenu wa kibinadamu halitakuwa kama mahali patakatifu palipotiwa unajisi. Ee ndugu na dada zangu, nawaagiza kwa jina la Yesu Kristo kufanya kazi yenu mahali pale pale Mungu anapofanya kazi yake. Sasa ndiyo siku ya nafasi nzuri iliyojaa neema na manufaa tele kwenu ninyi.

Utii na Utakaso

Makala hii ilitolewa katika gazeti la Signs of the Times,

Mei 19, 1890.

"Enendeni katika upendo, kama Kristo naye alivyotupenda sisi, tena akajitoa kwa ajili yetu, sadaka na dhabihu kwa Mungu, kuwa harufu nzuri ya manukato" (Waefeso 5:2, Tafsiri ya KJV). Katika utimilifu wake wote wa uungu, katika utukufu wote wa ubinadamu wake usio na waa, Kristo alijitoa kwa ajili yetu kama sadaka kamilifu inayotolewa bure, na kila mmoja anayekuja kwake anatakiwa ampokee kama vile ni yeye peke yake aliyelipiwa naye thamani [fidia] hiyo. Kama katika Adamu wote hufa, basi, katika Kristo wote huishi; kwa maana wale walio watiifu watafufuliwa ili wapate uzima wa milele, na yule ambaye ni mvunja sheria [mwenye dhambi] atafufuka kutoka kwa wafu ili kukabiliwa na mauti [ya pili], ambayo ni adhabu [mshahara] kwa ajili ya Sheria ile [Amri Kumi] aliyoiivunja.

Utii kwa Sheria hiyo ya Mungu [Amri Kumi] ndio Utakaso. Wako wengi walio na mawazo potofu kuhusu kazi hiyo [inayotakiwa kufanyika] ndani ya moyo wa mtu, lakini Yesu aliomba kwamba wanafunzi wake wapate kutakaswa kwa njia ya ile kweli, na kuongeza, akisema, "Neno lako ndiyo kweli" (Yohana 17:17 [Linganisha na Zaburi 119:142]). Utakaso si kazi ya ghafula [papo hapo], bali ni kazi inayoendelea daima, kama vile utii ulivyo wa daima. Kadiri Shetani anavyozidi kuyasukumiza majaribu yake juu yetu, ndivyo kadiri itakavyopaswa kupiganwa tena na tena vita ile ya kuishinda nafsi; lakini kwa njia ya utii, kweli ile itaitakasa nafsi yetu. Wale walio waaminifu kwa ile kweli, kwa njia ya wema wake Kristo, wataushinda udhaifu wao wote walio nao katika tabia zao ambao uliwafanya kufinyangwa kwa namna tofauti tofauti kulingana na kila jambo lililowapata katika maisha yao.

Madanganyo na Mtego wa Shetani

Wengi wamekuwa na msimamo usemao kwamba hawawezi kutenda dhambi ati kwa sababu wametakaswa, lakini msimamo huo ni mtego wa Shetani uliojaa udanganyifu mtupu. Kuna hatari ya kudumu ya kuweza kuanguka katika dhambi, kwa maana Kristo ametuonya tukeshe na kuomba tusije tukaingia majaribuni. Kama tunautambua udhaifu wa nafsi yetu, basi, hatutaweza kujitumainia wenyewe na kutojali tunapokabiliwa na hatari, bali tutaona haja ya kumtafuta yule aliye Chimbuko la nguvu zetu, Yesu aliye Haki yetu. Tutakuja kwake kwa toba na majuto, tukitambua hali ya kukatisha tamaa ya udhaifu wetu tulio nao, na kujifunza kwamba inatupasa

kujifunza kila siku kutumia wema wa damu yake Kristo, ili tupate kuwa vyombo vifaavyo kutumiwa na Bwana.

Tukiwa tunamtegemea Mungu kwa njia hiyo, hatutaonekana kuwa tunapigana na ile kweli, lakini sikuzote tutawezeshwa kuchukua msimamo wetu kuitetea haki. Tungeyashikilia sana mafundisho ya Biblia na kuacha kuzifuata desturi na mapokeo ya ulimwengu huu, pamoja na semi na matendo ya wanadamu.

Mafundisho potofu yanapotokea na kufundishwa kama ndiyo kweli hasa ya Biblia, hapo ndipo wale waliounganika na Kristo hawataweza kuamini yale wachungaji wao wanayosema, lakini, kama wale Waberoya waliokuwa waungwana [Matendo 17:11], watayachunguza Maandiko kila siku kuona kama mambo hayo ndivyo yalivyo. Wakigundua kwamba [mafundisho] hayo ni Neno la Mungu, basi, watachukua msimamo wao upande wa ile kweli. Wataisikia sauti ya Mchungaji yule wa Kweli akisema, "Njia ni hii, ifuateni." Kwa njia hiyo ninyi mtakuwa mmeelimishwa kuifanya Biblia kuwa mtu wenu wa kuwashauri, na sauti ya mgeni [yule asiyefuata Biblia] hamtaisikiliza wala kuifuata.

Mafundisho Mawili

Kama mtu atatakaswa na kutukuzwa, na kufanywa aweze kufaa kukaa katika majumba yale ya kifalme yaliyoko mbinguni, basi, kuna mafundisho mawili anayopaswa kujifunza ----- kujitolea mhanga na kujitawala mwenyewe. Baadhi wanajifunza mafundisho hayo muhimu kwa urahisi sana kuliko wengine, kwa maana wanazoezwa na nidhamu ile anayowapa Bwana ya upole na upendo. Wengine wanahitaji nidhamu ya polepole kwa njia ya mateso, ili moto ule utakasao upate kuitakasa mioyo yao kutokana na kiburi chao na kujitegemea wenyewe, kutokana na tamaa zao mbaya za ulimwengu huu na kule kujipenda nafsi, ili dhahabu halisi ya tabia ipate kuonekana, nao wapate kuwa washindi kwa njia ya neema yake Kristo.

Upendo wa Mungu utaiimarisha roho ya mtu, na kwa njia ya wema wa sifa za damu yake Kristo tunaweza kusimama bila kudhurika katikati ya moto wa majaribu na maonjo; lakini hakuna msaada mwingine wo wote unaoweza kufaa kutuokoa isipokuwa Kristo, Haki yetu, ambaye kwetu amefanyika kuwa hekima na utakaso na ukombozi.

Utakaso wa kweli si kitu kingine zaidi ya kumpenda Mungu kwa moyo wako wote, kwenda katika amri zake [kumi] na maagizo yake bila kuwa na lawama [hatia] yo yote. Utakaso si hisia [kujisikia moyoni], bali ni kanuni iliyotoka mbinguni ambayo inazileta tamaa zote mbaya za mwili na nyinginezo chini ya udhibiti wa Roho wa Mungu; na kazi hiyo inafanyika kwa njia ya Bwana na Mwokozi wetu.

Utakaso ule wa bandia [uongo] haumtukuzi Mungu bali unawafanya wale wanaodai kuwa wanao kujikweza na kujitukiza wenyewe. Uzoefu wo wote unaokuja katika maisha yetu ya Kikristo, kama ni furaha au huzuni, ambao haumwakisi [hauonyeshi tabia ya] Kristo wala

hauelekezi kwake kama ndiye Muasisi wa huo, ambao hauleti utukufu kwake wala kuizamisha nafsi yetu chini mahali isipoweza kuonekana, huo si uzoefu wa kweli wa maisha ya Kikristo.

Neema yake Kristo inapopandikizwa moyoni na Roho Mtakatifu, ndipo yule aliye nayo atakuwa na roho ya unyenyekevu, naye ataitafuta jamii ya wale ambao maongezi yao ni juu ya mambo yale yaliyoko mbinguni. Hapo ndipo Roho atakapoyatwaa yaliyo ya Kristo na kutuonyesha, naye atamtukuza, si yule aliyeyapokea, bali Mtoaji. Kwa hiyo, kama wewe unayo amani takatifu ya Kristo moyoni mwako, basi, kinywa chako kitajazwa na sifa na shukrani zako kwa Mungu. Sala zako, utekelezaji wa wajibu wako, ukarimu wako, kujikana nafsi kwako, mambo hayo hayatakuwa neno kuu la mawazo yako wala la maongezi yako, bali wewe utamtukuza yeye aliyejitoa nafsi yake kwa ajili yako ulipokuwa ungali mwenye dhambi. Utasema hivi: "Mimi najitoa mwenyewe kwa Yesu. Nimemwona yule ambaye Musa, katika torati yake, pamoja na manabii, waliandika habari zake." Unapomsifu yeye utapata mbaraka wa thamani, na sifa zote na utukufu wote utamrudishia Mungu kwa [cho chote] kile kinachofanyika kupitia kwako.

Si ya Makeke wala Si ile Isiyozuilika

Amani ya Kristo si tabia ile ya makeke [machachari], isiyozuilika ambayo inajidhihirisha katika makelele makubwa na misisimko ya mwili. Amani yake Kristo ni amani inayotumia akili, wala haiwafanyi wale walio nayo kuwa na dalili za ushupavu wa dini wala wazimu. Sio hisia ya kupayuka-payuka bali chimbuko lake ni kwa Mungu.

Mwokozi wetu anapompa mtu amani yake, moyo wake utakubaliana kabisa na Neno la Mungu, kwa maana Roho na Neno hupatana. Bwana analiheshimu sana Neno lake katika kushughulika kwake kote na wanadamu. Hilo ndilo mapenzi yake mwenyewe, sauti yake mwenyewe, iliyofunuliwa kwa wanadamu, na yeye hana mapenzi yake mapya, hana kweli yake mpya ya kuwafunulia watoto wake mbali na Neno lake. Kama una uzoefu wa ajabu ambao haupatani kabisa na maagizo yale yaliyokwisha kutolewa katika Neno la Mungu, basi, yakupasa kuwa na mashaka na uzoefu wako huo, maana chimbuko lake halitoki juu. Amani ya Kristo inakuja kwa kumjua Kristo ambaye Biblia inamfunua.

Iwapo furaha yako inapatikana kutoka katika vyanzo vya nje na sio kutoka kwenye Chemchemi ya Mungu, basi, itakuwa inabadilikabadilika tu kulingana na hali ya mambo inavyobadilikabadilika; lakini amani ya Kristo ni amani ya kudumu inayokaa ndani. Haitegemei hali yo yote ya mambo katika maisha yetu, wala juu ya kiasi cha mali alichu nacho mtu, wala juu ya marafiki wa kidunia alio nao. Kristo ndiye ile Chemchemi ya maji ya uzima, na furaha na amani inayopatikana kwake haitakosekana kamwe, kwa maana yeye ndiye kisima cha uzima kinachobubujika [daima]. Wale wanaomtumaini wanaweza kusema maneno haya, "Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, Ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari, Maji yake yajapovuma na kuumuka, Ijapopepesuka milima kwa kiburi chake. Kuna mto, vijito vyake vyaufurahisha mji wa Mungu, Patakatifu pa maskani zake Aliye juu" (Zaburi 46:1-4).

Tunayo sababu ya kutoa shukrani kwa Mungu bila kukoma kwa kuwa Kristo, kwa utii wake mkamilifu, ameipata tena mbingu ile aliyoipoteza Adamu kwa uasi wake. Adamu alitenda dhambi, na watoto wa Adamu wanashiriki hatia yake pamoja na matokeo yake; lakini Yesu alibeba hatia ya Adamu, na watoto wote wa Adamu wataomkimbilia Kristo, Adamu wa pili, wanaweza kuiepuka adhabu ya uasi ule. Yesu aliipata mbingu tena kwa ajili ya mwanadamu kwa kufaulu jaribio lile ambalo Adamu alishindwa kulistahimili; kwa maana yeye aliitii Sheria ile [Amri Kumi] kikamilifu, na wote wale walio na dhana sahihi juu ya mpango ule wa ukombozi wataona kwamba hawawezi kuokolewa wakati wanaendelea kuzivunja amri [kumi], takatifu, za Mungu. Yawapasa kukoma [kuacha kabisa] kuivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi] na kuzishikilia ahadi za Mungu ambazo zimetolewa kwa ajili yetu kwa njia ya wema wake Kristo.

Usiwatumainie Wanadamu

Imani yetu haitakiwa kujengwa juu ya uwezo wa wanadamu, bali katika uweza wa Mungu. Ipo hatari kubwa ya kuwatumainia wanadamu, hata kama wao wametumika kama vyombo vya Mungu kwa kufanya kazi kubwa na nzuri. Kristo hana budi kuwa nguvu yetu na kimbilio letu. Watu wale walio wema sana wanaweza kuanguka kutoka katika unyofu wao, na dini bora kuliko zote, ikipotolewa, inakuwa ya hatari mno katika mvuto wake juu ya mioyo ya watu. Dini iliyo safi, iliyo hai, inapatikana kwa njia ya utii kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Haki huliinua taifa, ukosefu wa hiyo hulidhalilisha na kumwangamiza mwanadamu.

"Amini, Amini Tu"

Kutoka kwenye mimbara za siku hizi maneno haya hutamkwa: "Amini, amini tu. Uwe na imani katika Yesu; hutakiwi kufanya jambo lo lote kuhusiana na Sheria ile ya zamani [Amri Kumi], wewe umtumainie tu Kristo." Maneno hayo hutofautiana jinsi gani na maneno yale ya nabii anayetangaza kwamba imani pasipo matendo imekufa. Anasema hivi, "Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu" (Yakobo 1:22). Yatupasa kuwa na imani le itendayo kazi kwa upendo na kuitakasa nafsi. Wengi wanatafuta kuwa na imani ya juu juu tu badala ya kuwa na unyofu wa maisha, nao wanadhani kwa njia hiyo watajipatia wokovu.

Bwana anataka leo hii [wakati huu] kile kile alichokitaka kwa Adamu kule Edeni ----- yaani, utii mkamilifu kwa Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Yatupasa kuwa na haki ile isiyokuwa na waa, yaani, isiyokuwa na dosari yo yote. Mungu alimtoa Mwanawe kuufia ulimwengu huu, lakini yeye hakufa ili kuitangua Sheria [Amri Kumi au Torati] ambayo ilikuwa takatifu, na ya haki, na njema [Warumi 7:12]. Kafara ya Kristo pale Kalvari ni hoja isiyokanushika inayoonyesha kule

kutokubadilika kamwe kwa Sheria hiyo [Amri Kumi]. Adhabu yake [kwa kuivunja] aliipata Mwana wa Mungu kwa niaba ya mwanadamu mwenye hatia, ili kwa njia ya wema wake, yule mwenye dhambi apokee tabia yake [Kristo] njema isiyo na waa kwa njia ya imani katika jina lake.

Mwenye dhambi alipewa nafasi ya pili ili apate kuishika Sheria ya Mungu [Amri Kumi] kwa uweza wa Mkombozi wake yule wa Kimbingu. Msalaba ule wa Kalvari unalihukumu milele wazo la Shetani aliloliweka mbele ya ulimwengu wa Kikristo, kwamba kifo cha Kristo hakikuitangua tu Sheria ile ya Kafara [Dhabihu] pamoja na ibada zake, bali [kiliitangua pia] Sheria ya Mungu [Amri Kumi], ambayo ndiyo msingi wa kiti chake cha enzi, chapa [nakala halisi] ya tabia yake.

Kwa kila hila iwezekanayo Shetani amejaribu kuibatilisha kafara ile ya Mwana wa Mungu, kuifanya fidia yake aliyolipa iwe haina maana yo yote, na utume wake uwe umeshindwa kabisa [kultimiza kusudi lake]. Amedai kwamba kifo chake Kristo kilifanya utii kwa Sheria hiyo [Amri Kumi] usiwe wa lazima na kumruhusu mwenye dhambi kupata upendeleo wa Mungu pasipo kuachana kabisa na dhambi zake. Amewatangazia kwamba kanuni ile [kipimo] ya Agano la Kale [Amri Kumi] ilishushwa chini na Injili, na kwamba wanadamu wanaweza kuja kwa Kristo, si kwa kusudi la kuokolewa kutoka katika dhambi zao, bali kuokolewa [pamoja] na dhambi zao.

Lakini Yohana [Mbatizaji] alipomwona Yesu alisimulia habari za utume wake. Alisema, "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" (Yohana 1:29). Kwa kila mtu anayetubu ujumbe ni huu, "Haya, njoni, tusemezane, asema BWANA. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu sana kama bendera, zitakuwa kama sufu" (Isaya 1:18).

SURA YA 12

Kuitumia Haki ya Kristo Katika Maisha Yetu

Makala hii ya kawaida, yenye kichwa "Udhaifu

wa Kiroho Hausameheki," ilitolewa katika gazeti
la Review and Herald, Julai 1, 1890. Sehemu yake
imo katika Selected Messages, Kitabu cha Kwanza,
uk. 363,364.

Wale wanaoitumainia kabisa haki yake Kristo, wakimtazama yeye kwa imani iliyo hai, wanamjua Roho wa Kristo, nao wanajulikana na Kristo. Imani ya kawaida tu humwezesha muumini huyo kujihesabu mwenyewe kwamba ameifia dhambi na kwamba yeye yu hai kwa Mungu kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu. Tunaokolewa kwa neema kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zetu, ni kipawa cha Mungu. Tungeweza kuzifunua ahadi hizo za thamani kwa wenye hekima wa dunia hii, wangetudhihaki tu; kwa maana "mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni" (1 Wakorintho 2:14).

Yesu alipokuwa karibu kupaa juu, aliwaambia wanafunzi wake maneno haya, "Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu" (Yohana 14:16,17). Kisha akasema, "Yeye aliye na amri zangu [kumi], na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake" (fungu la 21).

Kuna wengi wanaoridhika na kujiambatanisha na mafundisho ya uongo, hata hakuna usumbufu wo wote wala tofauti yo yote kati yao na ulimwengu; lakini watoto wa Mungu hawana budi kuishuhudia kweli, si kwa kalamu tu na sauti zao bali kwa nafsi na tabia zao. Mwokozi wetu anatangaza kwamba ulimwengu hauwezi kumpokea Roho wa kweli. Hawawezi kuifahamu kweli, maana hawamtambui Kristo, Muasisi wa kweli hiyo. Wafuasi wake walio na uvuguvugu, wanaojidai hivyo, walio na mioyo baridi, ambao hawajajazwa na Roho wa Kristo, hawawezi kuitambua thamani ya haki yake; bali wao wanajifanyia haki yao wenyewe.

Ulimwengu unatafuta mambo ya ulimwengu ----- biashara, heshima ya ulimwengu huu, kujionyesha, kujitosheleza nafsi zao. Kristo anataka kuivunjilia mbali nguvu hiyo ya uchawi iliyowaduwa na kuwazuia wanadamu wasije kwake. Anataka kuyageuza mawazo ya wanadamu na kuyaelekeza kwenye ulimwengu ule ujao, ambao Shetani alikuwa ameufunika kabisa kwa kivuli chake. Kristo anauleta ulimwengu ule wa milele katika upeo wa macho ya wanadamu, anaviweka vivutio vyake mbele yao, anawaambia kwamba anawaandalia makao, naye atakuja tena na kuwakaribisha kwake. Ni mbinu ya Shetani kuujaza moyo na tamaa nyingi mno ya mambo ya kimwili kiasi kwamba upendo kwa Mungu na tamaa ya kutaka kwenda mbinguni vitaondolewa mbali kutoka moyoni....

Tumeitwa Kuwa Mwakili Waaminifu

Mungu anawaagiza wale aliowakabidhi mali yake kuwa kama mawakili wake waaminifu. Bwana angetaka mambo yote ya kidunia yanayotupendeza sisi yapewe nafasi ya pili katika moyo na mawazo yetu; lakini Shetani angetaka mambo ya dunia hii yapewe nafasi ya kwanza katika maisha yetu. Bwana angependa kwamba sisi tuyakubali mambo yale yaliyo bora sana. Anatuonyesha pambano lile ambalo hatuna budi kupambana nalo, anatuonyesha asili na mpango ule wa ukombozi. Anaweka wazi mbele yenu hatari kubwa mtakazokabiliana nazo, kujikana nafsi kwenu kutakakotakiwa, kisha anawaagiza kuihesabu gharama, akiwahakikishia ya kwamba kama mtaingia katika pambano hilo kwa bidii, basi, uweza wa Mungu utaunganika na juhudi yenu ya kibinadamu.

Vita ya Mkristo si vita anayopigana na nyama na damu bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Mkristo analazimika kupambana na majeshi yasiyokuwa ya kibinadamu, lakini haachwi peke yake kupambana nayo. Mwokozi ndiye Kapteni wa wokovu wake, na mwanadamu akiwa naye, basi, anaweza kuwa zaidi ya mshindi.

Mkombozi wa ulimwengu huu asingependa kumwacha mwanadamu ye yote katika ujinga wa kutokuzijua hila za Shetani. Muungano mkubwa sana wa nguvu zile za uovu umejipanga dhidi ya wale ambao wangependa kupata ushindi; lakini Kristo angependa sisi tuyaangalie mambo yale yasiyoonekana, yaani, majeshi yale ya mbinguni ambayo yanafanya kituo kuwazunguka wale wampendao Mungu, ili kuwaokoa. Malaika wale wa mbinguni wanapendezwa na mwanadamu. Uweza wa Mungu Mwenyezi uko tayari kuwahudumia wale wanaomtumainia Mungu. Baba anaikubali haki ya Kristo kwa ajili ya wafuasi wake, nao wamezungukwa na nuru pamoja na utakatifu asioweza kuupenya Shetani. Sauti ya Kapteni wa wokovu wetu inawaambia wafuasi wake, ikisema, "Jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu. Mimi ndimi kinga yenu; songeni mbele kwenye ushindi."

Msalaba wa Kalvari

Kwa njia yake Kristo, uponyaji pamoja na upatanisho vimeandaliwa kwa ajili ya mwanadamu. Ufa ule uliofanywa na dhambi umeunganishwa kwa njia ya msalaba ule wa Kalvari. Fidia kamili imelipwa na Yesu, kwa hiyo yule mwenye dhambi anasamehewa zake na ile haki ya sheria inadumishwa. Wote wanaoamini kwamba Kristo ndiye sadaka ile ya fidia, wanaweza kuja na kupokea msamaha kwa ajili ya dhambi zao; maana kwa njia ya wema wa Kristo, mawasiliano yamefunguliwa kati ya Mungu na mwanadamu. Mungu anaweza kunikubali mimi kama mtoto wake, na mimi naweza kumdai yeye kama Baba yangu anipendaye na kufurahi katika yeye.

Matumaini yetu ya mbinguni ni lazima tuyaweke ndani ya Kristo peke yake, kwa kuwa yeye ndiye Badala yetu na Mdamini wetu. Sisi tumeivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi], na kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki. Juhudi bora kabisa ambazo mwanadamu anaweza kufanya kwa nguvu zake mwenyewe hazina faida yo yote katika kuitimiza Sheria yake takatifu na ya haki ilivyovunjwa; lakini kwa njia ya imani anaweza kuidai haki ya Mwana wa Mungu kuwa inatosha kabisa kwake. Kristo aliyatosheleza madai ya sheria katika asili yake ya kibinadamu. Alichukua laana ya Sheria kwa ajili ya mwenye dhambi, alifanya upatanisho kwa ajili yake, "ili kila mtu amwaminiye asipotee [asiangamie] bali awe na uzima wa milele." Imani ya kweli inaitumia haki ya Kristo katika maisha ya mtu huyo, na mwenye dhambi huyo anafanywa kuwa mshindi pamoja na Kristo; kwa kuwa anafanywa kuwa mshirika wa tabia ya uungu na kwa njia hiyo uungu huo huunganishwa na ubinadamu.

Yule anayejaribu kuingia mbinguni kwa matendo yake mwenyewe kwa kuishika Sheria [Amri Kumi] anajaribisha jambo lisilowezezana. Mwanadamu hawezi kuokolewa pasipo kuwa na utii, lakini matendo yake yasitokane na nafsi yake mwenyewe; Kristo anapaswa kufanya kazi ndani yake, kutaka kwake na kutenda kwake, kwa kulitimiza kusudi lake jema. Kama mtu angeweza kujiokoa mwenyewe kwa matendo yake, basi, angekuwa na kitu fulani cha kujisifia ndani ya nafsi yake. Juhudi anayofanya mtu kwa nguvu zake mwenyewe ili kujipatia wokovu inafananishwa na sadaka ya Kaini. Yote yale awezayo kufanya mwanadamu pasipo Kristo yamechafuliwa na ubinafsi na dhambi; lakini kile kinachofanyika kwa njia ya imani kinakubaliwa na Mungu. Tunapojaribu kujipatia mbingu kwa njia ya wema wake Kristo, hapo ndipo mtu anapofanya maendeleo [katika maisha yake ya kila siku]. "Tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu," tunaweza kusonga mbele toka nguvu hata nguvu, toka ushindi hata ushindi; kwa maana kwa njia ya Kristo neema ya Mungu imetupatia wokovu kamili.

SURA YA 13

Imani na Matendo ----- Bega kwa Bega

Makala hii ilitolewa katika gazeti la Signs of the Times,

Julai 21, 1890, ikiwa na kichwa cha "Nifanye Nini Nipate

Kuurithi Uzima wa Milele?"

Yesu alikuja ili kuwaokoa watu wake kutoka katika dhambi zao, na ukombozi ndani ya Kristo unamaanisha kukoma kuivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi] na kuwa huru mbali na kila dhambi; hakuna mtu ye yote aliyechochewa kuwa na uadui dhidi ya Sheria ya Mungu [Amri Kumi] awezaye kupatana na Kristo aliyeteswa pale Kalvari kuitetea na kuitukuza Sheria hiyo [Amri Kumi] mbele ya ulimwengu.

Wale wanaodai kwa ushupavu kuwa wanao utakatifu wanathibitisha kwa usemi wao huo kwamba hawajiangalii wenyewe katika nuru ya Sheria hiyo [Amri Kumi]; kwamba hawajaelimika kiroho, wala hawachukii kila aina ya uchoyo [ubinafsi] na kiburi. Kutoka kwenye midomo yao yenye dhambi hutoka maneno haya ya ukinzani: "Mimi ni mtakatifu, Mimi sina dhambi. Yesu ananifundisha mimi ya kuwa nikiishika Sheria [Amri Kumi], basi, nitakuwa nimeanguka kutoka katika neema. Sheria [Amri Kumi] ni kongwa la utumwa." Bwana asema hivi, "Heri wale wazishikao amri zake, wawe na haki kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake" [Ufunuo 22:14, Tafsiri ya KJV]. Yatupasa sisi kujifunza Neno la Mungu kwa uangalifu ili tupate kufikia maamuzi sahihi, na kutenda itupasavyo; maana hapo ndipo tutakuwa tunalitii Neno la Mungu na kuwa katika mwafaka na Sheria takatifu ya Mungu [Amri Kumi].

Hatuokolewi kwa Kuishika Sheria Wala kwa Kuivunja

Ingawa tunatakiwa kuishi kulingana na Sheria hiyo ya Mungu [Amri Kumi], sisi hatuokolewi kwa matendo ya sheria, hata hivyo, hatuwezi kuokolewa pasipo kuwa na utii. Sheria hiyo [Amri Kumi] ndiyo kanuni [kipimo] ambayo kwayo tabia yetu hupimwa. Lakini sisi hatuwezi kuzishika amri [kumi] za Mungu pasipo kuwa na neema ya Mungu inayotuzaa mara ya pili. Ni Yesu peke yake awezaye kutusafisha na dhambi zote. Yeye hatuokoi sisi kwa njia ya Sheria [Amri Kumi], wala hatatuokoa sisi kama tunaendelea kuivunja Sheria hiyo [Amri Kumi].

Upendo wetu kwa Kristo utakuwa kwa kiwango kile kile kinacholingana na kuhakikishiwa [kujulishwa] dhambi zetu [Luka 7:47], na kwa njia ya Sheria hiyo [Amri Kumi] sisi tunaweza kujua dhambi ni nini [Warumi 7:7]. Lakini tunapojiangalia wenyewe, hebu na tuangalie mbali nasi kwa Yesu, aliyejitoa nafsi yake kwa ajili yetu ili apate kutukomboza kutoka katika dhambi zote. Kwa imani shikilia wema wake Kristo, na damu ile inayoitakasa nafsi itatumika. Kadiri tunavyoweza kuyaona kwa wazi zaidi maovu na hatari kubwa zinazotukabili, ndivyo kadiri tutakavyozidi kuwa na shukrani nyingi kwa ukombozi huo kwa njia yake Kristo. Injili yake Kristo haiwapi watu leseni ya [kibali cha] kuivunja Sheria yake [Amri Kumi], maana ilikuwa ni kwa njia ya uvunjaji wa Sheria hiyo [Amri Kumi] ilipofunguliwa ile milango ya kufungia maji [kwenye bwawa kubwa] na kuleta maafa makubwa juu ya ulimwengu wetu huu.

Leo bado dhambi ni kitu kile kile cha kuchukiza mno kama ilivyokuwa siku zile za Adamu. Injili haitoi ahadi ya kupewa upendeleo wa Mungu mtu ye yote ambaye kwa moyo wake usio na toba anaivunja Sheria yake [Amri Kumi]. Unyonge wa moyo wa kibinadamu, hatia inayotokana na uvunjaji wa Sheria hiyo [Amri Kumi], maangamizi ya dhambi, vyote hivyo vinafunuliwa kwa njia ya msalaba ambao kwa huo Kristo ametufanyia njia ya kuokolewa.

Fundisho Lililojaa Udanganyifu Mtupu

Haki yetu wenyewe ndiyo hatari inayokikabili kizazi hiki; inamtenga mtu mbali na Kristo. Wale wanaotumainia haki yao wenyewe hawawezi kufahamu wokovu unavyokuja kwa njia ya Kristo. Wanaiita dhambi kuwa ndiyo haki, na haki kuwa ndiyo dhambi. Hawana ufahamu wote kuhusu uovu unaotokana na kuvunja Sheria [Amri Kumi], hawaijui hofu inayoletwa na Sheria hiyo [Amri Kumi]; kwa sababu hawaiheshimu kanuni hiyo ya Mungu ya Maadili [Amri Kumi]. Badala ya kanuni hiyo ya Mungu ya haki [Amri Kumi], watu wamejiwekea kanuni yao wenyewe ya kuipima tabia. Wanaona kwa utusitisi katika kioo na kufundisha kwa watu maoni yao ya uongo juu ya utakaso, hivyo wanaiendeleza hali ya kujikinai, kiburi, na haki yao wenyewe. Fundisho la utakaso linalotetewa sana na wengi limejaa udanganyifu mtupu, kwa vile linavutia sana kwa moyo ule wa asili [usioongoka], lakini jambo jema sana linaloweza kuhubiriwa kwa mwenye dhambi ni

ukweli ule unaohusu madai ya Sheria ya Mungu [Amri Kumi] yanayowafunga wanadamu wote. Imani na matendo havina budi kwenda bega kwa bega; kwa maana imani bila matendo imekufa.

Kulipima Fundisho la Biblia

Nabii huyo anatangaza ukweli ambao kwa huo tunaweza kuyapima mafundisho yote ya Biblia. Anasema, "Na waende kwa Sheria [Amri Kumi] na Ushuhuda [Biblia]; ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi [wamo gizani]" (Isaya 8:20). Ingawa mafundisho ya uongo [potofu] yamezagaa sana ulimwenguni humu, hakuna sababu ya watu kubaki katika udanganyifu huo. Kweli inaeleweka wazi, nayo ikipambanishwa na uongo [mafundisho potofu], tabia yake inaweza kufahamika. Raia wote wa neema ya Mungu wanaweza kufahamu kile kinachotakiwa kwao. Kwa imani tunaweza kuyalinganisha maisha yetu na kanuni hiyo ya haki [Amri Kumi], kwa sababu tunaweza kujipatia haki ya Kristo.

Katika Neno la Mungu mtafutaji mwaminifu ataipata kanuni ya utakaso ule wa kweli. Mtume asema hivi, "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, [wasioenenda kwa kuufuata mwili bali kwa kuifuata roho - KJV]... Maana yale yasiyowezekana kwa Sheria [Amri Kumi], kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili; ili maagizo ya torati [Sheria ile ya Amri Kumi] yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho. Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho. Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii Sheria ya Mungu [Amri Kumi], wala haiwezi kuitii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu. Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho." (Warumi 8:1-9).

SURA YA 14

Uzoefu wa Maisha ya Haki kwa Imani Wafafanuliwa kwa Muhtasari

Sehemu ya makala hii ilitolewa katika gazeti la
Review and Herald, Novemba 4, 1890, ikiwa na
kichwa cha "Kristo Njia ya Uzima." Ilichapishwa
katika Selected Messages, Kitabu cha Kwanza,
uk. 365-368.

"Yesu akaenda Galilaya, akihubiri Habari Njema ya
Mungu, akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu
umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili" (Marko 1:14,15).

Toba inaunganishwa na imani, tena inasisitizwa katika Injili kuwa ni ya muhimu sana kwa wokovu. Paulo alihubiri toba. Alisema, "Ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia neno lo lote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba, nikiwashuhudia Wayahudi na Wayunani wamtubie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo" (Matendo 20:20,21). Hakuna wokovu pasipo toba. Hakuna mwenye dhambi ye yote asiye na toba awezaye kuamini kwa moyo wake hata kupata wokovu. Toba inaelezwa na Paulo kama huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu kwa ajili ya dhambi ambayo "hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto" (2 Wakorintho 7:10). Toba hii ndani yake haina tabia yo yote ya kujisifu, bali inautayarisha moyo kumpokea Kristo kama Mwokozi peke yake, tumaini la pekee kwa mwenye dhambi aliyepotea.

Mwenye dhambi anapoiangalia Sheria [Amri Kumi], hatia yake inaonekana wazi kwake na kusisitizwa katika dhambi yake, naye anahukumiwa kuwa ana hatia. Faraja yake na tumaini lake pekee hupatikana kwa kuutazama msalaba ule wa Kalvari. Anapojipa moyo na kuzidai ahadi zake,

akimwamini Mungu kama asemavyo katika neno lake, faraja na amani huja moyoni mwake. Anapaza sauti yake, na kusema, "Bwana, Wewe umeahidi kuwaokoa wote wanaokuja kwako katika jina la Mwanao. Mimi ni mtu niliyepotea, nisiye na matumaini yo yote. Bwana, niokoe, la sivyo, mimi nitaangamia." Imani yake inamshika Kristo, kisha anahesabiwa haki mbele za Mungu.

Ingawa Mungu anaweza kuwa mwenye haki, na bado akawa mwenye kumhesabia haki mwenye dhambi huyo kwa njia ya wema wake Kristo, hakuna mtu ye yote anayeweza kuivika nafsi yake na mavazi yale ya haki ya Kristo wakati anaendelea kutenda dhambi zinazojulikana [kwake], au wakati anaacha kufanya majukumu anayoyajua. Mungu anataka tuusalimishe moyo wetu wote kwake, kabla kuhesabiwa haki hakujatokea; tena, ili mtu apate kuendelea kuhesabiwa haki hiyo, ni lazima pawe na utii wa kudumu, kwa njia ya imani hai itendayo kazi kwa upendo na kuitakasa nafsi yake.

Yakobo anaandika habari za Ibrahimu na kusema, "Je! baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipomtoa Isaka mwanawe juu ya madhabahu? Waona kwamba imani inatenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale. Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye alitwa rafiki wa Mungu. Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake" (Yakobo 2:21-24). Ili mwanadamu apate kuhesabiwa kuwa ana haki kwa njia ya imani, ni lazima imani yake ifikie mahali itakapoyadhibiti mapenzi na hisia za moyo wake; tena, ni kwa njia ya utii imani yenyewe inakamilishwa.

Imani ni Sharti la Ahadi

Pasipo neema yake Kristo, mwenye dhambi yuko katika hali isiyo na matumaini; hakuna lo lote liwezalo kufanyika kwa ajili yake; lakini kwa njia ya neema ya Mungu, uweza wa Mungu hutolewa kwa mwanadamu huyo na kufanya kazi katika akili na moyo na tabia yake. Ni kwa njia ya kupewa neema yake Kristo ndipo dhambi inaweza kutambuliwa katika hali yake ya kuchukiza mno na hatimaye kuondolewa mbali kutoka katika hekalu la mwili. Ni kwa njia ya neema sisi tunaletwa katika ushirika na Kristo, yaani, tunashirikiana naye katika kazi ile ya wokovu wetu. Imani ndilo sharti ambalo kwalo Mungu ameona inafaa kutoa ahadi ya msamaha kwa wenye dhambi; si kwamba kuna wema wo wote ndani ya imani hiyo ambao kwa huo wokovu unastahili kupokewa, bali kwa sababu imani inaweza kuushikilia wema wake Kristo, yaani, dawa ile iliyotolewa kwa ajili ya kuitibu dhambi. Imani inaweza kudai utii kamili wa Kristo kuwa badala ya uvunjaji wake wa Sheria [Amri Kumi] na usaliti wake yule mwenye dhambi. Mwenye dhambi anapoamini kwamba Kristo ni Mwokozi wake binafsi, ndipo kwa mujibu wa ahadi zake zisizoweza kushindwa, Mungu anaisamehe dhambi yake na kumhesabia haki bure. Mtu yule aliyetubu anatambua kwamba kuhesabiwa haki kwake kunakuja kwa sababu Kristo, kama Mmoja aliye Badala yake na Mdamini wake, amekufa kwa ajili yake, kwamba yeye ndiye upatanisho wake na haki yake.

"Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki. Lakini kwa mtu afanyaye kazi, ujira wake hauhesabiwi kuwa ni neema, bali kuwa ni deni. Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki" (Warumi 4:3-5). Haki ni utii kwa Sheria [Amri Kumi]. Sheria hiyo hudai haki, na hilo ndilo deni mwenye dhambi analowiwa na Sheria hiyo [Amri Kumi]; lakini hawezi kabisa kuitoa hiyo [haki]. Njia pekee ambayo kwayo anaweza kuifikia haki hiyo ni kwa imani. Kwa imani anaweza kumletea Mungu sifa za tabia ya Kristo, na Bwana anaweka utii wa Mwanawe kwenye akaunti ya mwenye dhambi huyo. Haki yake Kristo inakubaliwa badala ya kushindwa kwake mwanadamu, naye Mungu anampokea na kumsamehe na kumhesabia haki mwenye dhambi yule atubuye na kuamini, akimtendea kana kwamba alikuwa mwenye haki, tena anampenda kama vile ampendavyo Mwanawe. Hii ndiyo jinsi imani inavyohesabiwa kuwa haki; na mtu yule aliyesamehewa anasonga mbele toka neema hata neema, toka nuru kwenda kwenye nuru kubwa. Anaweza kusema hivi kwa furaha nyingi sana, "Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu, ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu; ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu" (Tito 3:5-7).

Tena: imeandikwa hivi, "Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliamini jina lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu" (Yohana 1:12,13). Yesu alitangaza hivi, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu" (Yohana 3:3). "Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu" (fungu la 5). Hicho si kiwango cha chini ambacho kimewekwa mbele yetu, kwa kuwa inatupasa kuwa watoto wake Mungu. Tunapaswa kuokolewa kama mtu mmoja mmoja, na katika siku ile ya kujaribiwa [kupimwa] na maonjo tutaweza kupambanua kati ya yule amtumikiaye Mungu na yule asiyemtumkia. Sisi kama waumini tunaokolewa mmoja mmoja katika Bwana wetu Yesu Kristo.

Wengi wanaipeleza njia ile ya kweli, hayo ni matokeo ya kufikiri kwao kwamba wanapaswa kupanda kwenda mbinguni, kwamba yawapasa kufanya kitu fulani kuweza kustahili kupewa upendeleo wa Mungu. Wanajaribu kujifanya wenyewe kuwa wema zaidi kwa nguvu zao wenyewe bila kupata msaada [wa Kristo]. Jambo hilo hawawezi kamwe kulitimiza. Kristo ametayarisha njia kwa kufa kama kafara [sadaka] yetu, kwa kuishi maisha yake kama Kielelezo chetu, kwa kuwa Kuhani wetu Mkuu. Yeye anatangaza hivi, "Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima" (Yohana 14:6). Endapo kwa juhudi yetu iwayo yote ile tungeweza kusonga mbele kupanda juu ya ngazi ile kwa hatua moja, basi, maneno hayo ya Kristo yasingekuwa ya kweli. Lakini tunapompokea Kristo, ndipo matendo mema yatakapotokea yenyewe kama ushahidi unaozaa matunda uonyeshao kwamba sisi tu katika njia ile ya uzima, na kwamba Kristo ndiye njia yetu, na kwamba tunakanyaga katika njia ile ya kweli iendayo mbinguni.

Yeye Anakuwa Haki Yetu

Kristo anaangalia roho tuliyo nayo, naye anapotuona sisi tukibeba mzigo wetu kwa imani, basi, utakatifu wake ulio mkamilifu unafidia mapungufu yetu. Tunapofanya kila tuwezalo, hapo ndipo yeye anakuwa haki yetu. Inachukua kila mwonzi wa nuru anaotutumia Mungu kuweza kutufanya sisi kuwa nuru ya ulimwengu ----- Letter 33, 1889.

SURA YA 15

Huko Ndiko Kuhesabiwa Haki kwa Imani

Hii ni sehemu ya Manuscript 21, 1891, iliyoandikwa
katika mwezi wa Februari 27, 1891. Ilichapishwa
katika SDA Bible Commentary, Gombo la 6,
uk. 1070,1071.

Mwenye dhambi aliyetubu, aliye na majuto mbele za Mungu, anapoutambua upatanisho wa Kristo uliofanywa kwa ajili yake na kuukubali upatanisho huo kama ndilo tumaini lake la pekee katika maisha haya na yale ya baadaye, hapo ndipo dhambi zake husamehewa. Huko ndiko kuhesabiwa haki kwa imani. Kila mtu aaminiye anatakiwa kuyafanya mapenzi yake yapatane kabisa na yale ya Mungu na kuwa katika hali ya toba na majuto, yaani, kuitumia imani yake kwa

kuuamini wema unaopatanisha wa Mkombozi huyo na kuendelea [kukua] toka nguvu hata nguvu, toka utukufu hata utukufu.

Msamaha na Kuhesabiwa Haki ni kitu kile kile kimoja. Kwa njia ya imani, muumini anahama kutoka mahali pa mwasi, yaani, mtoto wa dhambi na wa Shetani, kwenda mahali pa raia mtiifu wa Kristo Yesu, si kwa sababu ya wema wo wote uliomo ndani yake, bali kwa sababu Kristo anampokea kama mtoto wake wa kupanga [kuchaguliwa]. Mwenye dhambi huyo hupokea msamaha wa dhambi zake, kwa sababu dhambi hizo zinabebwa na yule aliye Badala yake na Mdamini wake. Bwana anamwambia Baba yake wa mbinguni, anasema, "Huyu ni mwanangu. Namwachilia kwa muda asipatwe na hukumu ile ya kifo, nampa hati ya Bima ya Maisha yangu ---- - yaani, uzima wa milele ----- kwa sababu mimi nimekuwa badala yake, tena nimeteswa kwa ajili ya dhambi zake. Yeye ni mwanangu mpendwa." Kwa njia hiyo mtu yule aliyesamehewa na kuvikwa mavazi mazuri ya haki yake Kristo, anasimama mbele za Mungu akiwa hana hatia yo yote.

Mwenye dhambi huyo [aliyesamehewa] huenda akafanya makosa [dhambi], lakini hatupwi pasipo kumwonea rehema. Hata hivyo, tumaini lake la pekee ni kuwa na toba kwa Mungu na imani katika Bwana wake Yesu Kristo. Ni haki ya Baba kusamehe uvunjaji wetu wa Sheria [Amri Kumi] pamoja na dhambi zetu, kwa vile Kristo ameichukua juu yake mwenyewe hatia yetu na kutuachilia, akituhesabia sisi haki yake mwenyewe. Kafara yake huyatosheleza kabisa madai ya ile haki [Amri Kumi].

Kuhesabiwa Haki ni kinyume cha Kuhukumiwa kuwa una hatia. Rehema ya Mungu isiyokuwa na mipaka hutolewa kwa wale wasiostahili kabisa. Anasamehe uvunjaji wao wa Sheria [Amri Kumi] pamoja na dhambi zao kwa ajili yake Yesu, ambaye amekuwa kipatanisho kwa dhambi zetu. Kwa njia ya imani katika Kristo, mwenye dhambi aliye na hatia analetwa katika upendeleo wa Mungu na katika tumaini thabiti la uzima ule wa milele.

SURA YA 16

Twakubalika Katika Kristo

Makala hii ilitolewa katika gazeti la Signs of the Times,

Julai 4, 1892.

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16). Ujumbe huu ni kwa ajili ya ulimwengu mzima, kwa maana "kila mtu" humaanisha kwamba ye yote na wote wale wanaotimiza sharti hilo wanaweza kuushiriki mbaraka huo. Wote wamtazamao Yesu, wakimwamini kwamba ni Mwokozi wao binafsi, hawata"pote[a], bali [watakuwa] na uzima wa milele." Maandalizi yote yamefanywa ili sisi tuweze kuipata ile thawabu ya milele.

Kristo ndiye Kafara yetu, Badala yetu, Mdhamini wetu, Mwombezi wetu wa mbinguni; yeye amefanywa kwetu kuwa haki, utakaso, na ukombozi. "Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu" (Waebrania 9:24).

Maombezi ya Kristo kwa Baba yake kwa ajili yetu ni yale ya kutuwekea sisi wema wake kutokana na kujitoa kwake kama Badala yetu na Mdhamini wetu; maana alipaa juu kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, "Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote" (1 Yohana 2:1,2). "Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpa Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu" (1 Yohana 4:10). "Aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombe" (Waebrania 7:25).

Kutokana na Maandiko hayo ni wazi kwamba si mapenzi yake Mungu kwamba wewe uwe na mashaka na kujitesa nafsi yako kwa hofu kwamba Mungu hatakupokea kwa sababu wewe u mwenye dhambi wala hustahili. "Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi" (Yakobo 4:8). Weka tatizo lako mbele zake, ukimsihi sana na kudai wema wa damu ile iliyomwagika kwa ajili yako juu ya msalaba ule wa Kalvari. Shetani atakushtaki wewe kuwa una dhambi nyingi sana, nawe huna budi kukiri hilo, lakini unaweza kusema hivi: "Najua kwamba mimi ni mwenye dhambi, na hiyo ndiyo sababu ninayomhitaji Mwokozi. Yesu alikuja ulimwenguni humu kuwaokoa wenye dhambi. 'Damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote'

(1 Yohana 1:7). 'Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote' (fungu la 9). Mimi sina sifa zo zote wala wema wo wote ambao kwa huo naweza kudai wokovu, lakini nadai mbele zake Mungu damu ile ipatanishayo ya Mwana wa Mungu yule asiyekuwa na waa, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Hilo ndilo ombi langu la pekee. Jina lake Yesu hunipa mimi njia ya kumfikia Baba. Sikio lake, moyo wake, viko wazi kulisikia ombi langu linalotolewa kwa unyonge kabisa, naye ananipa mahitaji yangu ya ndani kabisa."

Huko Ndiko Kuhesabiwa Haki

Ni haki yake Kristo inayomfanya mwenye dhambi yule aliyetubu kukubaliwa na Mungu na kuhesabiwa haki. Haidhuru maisha yake yawe yenye dhambi jinsi gani, akimwamini Yesu kuwa ndiye Mwokozi wake binafsi, anasimama mbele za Mungu katika mavazi yale yasiyo na waa ya haki yake Kristo aliyokwisha kumhesabia.

Mwenye dhambi ambaye hivi karibuni alikuwa amekufa katika makosa na dhambi zake anahuishwa kwa imani yake katika Kristo. Kwa imani yeye anamwona Yesu kuwa ni Mwokozi wake, na kwamba yu hai sikuzote, anaweza kuwaokoa "kabisa [wote] wamjiao Mungu kwa yeye."

Katika upatanisho ule uliofanywa kwa ajili yake, muumini huyo anauona upana na urefu na kimo na kina cha uwezo huo ----- anauona wokovu kamili kama huo, ulionunuliwa kwa gharama isiyokadirika, na moyo wake unajazwa na sifa na shukrani. Anauona kama ni katika kioo utukufu wa Bwana, kisha anabadilishwa na kufanana na sura iyo hiyo kwa Roho wa Mungu. Analiona vazi lile la haki ya Kristo, lililofumwa kule mbinguni, ambalo limetengenezwa kwa utii wake [Kristo], na kuwekwa kwenye akaunti ya mtu yule anayetubu kwa njia ya imani katika jina lake.

Mwenye dhambi huyo anapooona picha ya uzuri ule usiokuwa na kifani wa Yesu, dhambi kwake haionekani tena kuwa ina mvuto wo wote; kwa maana anamtazama yule aliye Mashuhuri miongoni mwa elfu kumi, Ndiye mzuri sana pia pia. Kutokana na uzoefu wa maisha yake anautambua uweza wa injili, ambao upana wa Kiolezo chake uko sawa tu na thamani ya kusudi lake.

Tunaye Mwokozi aliye hai. Hayumo katika kaburi jipya la Yusufu; amefufuka kutoka kwa wafu na kupaa mbinguni akiwa ndiye Badala yetu na Mdhamini wetu kwa kila mtu aaminiye. "Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo" (Warumi 5:1). Mwenye dhambi anahesabiwa haki kwa njia ya wema wake Yesu, na huo ndicho kibali cha Mungu cha fidia ile kamilifu iliyolipwa kwa ajili ya mwanadamu. Kwamba Kristo alikuwa mtii hata mauti ile ya msalaba, hiyo ndiyo ahadi kwa mwenye dhambi ya kukubaliwa na Mungu. Basi, je! tujiachilie wenyewe na kuwa na uzoefu wa maisha [ya Kikristo] unaoyumbayumba wa kuwa na mashaka na kuamini, kuamini na kuwa na mashaka? Yesu ndiye dhamana ya kukubaliwa kwetu na Mungu. Tunasimama katika upendeleo wake mbele za Mungu, si kwa sababu ya wema wo wote ulio ndani yetu, bali kwa sababu ya imani yetu katika "Bwana ni Haki yetu."

Yesu anasimama katika Patakatifu pa Patakatifu, sasa anaonekana mbele za Mungu kwa ajili yetu. "Pale haachi kamwe kuwaombea watu wake dakika kwa dakika, akiwa ametimilika ndani yake mwenyewe. Walakini, kwa kuwa tunawakilishwa hivyo mbele za baba yetu, hatupaswi kutazamia rehema yake [kufanya kazi kwa ajili yetu] bila kuwa na hakika huku tukiwa wazembe, tusiojali, wenye kujifurahisha kwa tamaa zetu za mwili. Kristo si mhudumu wa dhambi. Sisi tumetimilika ndani yake, tumekubalika katika yule Mpendwa, kama tunakaa tu ndani yake kwa imani.

Ukamilifu kwa njia ya matendo yetu mema hatuwezi kuupata. Mtu yule anayemtafuta Yesu kwa imani, anaachana kabisa na haki yake mwenyewe. Anajiona kuwa hajatimilika, toba yake kuwa haitoshi, imani yake thabiti kuwa ni udhaifu tu, kujitolea kwake mhanga anakokuona kuwa kumemgharimu sana kuwa ni gharama ndogo tu, naye anashuka kwa unyenyekevu chini ya msalaba ule. Lakini sauti huzungumza naye kutoka katika mashauri ya Neno la Mungu. Kwa mshangao mkubwa anasikia ujumbe huu, "Ninyi mmetimilika katika yeye." Sasa kila kitu moyoni mwake ni shwari. Hapaswi tena kujitahidi kutafuta kitu fulani ndani yake mwenyewe cha kumfanya ajione kwamba anastahili, yaani, tendo fulani la kumpatia sifa ya kupata upendeleo wa Mungu.

Ukweli Ulio Mgumu Kuuzingatia

Kwa kumtazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu huu, mtu anapata amani ya Kristo; kwa sababu msamaha umeandikwa mbele ya jina lake, na yeye analikubali Neno la Mungu lisemalo, "Ninyi mmetimilika katika yeye" (Wakolosai 2:10). Ni vigumu jinsi gani kwa wanadamu, waliozoea kwa muda mrefu kuwa na mashaka moyoni mwao, kuweza kuuzingatia ukweli huo mkuu! Lakini ni amani ilioje unayoleta moyoni, ni maisha hai yaliyoje! Kule kujiona wenyewe kuwa tuna haki yetu, ambayo kwayo tunaweza kupata nafasi ya kukubaliwa na Mungu, huwa tunatazama mahali pasipokuwa penyewe, "kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23). Yatupasa kumtazama Yesu; kwa maana "sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu" (2 Wakorintho 3:18). Unatakiwa kuupata utimilifu wako kwa kumtazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.

Akiwa amesimama mbele ya Sheria ya Mungu [Amri Kumi] iliyovunjwa, mwenye dhambi hawezi kujiosha [dhambi zake] mwenyewe; ila, kwa njia ya kumwamini Kristo, yeye anakuwa lengo la upendo wake wa milele, naye anavikwa vazi la haki yake lisilo na waa. Kwa wale wanaomwanini Kristo, Yesu aliwaambia hivi: "Uwatakase kwa ile kweli; Neno lako ndiyo kweli.... Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja" (Yohana 17:17-22). "Baba mwenye haki, ulimwengu haukukujua; lakini mimi nalikujua, na hao wamejua ya kuwa ndiwe uliyenituma. nami naliwajulisha jina lako, tena nitawajulisha hilo; ili pendo lile ulilonipenda mimi liwe ndani yao, nami niwe ndani yao" (fungu la 25,26)

Ni nani awezaye kuifahamu asili ya haki ile inayomfanya mwenye dhambi aminiye kuwa mzima, ikimkabidhi kwa Mungu akiwa hana waa, wala kunyanzi, wala lo lote kama hayo? Sisi tunalo Neno la Mungu kama dhamana yetu kwamba Kristo amefanywa kwetu kuwa haki, utakaso, na ukombozi. Mungu na atujalie kulitegemea Neno lake kwa imani thabiti, na kuifurahia mibaraka yake tele. "Kwa maana Baba mwenyewe awapenda kwa kuwa ninyi mmenipenda mimi, na kusadiki ya kwamba mimi nalitoka kwa Baba" (Yohana 16:27).

SURA YA 17

Ushauri kwa Mchungaji Maarufu Kuhusu

Hotuba Yake Juu ya Uhusiano Uliopo

Kati ya Imani na Matendo

Hii ni sehemu ya barua iliyoandikwa kwa A. T. Jones,

Aprili 9, 1893, Letter 44, 1893. Ilichapishwa katika

Selected Messages, Kitabu cha Kwanza, uk. 377-379.

Nilikuwa nahudhuria mkutano fulani, na mkusanyiko mkubwa wa watu ulikuwapo. Katika ndoto yangu, wewe ulikuwa unahubiri juu ya somo la Imani na Haki ya Kristo tunayohesabiwa kwa imani. Ulirudia mara kadhaa kusema kwamba matendo hayakuwa na faida yo yote, kwamba hapakuwa na masharti yo yote. Jambo hilo lilifundishwa kwa nuru ile ambayo mimi nilijua kwamba watu wengi wangeweza kuchanganyikiwa, tena, wasingeweza kupokea picha sahihi kuhusu imani na matendo, nami nikaamua kukuandikia. Unalielezea jambo hilo kwa nguvu mno. Yapo masharti kwetu ili tupate kupokea kuhesabiwa haki na utakaso, na haki ya Kristo. Najua maana yako, lakini wewe unaacha mvuto mbaya juu ya watu wengi. Ingawa matendo mema hayatamwoko mtu hata mmoja, lakini haiwezekani kwa mtu hata mmoja kuokolewa pasipo kuwa na matendo mema. Mungu anatuokoa sisi chini ya kanuni ile isemayo kwamba yatupasa kuomba kama tunataka kupokea, kutafuta kama tunataka kuona, na kubisha kama tunataka mlango ufunguliwe kwetu.

Kristo anajitoa mwenyewe kuwa yuko tayari kuwaokoa kabisa wote wamjiao yeye. Anawaalika wote kuja kwake. "Ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe" (Yohana 6:37). Kwa kweli, wewe unayaangalia masomo haya kama mimi ninavyoangalia, lakini kutokana na usemi wako unayafanya masomo haya kuleta utata kwa watu. Na baada ya kueleza maoni yako yote kimsingi kuhusu matendo, maswali yanapoulizwa kwako juu ya somo lilo hilo, unaliweka si katika maelezo yaliyo dhahiri hata katika mawazo yako mwenyewe, wala huwezi kuzifafanua kanuni hizo sahihi kwa watu wengine, na wewe mwenyewe huwezi kuzifanya semi zako ziweze kupatana na kanuni na imani yako.

Yule mwanaume kijana alikuja kwa Yesu na swali hili, "Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?" (Marko 10:17). Kristo akamwambia, "Kwani kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri. Akamwambia, Zipi? Yesu akazitaja kadhaa [katika zile kumi], na yule mwanaume kijana akamwambia, Haya yote nimeyashika tangu utoto wangu; nimepungukiwa na nini tena?" Yesu akamwambia, "Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuata." Hapa ndipo yalipo masharti yenyewe, na Biblia imejaa masharti. "Yule kijana alipolisikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi" (Mathayo 19:17,20,21,22).

Mambo ya Kujihadhari

Basi, wewe unaposema kwamba hakuna masharti yo yote, na maneno yako mengine yanaelezwa kwa upana sana, unawalemea sana watu, na wengi hawaoni ulinganifu wa maneno yako. Hawawezi kuona kwa jinsi gani wanaweza kuyasuluhisha maneno hayo na semi zile zilizo wazi za Neno la Mungu. Tafadhali jihadhari na mambo hayo. Madai yako yenye nguvu kuhusu matendo hayaufanyi msimamo wetu kuwa na nguvu zaidi. Maneno hayo huudhoofisha msimamo wetu, kwa kuwa wapo wengi watakaokufikiria wewe kuwa una msimamo mkali sana, na hao watapoteza mafundisho hayo ya thamani uliyo nayo kwao juu ya masomo yayo hayo wanayohitaji kuyajua... Kaka yangu, ni vigumu kwa akili kulielewa jambo hili, wala usimchanganye mtu ye yote kwa maoni yako yale yasiyoweza kupatana na Neno. Tafadhali fikiria kwamba chini ya mafundisho yake Kristo wengi wa wanafunzi wake walikuwa wajinga kwa kiwango cha kusikitisha; lakini Roho Mtakatifu, ambaye Yesu alikuwa ameahidi, alipokuja juu yao na kumfanya Petro, mwenye msimamo unaoyumbayumba kuwa shujaa wa imani, ni badiliko lililoje lililotokea katika tabia yake! Lakini wewe usiweke changarawe moja mbele ya mtu mmoja aliye dhaifu na kumfanya ajikwae juu yake, kwa njia ya hotuba au maneno yako yanayochosha mno. Uwe na ulinganifu, uwe mtulivu, mwenye kwenda chini kwa kina, na thabiti. Usizidi kiasi katika jambo lo lote, lakini weka miguu yako juu ya mwamba ule imara. Mwokozi huyo ni wa thamani sana! "Yeye aliye na amri zangu [kumi], na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake" (Yohana 14:21).

Hicho ndicho kipimo halisi ----- yaani, kuyatenda maneno ya Kristo. Tena, huo ndio ushahidi wa upendo kwa Yesu utokao kwa mjumbe wake wa kibinadamu, na yule anayeyafanya mapenzi yake [Mungu] anaupa ulimwengu huu ushahidi kwa njia ya matendo yake wa matunda yale anayoyadhihirisha kwa utii wake, usafi wake, na utakatifu wa tabia yake....

Ee kaka yangu, tembea kwa uangalifu na Mungu wako. Lakini kumbuka kwamba kuna baadhi ya watu ambao macho yao yamekazwa kwa makusudi juu yako, wakitarajia kwamba utauvuka mstari ule [wa ile kweli] na kujikwaa na kuanguka. Lakini kama kwa moyo wa unyenyekevu wewe unakaa karibu sana na Yesu, basi, yote ni salama....

Hakuna hatua yo yote katika shule ya Kristo tunapoweza kusema tumehitimu. Yatupasa kufanya kazi yetu kwa mpango ule wa kuongeza, na Bwana naye atafanya kazi yake kwa mpango ule wa kuzidisha. Ni kwa njia ya bidii inayoendelea daima, kwa neema yake Kristo, sisi tunaweza kuishi kwa mpango ule wa kuongeza, tukikufanya imara kuitwa kwetu na uteule wetu.... "Maana mkitenda hayo hamtajikwa kamwe. Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo" (2 Petro 1:10,11).

SURA YA 18

Mwanadamu Anaweza Kuwa Mtakatifu

Katika Mazingira Yake Kama Vile

Mungu Alivyo Mtakatifu

Katika [Mazingira] Yake

Hii ni sehemu ya makala yenye kichwa cha "Hujitakasa"

ambayo ilitolewa katika gazeti la Signs of the Times,

Juni 20, 1895.

"Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo" (1 Yohana 3:2). Urithi wa watu wa Mungu unafahamika kwa njia ya imani katika Neno la Mungu. "Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma" (Yohana 17:3).

Kwa njia ya imani watoto wa Mungu wanajipatia maarifa ya kumjua Kristo na kulihifadhi tumaini lao la kuja kwake kuuhukumu ulimwengu huu kwa haki, mpaka hapo litakapogeuka na kuwa tumaini lenye utukufu; kwa maana wakati huo watamwona kama alivyo na kufanana naye, na kuwa pamoja na Bwana milele. Watakatifu wanaolala [mauti makaburini], wakati huo wataitwa na kutoka makaburini mwao kupewa miili ya utukufu, isiyokufa. Siku ile ya ukombozi itakapofika, hapo ndipo ninyi mtakaporudi na kupambanua kati ya yeye amtumikiaye Mungu na yeye asiyemtumikia. Kristo atakapokuja, itakuwa ni kwa kutamaniwa [waovu watawatamani sana] wale wote waaminio, na falme za ulimwengu huu zitakuwa ufalme wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo.

Wale wanaotarajia ufunuo wake [kutokea kwake] Kristo katika mawingu ya mbinguni kwa nguvu na utukufu mkuu, kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, katika maisha yao na tabia zao watajaribu kumwakilisha katika ulimwengu huu. "Na kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu" (1 Yohana 3:3). Wataichukia dhambi pamoja na maovu yote, kama vile Kristo alivyoichukia dhambi. Watazishika amri [kumi] za Mungu, kama vile Kristo alivyoizishika amri [kumi] za Baba yake. Watatambua kwamba haitoshi tu kuyakubali mafundisho ya kweli hiyo, bali kwamba kweli hiyo ni lazima itumiwe moyoni mwao, na kuwekwa katika matendo maishani mwao, ili wafuasi wa Kristo wapate kuwa umoja naye, na kwamba watu wawe watakatifu katika mazingira yao kama vile Mungu alivyo mtakatifu katika [mazingira] yake.

Si Wasikiaji Tu, Bali Watendaji

Kumekuwako na watu katika kila kizazi waliodai kwamba wao ni wana wa Mungu, ambao walilipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini walioishi maisha ya kikafiri, kwa sababu waliyaacha mambo makuu ya Sheria [Amri Kumi] ----- rehema, haki, na upendo wa Mungu.

Leo wako wengi walioingia katika udanganyifu kama huo; kwa maana wakati wanaonyesha utakatifu mwingi [kwa nje], hao si watendaji wa Neno la Mungu. Ni jambo gani basi, linaloweza kufanyika ili kuyafumbua macho ya watu hao wanaojidanganya wenyewe kama sio kuweka mbele yao mfano wa utauwa wa kweli na sisi wenyewe kutokuwa wasikiaji tu bali watendaji wa amri [kumi] za Bwana, kwa njia hiyo twaweza kuiakisi [kuiangaza] nuru takatifu ya tabia yetu katika njia yao.

Si Kama Walimwengu

Wana wa Mungu hawatafanana na walimwengu; maana kweli ile iliyopokewa moyoni mwao itakuwa ndiyo njia ya kuutakasa moyo wa mtu na kuibadilisha tabia yake na kumfanya yule mpokeaji kuwa na nia inayofanana na ile ya Mungu. Mtu asipokuwa na nia inayofanana na ile ya Mungu, basi, yeye yu ngali bado katika tabia yake potofu ya asili [ya kuzaliwa nayo].

Kristo akiwa moyoni, basi, ataonekana nyumbani, kwenye karakana, sokoni, na kanisani. Uwezo wa ile kweli utaonekana katika kuikuza na kuiadibisha akili na kuulainisha na kuutiisha moyo, ukimleta mtu mzima katika umoja na Mungu. Yule aliyebadilishwa na ile kweli ataiangaza nuru yake ulimwenguni. Yule aliye na tumaini la Kristo ndani yake atajitakasa kama yeye [Mungu] alivyo mtakatifu. Tumaini la kuja kwake Kristo ni tumaini kuu, lenye athari nyingi. Ni tumaini la kumwona Mfalme katika uzuri wake na kufananishwa naye.

Kristo atakapokuja dunia hii itatetemeka mbele zake, na mbingu zitakunjwa kama karatasi, na kila mlima na kila kisiwa kitaondolewa mahali pake. "Mungu [Kristo] wetu anakuja wala hatanyamaza, Moto utakula mbele zake, na tufani yavuma sana ikimzunguka pande zote. Ataziita mbingu zilizo juu, Na nchi pia awahukumu watu wake. Nikusanyieni wacha Mungu wangu waliofanya agano nami kwa dhabihu [1 The.4:15-17(18); Mt. 24:30,31]. Na mbingu zitatangaza haki yake [Amri Kumi zitaonekana mbinguni], kwa maana Mungu ndiye aliye hakimumu" (Zaburi 50:3-6). Kwa sababu ya siku ile [kuu] ya Mungu, tunaweza kuona ya kwamba usalama wetu pekee utapatikana katika kuachana na dhambi zote pamoja na maovu yote. Wale wanaoendelea katika dhambi wataonekana miongoni mwa wale waliohukumiwa adhabu na kuangamizwa.

Mwisho wa Waasi

Yohana aliuona mwisho wa wale wanaoichagua njia ya uasi [uvunjaji wa Amri Kumi], anasema: "Na wafalme wa dunia [Ma-Rais], na wakuu, na majemadari [Mameja Jenerali], na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana, wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima, wakiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na Hasira ya Mwana-Kondoo [Ufu. 14:9,10,17-20; 15:1; 16:1-21;

19:11-21]. Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao imekuja; naye ni nani awezaye kusimama? [Silaha za nyuklia hazitakuwa na kazi]" (Ufunuo 6:15-17).

Maangamizi ya kutisha sana yanamngojea mwenye dhambi [asiyetubu], na hivyo ni muhimu kwetu kwamba tujue dhambi ni nini, ili tupate kujiepusha na uwezo wake. Yohana asema hivi, "Kila mtu atendaye dhambi anavunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi], maana dhambi ni uvunjaji wa Sheria [Amri Kumi]." (1 Yohana 3:4, AJKK). Hapa tuna tafsiri sahihi ya dhambi; ni "uvunjaji wa Sheria [Amri Kumi]." Ni mara ngapi mwenye dhambi anasihwa sana kuachana na dhambi zake [uvunjaji wake wa Amri Kumi], na kuja kwa Yesu; lakini, je! mjumbe yule aliyetumwa kwake amefanikiwa kumleta kwa Kristo kwa kumwonyesha njia ile iliyo wazi? Je! ameonyesha waziwazi ukweli kwamba "dhambi ni uvunjaji wa Sheria [Amri Kumi]," na ya kwamba anapaswa kutubu na kuacha kuzivunja amri [kumi] za Mungu?...

Mungu asingeweza kubadili hata yodi [,] moja wala nukta [,] moja ya Sheria yake takatifu [Amri Kumi] ili kuafikiana na mwanadamu katika hali yake ya kuanguka; maana jambo hilo lingemfedhehesha sana Mungu kuhusu hekima yake katika kuitoa Sheria hiyo [Amri Kumi] ambayo kwayo anaitawala mbingu na dunia hii. Lakini Mungu aliweza kumtoa Mwanawe pekee kuwa Badala ya mwanadamu na kuwa Mdamini wake, kupata adhabu aliyostahili kupata yule mvunja Sheria [Amri Kumi], na kumpa mwanadamu aliyetubu haki yake kamilifu. Kristo akawa Kafara isiyo na dhambi kwa ajili ya wanadamu wenye dhambi, akiwafanya wanadamu kuwa wafungwa wenye matumaini, ili kwa njia ya toba kwa Mungu kwa sababu walikuwa wameivunja Sheria yake takatifu [Amri Kumi], na kwa njia ya imani katika Kristo kama [mmoja aliye] Badala yao, Mdamini wao, na Haki yao, wangeweza kurudishwa katika uaminifu wao kwa Mungu na utii wao kwa Sheria yake takatifu [Amri Kumi].

Haki ya Kristo Hufanya Utii Uwezekane

Ilikuwa haiwezekani kabisa kwa mwenye dhambi kuishika Sheria ya Mungu [Amri Kumi], ambayo ni takatifu, ya haki, na njema [Warumi 7:12]; lakini kutowezekana huko kuliondolewa kwa kutoa Haki yake Kristo kwa mtu yule anayetubu na kuamini. Maisha na kifo chake Kristo kwa ajili ya mwanadamu mwenye dhambi ilikuwa ni kwa kusudi la kumrejsha mwenye dhambi huyo katika upendeleo wake Mungu, kwa kumpa haki ambayo ingetimiza [ingekidhi] madai ya Sheria [Amri Kumi] na kukubalika kwa Mungu.

Lakini daima ni kusudi lake Shetani kuitangua [kuifutilia mbali - Ufu. 12:7-9,12,17] Sheria ya Mungu [Amri Kumi] na kupotosha maana ya kweli ya mpango ule wa wokovu. Kwa hiyo ameanzisha uongo kwamba Kafara ya Kristo juu ya msalaba ule wa Kalvari ilikuwa kwa kusudi la kuwaweka watu huru wasiwajibike kuzishika amri [kumi] za Mungu. Ameughilibu akili ulimwengu huu kwa madanganyo yake akisema kwamba Mungu ameitangua Katiba yake [Amri Kumi], yaani, ameitupilia mbali Kanuni yake ya Maadili [Amri Kumi], na kuitangua Sheria yake takatifu na kamilifu [Amri Kumi]. Angekuwa amefanya hivyo [Mungu], basi, ingekuwa gharama ya kutisha jinsi gani kwa Mbingu! Badala ya yeye [Mungu] kutangaza kwamba ameitangua

[ameifutulia mbali] Sheria yake [Amri Kumi], msalaba ule wa Kalvari unatangaza kwa sauti kama za ngurumo kwamba kulingana na tabia yake [Sheria hiyo ya Amri Kumi] haiwezi kubadilika na kwamba inadumu milele. Kama Sheria hiyo [Amri Kumi] ingeweza kufutuliwa mbali, na wakati uo huo Serikali ile ya mbinguni na duniani na dunia zingine za Mungu zisizohesabika ingeweza kuimarishwa, basi, Kristo asingekuwa na haja yo yote ya kufa. Kifo chake Kristo kilikuwa kwa ajili ya kuamua kwa milele zote hoja ya uthabiti wa [kudumu kwa] Sheria yake Yehova [Amri Kumi]. Baada ya kupata adhabu kamili kwa ajili ya ulimwengu huu wenye dhambi [uliovunja Amri Kumi], Yesu akawa Mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu, ili kumrejsha mwenye dhambi [mvunja Sheria] atubuye katika upendeleo wa Mungu kwa kumpa neema ya kumwezesha kuishika Sheria hiyo [Amri Kumi] ya yule Aliye Juu. Kristo hakuja kuivunjilia mbali Sheria [torati], wala manabii, bali kuitimiliza [kuitekeleza] kabisa [Mt. 5:17-19; Luka 16:17]. Upatanisho ule uliotolewa pale Kalvari uliithibitisha Sheria ya Mungu [Amri Kumi] kuwa ni takatifu, ya haki, na ya kweli [Warumi 7:12; 3:31; Zaburi 119:142], sio tu mbele ya ulimwengu wetu huu ulioanguka [dhambini] bali mbele ya mbingu na mbele ya dunia zile nyingine [zenye watu - Ayubu 1:6-8] ambazo hazikuanguka [dhambini]. Kristo alikuja kuitukuza [kuiinua juu] Sheria [Amri Kumi] na kuiadhimisha (kuitunza au kuishika - Yohana 15:10). [Isaya 42:21.]

SURA YA 19

Maoni Yetu na Desturi Zetu

Ni Lazima Zipatane na Neno la Mungu

Imechaguliwa kutoka katika makala ya gazeti la Review
and Herald, Machi 25, 1902.

Kuna wengi wanaodai kwamba wao wametakaswa na Mungu, lakini Kanuni ile Kuu ya Haki [Amri Kumi] inapohubiriwa kwao wanakasirika sana na kuonyesha roho inayothibitisha kwamba hawajui kitu cho chote juu ya maana ya kutakaswa. Hawana roho ile ya Kristo; kwa maana wale waliotakaswa kweli kweli wataliheshimu sana na kulitii upesi Neno la Mungu kadiri linavyozidi kufunuliwa kwao, tena wataonyesha shauku kubwa ya kujua kweli ni nini kwa kila fundisho. Hisia ya furaha kuu moyoni si ushahidi wa utakaso. Madai haya ya kusema, "Mimi nimeokoka, mimi nimeokoka," hayathibitishi kwamba mtu huyo ameokolewa ama ametakaswa.

Wengi wanaopata msisimko mkubwa wanaambiwa kwamba wametakaswa, wakati wao hawana wazo lo lote la busara kuhusu [hawaelewi] maana ya neno hilo, kwa vile hawayajui Maandiko wala uweza wa Mungu. Wanajisifu wenyewe kwamba wanapatana kabisa na mapenzi ya Mungu kwa sababu wanajisikia furaha; lakini wanapojaribiwa [wanapopimwa], yaani, Neno la Mungu linapoletwa kuupima uzoefu wao huo, basi, wao wanayaziba masikio yao wasiisikie kweli, huku

wakiendelea kusema, "Mimi nimetakaswa," na maneno hayo yanazima majadiliano yote. Hawataki kabisa kujishughulisha wala kuyachunguza Maandiko ili kujua kweli ni nini; nao huonekana ya kuwa wamejidanganya wenyewe vibaya sana. Utakaso una maana zaidi ya kuwa na hisia ya furaha inayopita ghafula moyoni.

Misisimko sio utakaso. Kupatana kabisa na mapenzi ya Baba yetu aliye mbinguni ndio utakaso peke yake, na mapenzi ya Mungu yamefunuliwa katika Sheria yake takatifu [Amri Kumi]. Kuzishika amri zote [kumi] za Mungu huo ndio utakaso. Kujionyesha kwamba ninyi ni watoto watiifu wa Neno la Mungu huo ndio utakaso. Neno la Mungu linatakiwa kuwa kiongozi chetu, sio maoni wala mawazo ya wanadamu. Hebu wale wanaotaka kutakaswa kweli kweli na walichunguze Neno la Mungu kwa uvumilivu, kwa maombi, na kwa unyenyekevu na majuto moyoni. Hebu na wakumbuke kwamba Yesu aliomba hivi, "Uwatakase kwa ile kweli; Neno lako ndiyo kweli" (Yohana 17:17).

Kuishi Kwa Kila Neno La Mungu

Ukristo ni kuishi tu kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu [Biblia]. Yatupasa kuamini na kuishi ndani ya Kristo, ambaye ndiye Njia, Kweli, na Uzima. Tunayo imani kwa Mungu tunapoliamini Neno lake; tunamtumaini na kumtii Mungu tunapozishika amri zake [kumi]; nasi tunampenda Mungu tunapoipenda Sheria yake [Amri Kumi].

Kule kuuamini uongo [mafundisho potofu] hakutumfanya mtu ye yote miongoni mwetu kuwa katika njia ile ya kupata utakaso. Wachungaji wote ulimwenguni wangetuambia sisi kwamba tuko salama kwa kutoitii amri moja ya Kanuni hiyo takatifu ya Haki [Amri Kumi], basi, jambo hilo lisingepunguza uwajibikaji wetu wala kuifanya hatia yetu kuwa pungufu, endapo sisi tunakataa kutii amri iliyo wazi isemayo "Ufanye hivi" au "Usifanye hivi." Hatuna haja ya kuwaza kwamba kwa sababu baba zetu walifanya mambo yao kwa njia fulani na kufa kwa furaha, basi, sisi tunaweza kufuata nyayo zao na kukubalika [na Mungu] kutoa huduma ile ile na kufanya matendo yale yale waliyofanya wao.

Sisi tunayo nuru nyingi sana kuliko ile waliyokuwa nayo wao katika siku zao; na kama tunataka kukubaliwa na Mungu, basi, yatupasa kuwa waaminifu katika kuitii nuru tuliyo nayo na kwenda katika hiyo kama vile wao walivyokuwa katika kuipokea na kuitii nuru aliyowapelekea Mungu. Yatupasa kuipokea na kuitumia vizuri nuru inayoangaza katika njia yetu kwa uaminifu kama vile wao walivyoipokea na kuitumia vizuri nuru ile iliyowaangazia katika njia yao kwa kizazi chao. Tutahukumiwa kulingana na nuru ile inayoangaza katika hekalu la mwili wetu katika siku hizi zetu; na kama tutaifuata nuru hiyo, basi, tutakuwa wanaume na wanawake walio huru [kweli kweli] katika Kristo Yesu.

